# Nipashe

Ijumaa Machi 15, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 - Na. 0579866

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

om/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Askari Polisi afia baa akiwa amelewa chakari

UKURASA 3




UKURASA 13

# Spika afunguka kufyeka mshahara, posho za Lissu

UKURASA 2



## YALIYOMO


UKURASA WA 3

**MABILIONI YAOKOLEWA MATIBABU YA FIGO NJE**

SERIKALI imesema imeokoa Sh. bilioni 3.4 ambazo zingetumika...

UKURASA WA 3

**MBOWE, WENZAKE WASOMEWA UPYA MASHTAKA**

VIGOGO tisa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema)...


## Joshua Nassari apoteza ubunge

UKURASA 2




Mkurungenzi wa Mashtaka nchini (DPP), Biswalo Mganga, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma jana, wakati akitangaza kufutiwa kesi ya mauaji namba 8 ya mwaka 2018, kwa watuhumiwa Musa Sadiki na Edward Matiku. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# DPP awaumbua Polisi

• **Asimulia** walivyombambika mfanyabiashara kesi ya mauaji baada ya kumpoka fedha zake... *Ukurasa 2*


TAIFA STARS vs UGANDA

MACHI 24, 2019 • UWANJA WA TAIFA




18+ TAFADHALI KUNYWA KISTAARABU

xxxxxx

HABARI KITAIFA

# Joshua Nassari avuliwa ubunge

**Na Romana Mallya**

BUNGE limetangaza kuwa Mbunge wa Arumeru Mashariki (Chadema), Joshua Nassari, amepoteza sifa za kuwa Mbunge kutokana na kutohudhuria mikutano mitatu mfululizo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana jioni na Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa cha Bunge, Spika wa Bunge Job Ndugai, amemwandikia barua Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Jaji Semistocles Kaijage, kuwaarifu kuwa Jimbo la Arumeru Mashariki liko wazi.

Nipashe ilipomtafuta Mkurugenzi wa Uchaguzi wa NEC, Dk. Athuman Kihamia, kuhusu barua hiyo kama wameipokea, alisema: "Ni kweli tumeipokea barua hiyo leo (jana) kutoka bungeni na tumeanza mchakato kumpata mbunge mpya."

Dk. Kihamia alisema sheria inasema mwisho wa kuzibwa nafasi ni miezi 12 kabla ya Bunge la mwisho linalotarajia kuvunjwa Julai, mwakani. Taarifa ya Bunge ilibainisha kuwa jimbo la Arumeru Mashariki linaloongozwa na Nassari kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) liko wazi kutokana na mbunge huyo kupoteza sifa.

Pia taarifa hiyo ilisema Nassari amepoteza sifa hiyo kwa kutohudhuria mfululizo mikutano ambayo ni mkutano wa 12 wa Septemba 4 hadi 14, mwaka jana, mkutano wa 13 wa Novemba 6 hadi 16 na mkutano mwaka 2018.

Pia taarifa hiyo ilisema Nassari hakuhudhuria mkutano wa 14 uliofanyika kuanzia Januari 29 hadi Februari 9, mwaka huu.

"Uamuzi huu wa Spika umezingatia masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 71 (1) (c). Ibara hii inaeleza kuwa, 'Mbunge atakoma kuwa Mbunge na ataacha kiti chake katika Bunge ikiwa atakosa kuhudhuria vikao vya mikutano ya Bunge mitatu mfululizo bila ya ruhusa ya Spika,'" ilisema taarifa hiyo.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa Ibara hiyo imefafanua katika Kanuni ya 146 (1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Januari, 2016. "Kanuni hiyo inaeleza kuwa, 'Kuhudhuria vikao vya Bunge na Kamati zake ni wajibu wa kwanza wa Mbunge. Mbunge yeyote atakayeshindwa kuhudhuria mikutano ya Bunge mitatu mfululizo bila ruhusa ya Spika iliyotolewa kwa maandishi, atapoteza ubunge wake na Spika ataiarifu NEC," ilisema.

Aidha, taarifa hiyo ilisema tume ya uchaguzi inaweza kuendelea na mchakato wa kumpata mbunge wa kujaza nafasi hiyo iliyo wazi ya Jimbo la Arumeru Mashariki.

# Spika afunguka kufyekwa posho, mshahara wa Lissu

**Na Romana Mallya**

MBUNGE wa Singida Mashariki, Tundu Lissu, amelilalamikia Bunge kusitisha mshahara wake na posho tangu Januari, mwaka huu, huku Spika Job Ndugai akiahidi kulitolea ufafanuzi suala hilo.

Taarifa iliyoandikwa na Lissu jana kwenye mitandao ya kijamii, ilisema Bunge limesitisha mshahara na posho zake tangu Januari na kwamba lilifanya hivyo kabla ya mwongozo kutolewa bungeni.

Alisema mwongozo uliombwa baadaye ili kuhalalisha uamuzi ambao ulikwishafanyika.

Nipashe ilipomtafuta Spika Ndugai ili kuzungumzia suala hilo, aliahidi kutoa taarifa kuhusu malalamiko hayo ya Lissu.

"Sijasikia wala kuona kama Lissu amesema hayo ila nimepigiwa simu na wenzako wakiniambia Lissu amezungumza kuwa Bunge limesitisha mshahara na posho zake," alisema na kuongeza:

"Naomba mumuulize Lissu swali hili kama mwajiri hajakupa mshahara unaodai je, unakimbilia kwenye mitandao ya kijamii au utazungumza na mwajiri wako kwa taratibu zilizowekwa? Hata hivyo nitatoa taarifa," alisema.

Ndugai alisema Lissu anatakiwa kueleza lini alijadiliana na mwajiri wake kuhusu kusitishiwa mshahara na posho.

Katika Mkutano wa Bunge uliopita, Mbunge wa Geita Vijijini (CCM),

INAENDELEA UK. 8




Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi (CUF), Profesa Ibrahim Lipumba, (katikati), akiwaongoza viongozi waandamizi kuimba wimbo wa chama wakati wa mkutano mkuu wa saba wa Taifa wa uchaguzi wa chama hicho unaofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

KILIMANJARO CO-OPERATIVE BANK LTD

TAARIFA KWA UMMA

KILIMANJARO CO OPERATIVE BANK LTD INAPENDA KUWAJULISHA WATEJA WAKE AMBAO NI WADAIWA SUGU WA MIKOPO KWA KIPINDI CHA KUANZIA MWAKA 2005 HADI 2018 KUFIKA BENKI KWA AJILI YA KULIPA MIKOPO YAO.

BAADA YA SIKU 14 TOKA TAREHE YA TANGAZO HILI, BENKI ITALAZIMIKA KUCHUKUA HATUA KALI ZA KISHERIA KWA WALE WOTE AMBAO HAWATATEKELEZA IKIWA NI PAMOJA NA KUTANGAZA MAJINA YAO NA KUWAFUNGULIA MASHITAKA.

*TAFADHALI ZINGATIA*

215116102

MAWASILIANO: 0754 743385, 0752 364740
BARUA PEPE: info@kilicobank.com

# DPP awaumbua polisi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

OFISI ya Mkurugenzi wa Mashitaka (DDP), imeliumbua Jeshi la Polisi baada ya kueleza baadhi ya askari wake walivyombambika kesi ya mauaji mfanyabiashara Mussa Adam Sadiki baada ya kumpoka fedha.

Kutokana na kadhia hiyo, Rais John Magufuli ameagiza hatua zaidi zichukuliwe dhidi ya wote waliohusika katika tukio la kumbambika kesi ya mauaji namba 8/2018 mfanyabiashara huyo.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma jana, DPP Biswalo Mganga, alisema Machi 6, mwaka huu, Sadicki aliandika barua ya wazi kwa Rais Magufuli kupitia moja ya magazeti ya kila siku nchini, akilalamika kubambikwa kesi hiyo mkoani Tabora.

Mganga alieleza kuwa baada ya mfanyabiashara huyo kukamatwa na askari polisi, walimnyang'anya Sh. 788,000, simu ya mkononi na mali alizokuwa amenunua kwa ajili ya wakulima wakati anakwenda kufanya ununuzi.

"Kwa mujibu wa malalamiko yake yaliyoandikwa kwenye gazeti tajwa, baada ya kukamatwa aliwekwa kwenye Kituo Kikuu cha Polisi Tabora kwa kumbambikia kesi ya kuvunja na kuiba na alikaa kituoni kwa juma moja na alipopelekwa mahakamani, alisomewa shitaka la mauaji," alisema Mganga.

Mkurugenzi huyo alisema baada ya Rais kusoma barua hiyo, aliagiza Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ifuatilie malalamiko ya mwananchi huyo kwa haraka ili kujua ukweli wake.

"Baada ya maelezo hayo, Ofisi ya Taifa ya Mashitaka ilifuatilia suala hilo na kufanya mahojiano na mlalamikaji pamoja na kupitia nyaraka mbalimbali zilizopo katika Kituo cha Polisi cha Tabora Mjini zinazohusiana na suala lake," alisema.

Katika kufuatilia malalamiko hayo, Mganga alisema ofisi hiyo imebaini malalamiko ya mfanyabiashara huyo ni ya kweli kwa kuwa kitabu cha kuzuia wahalifu (detention register) kilichoko katika kituo hicho cha polisi kinaonyesha Sadick alikamatwa Juni 21, 2018 kwa kosa la kuvunja nyumba usiku na kuiba na aliingizwa mahabusu ya polisi saa tisa alasiri.

Alisema kitabu hicho pia kinaonyesha Juni 29, 2018, mlalamikaji alitolewa mahabusu saa mbili asubuhi na kupelekwa mahakamani na tarehe hiyohiyo, alifunguliwa kesi ya mauaji namba 8/2018 ikionyesha Mei 6, 2018, akiwa Barabara ya Kazima, Tabora Mjini, alimuua Jackson Thomas.

Mganga alisema wakati wa kufuatilia malalamiko hayo, ofisi yake ilibaini kuwa Julai Mosi, 2018, alikamatwa Edward Matiku Nduli kwa kosa la kuvunja nyumba usiku na kuiba. Julai 16, 2018 naye aliunganishwa katika shauri la mauaji namba 8/2018 akihusishwa na mauaji dhidi ya Jackson Thomas.

"Baada ya kubaini hayo, mnamo

INAENDELEA UK. 8

## HABARI KITAIFA

# Askari polisi afia baa akiwa amelewa chakari

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

ASKARI Polisi mkoani Ruvuma, amekutwa amekufa kwenye baa ya Friend's Pub iliyoko katikati ya mji wa Songea huku ikielezwa kuwa alikuwa amekunywa pombe kupindukia.

Akizungumza na waandishi wa habari jana ofisini kwake, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Simon Marwa, alimtaja askari polisi aliyekutwa amekufa kuwa ni Konstebo Donald Motoulaya (29), ambaye ni askari katika ofisi ya Kamanda wa Polisi wa Mkoa.

Alisema ilidaiwa kuwa siku ya tukio hilo, juzi majira ya saa 4:15 asubuhi, Jaibu Nyoni (26) ambaye ni mhudumu wa baa hiyo, alitoa taarifa kwenye Kituo Kikuu cha Polisi kuwa askari Donald amelala kwenye kochi na amejaribu kumwamsha lakini imeshindikana.

Kamanda Marwa alifafanua zaidi kuwa baadaye askari waliongozana na daktari kwenda eneo la tukio ambako walimkuta askari huyo akiwa amelala kwenye kochi ambalo liko ndani ya baa hiyo.

Marwa alisema katika uchunguzi ilibainika kuwa askari huyo alifika kwenye baa hiyo Machi 12, majira ya saa 4:30 usiku akitokea katika baa nyingine iitwayo Mtini Pub ambako alikuwa akinywa pombe.

Alisema mtoa taarifa alieleza kwamba wakati askari huyo anaingia Friend's Pub, aliteleza na kuanguka kwenye ngazi na baadaye alimwinua na kumtoa nje kisha askari huyo alirejea na kukaa kwenye kochi wakati huo mhudumu akiendelea kuhudumia wateja.

"Ilipofika majira ya saa 4:15 asubuhi jana (juzi), wahudumu wakiwa wanafanya kazi za usafi, ndipo walipomwona PC Donald akiwa kwenye kochi wakidhani amelala lakini walipojaribu kumwamsha hakuamka ndipo walipotoa taarifa polisi.

Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Ruvuma, Dk. Hassan Lumbe, alipohojiwa na waandishi wa habari kuhusu tukio hilo, alisema mwili wa askari huyo ulifikishwa hospitalini hapo na watu ambao hawakujitambulisha na ulipokewa na mganga wa zamu.

Dk. Lumbe alifafanua kuwa baada ya kufanya uchunguzi wa kitabibu ilionekana kuwa askari huyo ameshafariki dunia muda mrefu uliopita na kwamba uchunguzi huo ulionyesha hakuwa na mchubuko wowote isipokuwa kulikuwa na mchubuko mdogo kwenye shavu la kushoto.

Alisema baadaye walipohojiwa watu waliomleta walidai kuwa alikuwa amekunywa kiasi kikubwa cha pombe, hivyo uchunguzi wa kitaalam wa sababu ya kifo chake ni kwamba alikuwa amekunywa pombe kwa kupindukia.

# Mabilioni yaokolewa matibabu ya figo nje

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema imeokoa Sh. bilioni 3.4 ambazo zingetumika kugharamia matibabu ya wagonjwa wa figo 42 nje ya nchi tangu ianze kutoa matibabu hayo nchini.

Vilevile, imesema matumizi ya dawa za kutuliza maumivu mara kwa mara, ni miongoni mwa vitu vinavyochangia uharibifu wa figo.

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, aliyasema hayo jijini Dodoma jana alipozungumza kwenye maadhimisho ya Siku ya Figo Duniani.

Alisema hadi sasa, katika Hospitali ya Taifa Muhimbili jijini Dar es Salaam na Hospitali ya Benjamin Mkapa jijini Dodoma, wagonjwa waliopandikizwa figo ni 42.

"Kati yao, 38 wamepatiwa huduma Hospitali ya Taifa Muhimbili na wanne Hospitali ya Benjamin Mkapa," alisema.

Alisema kuwa kama wangepelekwa nje ya nchi, ingeigharimu serikali Sh. bilioni 4.2 wakati huduma hiyo nchini inagharimu kiasi cha Sh. milioni 21 kwa kila mgonjwa, hivyo ingekuwa Sh. milioni 882, hivyo kiasi kilichookolewa ni Sh. bilioni 3.4.

Alisema upatikanaji wa huduma za upandikizaji figo nchini umepunguza gharama kubwa ambazo serikali ilikuwa inalipa kupeleka wagonjwa nje ya nchi.

INAENDELEA UK. 8

# Mbowe, wenzake wasomewa upya mashtaka

**Na Hellen Mwango**

VIGOGO tisa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), wanaokabiliwa na kesi ya uchochezi na kufanya mkusanyiko usio halali akiwamo Mwenyekiti Taifa wa chama hicho, Freedman Mbowe, wamesomewa upya mashtaka.

Washtakiwa hao walisomewa mashtaka hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba.

Hakimu Simba alisema amepangiwa kusikiliza kesi hiyo baada ya hakimu wa awali kuhama kituo cha kazi na sasa jalada limehamishiwa mbele yake.

"Kwa kuwa kesi hii imehamishiwa kwangu washtakiwa watakumbushwa kwa kusomewa mashtaka yao upya kabla ya kuendelea kusikiliza ushahidi wa Jamhuri na tutaanza Machi 28 na 29, mwaka huu "alisema Hakimu Simba.

Mapema mahakamani hapo upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili wa Serikali Simon Wankyo akisaidiana na Wakili wa Serikali Mwandamizi Patrick Mwita, ulidai kuwa washtakiwa wote wapo na kesi hiyo imepangwa kwa ajili ya kutajwa.

Wankyo aliwakumbusha washtakiwa mashtaka yao na wote kwa nyakati tofauti waliyakana.

Upande wa Jamhuri uliomba mahakama kurejea amri ya Mahakama Kuu iliyokuwa imeketi chini ya Jaji Rumanyika Machi 7, mwaka huu, kwamba kesi hii iendelee kusikilizwa.

"Mheshimiwa tunaomba tarehe ya kusikiliza ushahidi wa Jamhuri ili tuanze kuita mashahidi,"alidai Wankyo.

Upande wa utetezi ukiongozwa na jopo la mawakili Profesa Abdalah Safari, Jeremiah Mtobesya, Hekima Mwasipu, Peter Kibatala na John Mallya, uliomba mahakama ipange tarehe za kusikiliza bila kuingiliana na ratiba zao za Mahakama Kuu.

"Tumeshalipwa na wateja mheshimiwa hakimu hatuwezi kuacha kwenda kusikiliza kesi Mahakama Kuu kwa ajili ya kesi hii moja," alidai Profesa Safari.

Hata hivyo, Hakimu Simba alisema mahakama yake haiwezi kufanya kazi kwa kufuata ratiba ya utetezi.

INAENDELEA UK. 8

IFAD
Investing in rural people

FARM RADIO
INTERNATIONAL

**CALL FOR EXPRESSION OF INTEREST**

**Terminal Evaluation of Up-scaling of Interactive Information and Communication Technologies to Increase Uptake of Agricultural Innovations in Tanzania (UPTAKE) Project**

**1.0 Background**

Farm Radio International (FRI) is a Canadian non-profit organization that is at the forefront of using radio combined with other ICTs to serve smallholder farmers. The **Up-scaling of interactive information and communication technologies to increase uptake of agricultural innovations in Tanzania** (UPTAKE) project is funded by IFAD and contributes to the overall New Alliance Programme for Food Security and Nutrition under its Information and Communications Technology (ICT) Extension Challenge Fund. The project is implemented in collaboration with CABI.

The specific goal of the project is to contribute to increased agricultural production and productivity by scaling up the use of productivity-enhancing agricultural innovations and marketing mechanisms by small-scale farmers, using a combination of ICT-enabled agriculture extension approaches (participatory radio, mobile services), integrated and engaging with traditional extension services and linking to IFAD's existing programmes.

**2.0 Evaluation objectives and questions**

The primary objective of the terminal evaluation is to assess the achievement of objectives of the UPTAKE project. It will also identify and document lessons learned, and provide concrete recommendations for improving the performances of UPTAKE consortium members in future interventions.

**3.0 Scope of the Assignment**

The terminal evaluation will be conducted in the Pwani, Tanga, Njombe, Mbeya, Songwe, Kilimanjaro, Arusha and Iringa regions of the United Republic of Tanzania. These are the areas in which the UPTAKE project was implemented. The evaluation will focus on synthesizing evidence of the relevance, effectiveness, efficiency, impact, and sustainability of the project, and on lessons learned, based on information collected from farmers, broadcasters, project staff, knowledge partners, and input supply partners.

**4.0 The Consultancy Team and Required Qualifications**

The competing firms for this assignment should be **"NATIONAL CONSULTANTS"** and possess the following competencies and qualifications.

- The evaluation team should be composed of a communication for development (C4D) and/or ICT for development (ICT4D) expert, agricultural extension expert, a social scientist, and a statistician.
- Extensive and dependable experience, skill and knowledge of conducting surveys, interviews, participatory methodologies, and data analysis (qualitative and quantitative).
- Experience evaluating communication for development projects (preferably rural and agricultural development) is mandatory.

**5.0 Proposal Submission**

- Bidders should submit renewed trade licenses, tax certificates, professional licenses, and other required documentation as indicated in the instruction to bidders.
- Bidders should submit their technical and financial proposals electronically at the following address: **tanzania@farmradio.org**
- The deadline for submission of proposal is **March 20, 2019.**
- No bid documents submitted after the specified deadline will be accepted.
- Incomplete applications will be disqualified.

*Any inquiries about the comprehensive ToR should be addressed to rchapota@farmradio.org*

215114901

# Mwandishi aachiwa kwa dhamana

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MWANDISHI wa habari wa kujitegemea wa jijini Arusha, Basil Elias, ameachiwa kwa dhamana na Jeshi la Polisi baada ya kushikiliwa tangu juzi kutokana na kufuatilia malalamiko ya wananchi wanaougua matumbo na kuharisha.

Baadhi ya wakazi jijini hapa kwa nyakati tofauti, wamekuwa wakilalamika kuumwa homa za matumbo, kuharisha na kutapika kwa kile walichodai ni kutokana na kunywa maji yaliyochanganyika na maji taka.

Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira (Auwsa), ndiyo inayolalamikiwa lakini uongozi wa mamlaka hiyo ulitoa taarifa ya kukanusha kuwepo kwa maji yaliyochanganyika na maji taka (kinyesi).

Kuachiwa kwa mwandishi huyo kumetokana na waandishi wa habari mkoani hapa kwenda kwa Ofisi za Kamanda wa Polisi wa Mkoa huo mapema asubuhi jana, kuomba aachiwe kwa kuwa alikamatwa wakati akitekeleza majukumu yake ya kazi.

Akizungumza mara baada ya kuachiwa, Elias alisema kabla ya kukamatwa Machi 13, majira ya saa 11:00 jioni, alipigiwa simu na mwananchi aliyejitambulisha kwa jina la Anna Nathaniel, Mkazi wa Engutoto jijini hapa na kutoa malalamiko yake ya kutiririshiwa maji taka kwenye bomba lake la Auwsa.

Alisema baada ya kupata taarifa hizo ikiwa mara ya pili kujirudia kitu hicho kwake, aliwasiliana na Katibu Tawala wa Mkoa (RAS) na kuelekezwa kwenda kwa Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Gabriel Daqarro, ambaye naye alimpatia wataalamu wa kwenda nao eneo la tukio kujiridhishisha na taarifa hizo.

"Tuliongozana hadi kwa mama huyu na tulipofika tukaona kweli kuna hilo tatizo, wataalamu waliamua kutoa maji machafu kwenye chemba za majirani zake, wakidhani labda yanaingia kwake na walipoyatoa bado wakaona yanaendelea kutoka wakadhani mtandao wa Auwsa umepasuka mahali na kuingia kwake, ikabidi nimpigie Mkurugenzi wa Auwsa kumweleza suala hili," alisema.

Alisema baada ya kumaliza kuona hali halisi waliondoka na kurudi mjini, lakini wakiwa njiani mmoja wa wataalamu hao walimweleza amepokea simu toka kwa Mkurugenzi wa Auwsa kuwa wampeleke kituo

INAENDELEA UK. 26

# Lukuvi ashtukia uswahiba kupandishana vyeo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amesema ana taarifa za baadhi ya watendaji wa wizara hiyo kupandishana vyeo kiholela kutokana na kujuana.

Kutokana na changamoto hiyo, waziri huyo amemwagiza Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dorothy Mwanyika, kuhakikisha watendaji wa wizara hiyo wanapewa nafasi za kuongoza kwa uwezo wao na si upendeleo kama ilivyokuwa awali.Lukuvi aliagiza kufanyika kwa mchujo wa watendaji wa wizara hiyo kwa kuwa baadhi yao wamekuwa wakiipa sifa mbaya wizara kutokana na kujihusisha na rushwa na kuonea wananchi.

Lukuvi alifichua changamoto hiyo jana jijini Dodoma alipofungua kikao cha baraza la wafanyakazi wa wizara hiyo kilichojadili utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2018/19 na mwelekeo wa bajeti ya mwaka huu wa fedha (2019/20).

Alisema kuna vijana wengi wenye uwezo, lakini wananyimwa na kunyimwa nafasi hizo kutokana na mafaili yao kuonekana "ni mepesi na hawana uzoefu kazini".

"Matokeo yake, wizara inakosa ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake kutokana kuwa na viongozi wasio na tija wala sifa ya kutekeleza majukumu husika. Siwezi kukubali mtu anasukumiwa jalada wakati mtu hana uwezo, halafu yeye anapitisha na kumpa mtu cheo," alisema.

Lukuvi aliagiza kuwa kufikia Julai 7, mwaka huu, watumishi wote kuanzia ngazi ya wilaya hadi mkoa, wawe chini ya Katibu Mkuu wa wizara hiyo.

"Nakuagiza Katibu Mkuu kupanga upya watumishi kwa mujibu wa uwezo wao na sifa ya kusimamia shughuli za wizara, ili kila mtu anayestahili aongoze, siyo kwa kujuana kama ilivyokuwa ikifanyika hapo zamani, mtu kupewa cheo lazima kujuana," alisema.

Lukuvi: "Nina taarifa za mtumishi ambaye ana uwezo mkubwa, lakini mmempiga teke mara zote, kila nafasi aliyostahili amenyimwa, lakini hivi sasa ameshastaafu, ndiyo katibu mkuu anasema amegundua ana sifa.

"Sasa mnataka mumrudishe kwa mkataba, sasa ndiyo mmejua ana uwezo baada ya kustaafu? Nimeshangazwa sana."

Lukuvi alitoa miezi miwili hadi Mei 30, mwaka huu, watendaji wa wizara hiyo wawe wamekusanya kodi kwa wadaiwa wote wa kila kanda na kila wilaya kwa mujibu wa watu waliowasajili na wanaomiliki ardhi katika maeneo hayo.

Alisema katika eneo hilo, anataka wafanye marekebisho na marejeo kwa kuingiza takwimu sahihi katika mitandao yao na kila wilaya lazima watu wote waliomilikishwa watambulike kwenye mfumo.

Waziri huyo pia alisema bado kuna malalamiko kutoka kwa wananchi kuendelea kuwapo kwa mchezo mchafu wa kuficha mafaili katika ofisi ya msajili na sehemu nyingine.



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) taifa, Freeman Mbowe (wa tatu kulia) akiwa na viongozi waandamizi wa chama wakati kesi yao ilipotajwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Waziri wa Kilimo atishia kuifuta NFRA

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, ametishia kuufuta Wakala wa Hifadhi ya Chakula (NFRA), kama hautakuwa na uwezo wa kununua tani 500,000 za mazao kutoka kwa wakulima nchini.

Hasunga alieleza kusudio hilo jana alipozindua mashine maalum ya kusafisha mahindi iliyotolewa kupitia Mpango wa Chakula Duniani (WFP) kwa NFRA jijini hapa.

Alisema kuna mabadiliko makubwa yanayopaswa kufanyika NFRA kwa kuwa kazi yao si tu kuhifadhi chakula, bali pia lazima wanunue mazao yote ya ziada kwa wananchi na baadaye kuyauza.

"Nimewashangaa mpo kwa ajili ya kuhifadhi, eti chakula cha taifa wakati mazao yako kwa wananchi badala ya kwenda kutafuta masoko mkayanunue mazao yaliyopo kwa wakulima, kuna masoko kama Misri, nendeni mkatafute masoko," Hasunga aliagiza.

Waziri huyo alitaja mambo matatu yanayotakiwa kufanywa na wakala huo ili usifutwe, ikiwa ni pamoja na kununua tani 500,000 za mazao kutoka kwa wakulima

"Jambo la kwanza lazima muwe na uwezo wa kununua tani laki tano (500,000) kama hamna uwezo, nitafuta NFRA, nunua na kuuza si kuhifadhi tu, siyo mnakaa hapa hata kutafuta masoko hamtafuti.

"Hilo sikubaliani nalo, nategemea mnunue mazao kwa wananchi, mnasema hamna mtaji wakati mnao, nunua, uza, nunua, uza... Hapa mnajifanya mpo 'busy' (tingwa na majukumu) kwa hizo tani 36,000 za WFP, hapana! Mnatakiwa kufanya kazi zaidi," Hasunga alisema.

Waziri huyo alisema jambo la pili ni lazima wakala huo uwe na maghala ya kuhifadhi vizuri mazao kwa miaka mitano, akibainisha kuwa yaliyopo yana uwezo wa kuhifadhi kwa miaka miwili hadi mitatu na baada ya hapo yanakuwa yameharibika.

"Mtafute maghala mazuri, kama Marekani wanaweza kutunza kwa miaka 10 hadi 15, kwanini sisi? Jambo la tatu, lazima mbadili mfumo wa ununuaji nafaka, mfumo mnaotumia una gharama kubwa, kuna mifumo mizuri ipo ya kielektroniki," alisema.

Hasunga ambaye kitaaluma ni mhasibu mwenye kiwango cha CPA, alisema kama wasipopunguza gharama za uendeshaji, atawaondoa.

Alisema gharama za usafirishaji kwa gunia moja katika wakala huo ni Sh. 7,500 wakati watu binafsi wanasafirisha gunia moja kwa Sh. 2,000 hadi 3,000.

"Hilo sitakubadiliana nalo. Kwa hiyo, mbadilishe mfumo na fikra zenu, msipobadilisha, nitabadilisha kwa lazima," Hasunga alisisitiza.

Waziri huyo alisema mpango mkakati wa WFP wa miaka mitano,

INAENDELEA UK. 8

## HABARI KITAIFA

# Madaktari Saudia Arabia wapiga kambi Muhimbili

**Na Elizabeth Zaya**

JOPO la madaktari kutoka Saudi Arabia wameweka kambi katika Hospitali ya Taifa Muhimbili kutoa matibabu kwa watoto.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Balozi wa Tanzania nchini Saudi Arabia, Hemed Mgaza, alisema madaktari wametoka katika hospitali mbalimbali za nchi hiyo ambazo zimebobea katika magonjwa ya watoto.

Alisema mbali na kutoa huduma kwa watoto, jopo hilo pia linatoa mafunzo kwa madaktari kutoka katika hospitali mbalimbali nchini.

“Madaktari hawa huwa wanakuja kila mwaka na safari hii mbali na kuja kutoa huduma ya matibabu, wamekuja pia kutoa mafunzo kwa madaktari wa Tanzania katika hospitali mbalimbali nchini, ambao wanahudumia katika wodi za uangalizi maalum,” alisema.

Balozi huyo aliongeza: “Mafunzo haya ni muhimu sana kwa sababu, kundi la wagonjwa wa namna hii linahitaji uangalizi wa hali ya juu na wa kitaalamu zaidi kuokoa maisha yao. Kwa hiyo, tunashukuru kwamba yatakuwa na tija kwa nchi yetu.”

Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Mohamed Bakari, alisema Tanzania ina mpango mkubwa wa kuhakikisha inawekeza zaidi kwa wataalamu wabobezi katika sekta ya afya.

“Tanzania tuna mpango mkubwa wa kuhakikisha tunawekeza zaidi katika wataalamu wabobezi katika maeneo mbalimbali ya utoaji huduma kwenye sekta ya afya.

“Kwa mfano, kwa Muhimbili ni eneo ambalo ni mtaji wetu wa kuzalisha wataalamu hao na hapa ndipo panaweza kuleta tafsiri nzuri namna ambavyo serikali imejizatiti kuongeza nguvu katika suala hilo.

“Tunafanya juhudi hizi ili kuhakikisha kila Mtanzania anapata huduma bora zaidi za kiafya hususani ambazo ni za kibobezi na ndiyo maana tunaendelea kufanya juhudi mbalimbali za kufanikisha hilo, ikiwa ni pamoja na timu mbalimbali kama hizi za wataalamu wanaokuja nchini kwetu kutuongezea utaalamu,” Prof. Bakari alisema.

Aliishukuru serikali ya Saudi Arabia kwa mchango huo na ushirikiano wao hususani katika sekta ya afya, huku akiahidi kwa watahakikisha ushirikiano huo unakuwa wa kudumu.

# Mwakyembe akerwa uharibifu maeneo ya kihistoria

**Na Tiganya Vincent,** TABORA

SERIKALI imekemea tabia ya kuharibu maeneo ya kihistoria yakiwamo majengo ya kale kwa madai potofu kuwa wakoloni walificha madini ndani yake.

Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, alisema hayo jana wakati wa ziara yake katika Manispaa ya Tabora kutembelea maeneo ya urithi wa ukombozi wa bara la Afrika.

Alisema vitendo vya aina hiyo vinasababisha serikali kutumia gharama kubwa pindi inapotaka kukarabati na kurudisha historia ya maeneo hayo.

“Hakuna ambaye ni mjinga aweke ndani ya nyumba dhahabu halafu asiifuate. Hata wangekuwa wameweka mali ndani ya majengo yao wangekuja na njia nyingine ya kutaka kuendeleza maeneo hayo kwa kuweka miradi ya kuchimba visima ili wachukue madini kama yangekuwapo” alisema.

Dk. Mwakyembe alisema maeneo hayo ni muhimu sana katika historia ya Tanzania na pia katika ukuzaji wa utalii kwa ajili ya kulipatia taifa fedha za kigeni.

Aliongeza kuwa maeneo hayo ni muhimu katika kutoa elimu kwa vijana wa kitaifa kufahamu historia ya nchi yao kwa ajili ya kuwa wazalendo wazuri wa Tanzania.

Mwakyembe alisema wizara yake inaendelea na utaratibu wa kuyaorodhesha maeneo yote ya kihistoria kwa ajili ya kuyahifadhi na kuyakarabati kwa ajili faida ya kizazi cha sasa na kijacho.


THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRIME MINISTER’S OFFICE
LABOUR, YOUTH, EMPLOYMENT AND THE PEOPLE WITH DISABILITIES
OCCUPATIONAL SAFETY AND HEALTH AUTHORITY (OSHA)

**Awards for Occupational Safety and Health (AOSH) 2019**




Theme of the year: ***Safety and health and the future of work: towards industrial economy***

**Introduction**

In commemorating World day for Safety and Health at Work and as a part of National OSH promotion and awareness creation activities, Occupational Safety and Health Authority (OSHA) is inviting all owners of workplaces or employers to compete for the Awards for Occupational safety and Health (AOSH).

**Aim**

To encourage private and public workplaces throughout Tanzania to develop, implement and evaluate strategies that help achieve a healthier and safer work environment.

**Entry Eligibility**

Applications are open only for workplaces which are registered and operated in Tanzania Mainland, and having OSHA Registration Certificate. All workplaces in both public and private sectors and from all sizes, economic sectors and categories as shown in the Application Form are encouraged to participate. If your workplace has planned or implemented any innovative idea or program which contributed in the promotion of safety and health at your workplace you are encouraged to apply. All applications selected for the awards will be visited for verifications. Safety and health information to be verified are shown in the Application Form.

**Rules for Participation**

i) Download the Application Form from the website **www.osha.go.tz,** or collect it from the nearest OSHA office.
ii) Complete the Form Field in Permanent Ink or Electronically. Note that incomplete Forms may not be considered.
iii) Applicant should pay entry fee of **TZS 50,000/=** non-refundable, Payments will be done electronically through GePG. Please visit the nearest **OSHA** office or contact through email or phone to get your Control Number **(zakaria.sumunijohn@osha.go.tz, 0754789752, 0715914628).**
iv) Print Application Form and have it signed by the authorized person, complete with Company Stamp. The completed Application Form must be submitted by **15th April 2019, 15:30 Hrs**. Do not attach any document during submission except for proof of payment.
v) The Form may be submitted in any of the following ways:-
   (a) To the **Chief Executive, OSHA**, P.O Box 519 **Dar es Salaam;** or submit the hard copy to the nearest OSHA Offices located in Dar es Salaam, Mwanza, Dodoma, Arusha, Mbeya, Mtwara, Tanga, Njombe, Morogoro and Bukoba
   (b) Email to: info@osha.go.tz or, **zakaria.sumunijohn@osha.go.tz**
vi) Competitors for **AOSH** must participate on the Exhibition to show their competency
vii) All participants and winners of Awards are invited to attend the award giving ceremony to be held on the **28th April 2019** in Mbeya Region, and they may be asked to be available for media interviews or other publicity.
viii) All written information will be verified by the Award Team. Participants are subject to OSH audits including site audit.

215115902

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tunahitaji teknolojia mbadala barabarani

**KILA** anayeingia Dar es Salaam anafahamu jinsi wakati mwingi kunavyokuwa na ugumu wa kuendesha chombo cha usafiri kwenye barabara za jiji hili.

Hata hivyo, ni jukumu la kila dereva na abiria kulinda maisha kwa kuzuia ajali za barabarani, ziwe zinazotokana na kutembea au kuwa kwenye vyombo vya moto.

Licha ya ugumu huo, serikali na wadau wanajitahidi kuhakikisha kila wakati wasafiri na watumia barabara wanalindwa na kuwa salama.

Kila mara unapofanyika ukaguzi na ukamilishaji wa jukumu la wiki ya nenda kwa usalama barabarani, ulinzi na usalama zaidi ni mambo yanayozingatiwa kulinda maisha ya polisi, abiria, vyombo na watumia barabara kwa ujumla.

Hata hivyo, tunaona kuwa tunahitaji kuwalinda zaidi na kutoa kipaumbele cha usalama kwa maofisa usalama wa barabarani, wanaoongoza magari kwa kuwa kama ilivyo vigumu kuendesha, ndivyo inavyokuwa taabu pia kwa wasimamizi hawa wa barabarani kufanyakazi zao kwa usalama hasa wanapoongoza magari asubuhi, jioni na usiku.

Tunashauri kuwa wakati huu zinapojengwa barabara mpya jijini Dar es Salaam na miji mingine zibuniwe mbinu za kisasa za kuwawezesha trafiki kufanyakazi zao kwa usalama na weledi zaidi kwani kinachojiri leo kinawaweka kwenye hatari kubwa zaidi.

Umma utakubaliana nasi kuwa, wanaoendesha magari wana ufahamu tofauti, wapo wanaojua wanachokifanya, wengine hawaelewi wala hawazingatii sheria za barabarani, wapo wagonjwa wa akili, wengine inawezekana wana msongo wa mawazo na wamechanganyikiwa au inawezekana baadhi wana taharuki kutokana na maisha au mazingira na mikasa inayowapata wakati huo.

Wapo wanaendesha kasi kupindukia, kuna wengine wenye magari mabovu, wapo baadhi wasiojua kuendesha na kwa ujumla barabarani panakuwa si mahali salama kwa yeyote.

Kwa hiyo wote hawa wanapokuwa barabarani kuanzia wenye magari makubwa kwa madogo, pikipiki, baiskeli, mikokoteni na bajaj, wanayaweka mazingira ya trafiki hatarini zaidi na maisha kuwa rehani kila wakati. Ndiyo maana tunazishauri mamlaka za kitafiti na kitaalamu kutafuta mbinu za kisasa zaidi za kuwasaidia trafiki kufanyakazi zao kwa usalama na weledi kuliko kuacha mambo kubaki kama yalivyo leo.

Tunafikiria zaidi kutokana na polisi hao kufanyakazi katika mazingira magumu na wakati mwingine kulazimika kusimama katikati ya barabara na kuhatarisha maisha yao.

Jana gazeti hili liliandika taarifa za kusakwa kwa dereva wa bajaj aliyemgonga na kumjeruhi polisi wa barabarani mkoani Shinyanga. Hili lituguse sote kuwa polisi hawa wanaumia, maisha yao yako hatarini. Ni wakati wa kutumia mbinu mpya na mikakati ya kisasa ya kuokoa maisha ya trafiki badala ya kuwaacha kufanyakazi katika mazingira magumu kwenye barabara zetu.

Iwapo tunajiridhisha kuwa wingi wa magari barabarani haudhibiti kwa kutumia taa ni vyema sasa kujiongeza zaidi na kujipanga kwa kuangalia mifano kwenye nchi nyingine ambazo nazo zilikuwa na tatizo la kuongoza magari kwa kutumia taa za usalama.

Tunatoa ushauri huu kwa sababu dunia imebadilika kitekinolojia na vyombo vya usafiri navyo vimebadilika vingi vinatumia utaratibu wa kujiendesha vyenyewe au teknolojia ya 'automatic' ambayo ndiyo iliyoko kwenye uendeshaji wa mitambo viwandani na magari. Tunashauri wataalamu wa vyuo vikuu UDSM, Chuo cha Usafirishaji, Taasisi za Ufundi na Teknolojia za Dar es Salaam na Arusha pia zihusishwe kumaliza tatizo hili.

Tunashauri wadau wengine wenye utaalamu wa kiuhandisi wajitokeze na kushauriana na mamlaka za kitafiti na Jeshi la Polisi ili kupata teknolojia mbadala inayolinda maisha ya trafiki wanaoongoza magari barabarani.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Mary Geofrey

# Umefika wakati kutambua viongozi wanaofaa na feki

**KUELEKEA** Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, wabunge na madiwani wameanza kujirudi kwa wananchi kuanza kutoa misaada mbalimbali.

Kila ukiangalia vyombo vya habari mwaka huu, utaona habari za mbunge huyu na diwani yule, wametoa msaada wa vitu kadha wa kadha kwa wananchi wa maeneo yao.

Sawa, ni wajibu wenu kutimiza vile mlivyoahidi kwa wananchi waliowapigia kura, kwa sababu lengo la kuomba kura lilikuwa ni kuwaongoza, kuwasemea na kuwapa misaada inayotakiwa.

Lakini, kipindi hiki kisitumike kama fursa kwenu viongozi ambao mlishindwa kutimiza wajibu wenu katika kipindi cha miaka minne mliyopewa, nafasi ya kutumika katika maeneo husika, mkatumia muda huu kuwalaghai wananchi.

Isiwe tangu mmechaguliwa mlitulia kula maisha, mkaacha kujishughulisha na matatizo ya wananchi kwa madai mko 'bize.' wakati huu ndio mnarudi mkijifanya kazi mliyopewa mnaimudu.

Ni vyema na haki kwa kiongozi aliyekuwa anatimiza wajibu wake wakati wote wa uongozi tangu alipochaguliwa, akaendelea kutimiza wajibu hata sasa, tunapoelekea kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.

Lakini isiwe umerudi jimboni kwa sababu umejua uchaguzi mkuu unakaribia na wewe bado unataka kupewa nafasi ya kuendelea kuongeza eneo ulilopo.

Msiwafanye wananchi hawana akili za kupambanua mambo, mkadhani hawajui vyema kuwa mlishindwa kutimiza wajibu wenu, leo ndio mrudi kwa zawadi za hapa na pale.

Wakati huu wa kurudi jimboni au kwa wananchi wakati miaka mingine ulikuwa 'bize' na mambo yako, inatia shaka machoni mwa wananchi ambao naamini ni weelewa wazuri wa kupambanua mambo katika nyakati tofauti.

Inashangaza sana kuona kiongozi anarudi jimboni na kuanza kuchangia mifuko ya saruji ya Sh. 500,000 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa yaliyokuwa yameinama tangu anaomba kuchaguliwa 2015.

Inashangaza na kutia hasira zaidi pale anapochukua waandishi wa habari, ili watoe habari hiyo kwa lengo la kuuaminisha umma wa Watanzania, kuwa ni kiongozi wa kuigwa.

Utakuwa wa maana, kama ulikuwa unafanya hivyo miaka yote bila ya kujali, ulikuwa unatangaza au la, kwa sababu Watanzania wanaona na wanafahamu ni nani anawafaa.

Nayaeleza hayo, kwa sababu wapo madiwani na wabunge ambao baada tu ya kuchaguliwa, walihama kabisa maeneo yao nao wakaenda kuishi mjini kula maisha kwanza.

Wapo na wengine ambao mara baada ya uchaguzi mkuu wa 2015, walikata mawasiliano na wananchi katika namna ya hawana tena muda wa kupoteza, kwa ajili ya kuzungumza na wakadhani miaka mitano ni mingi sana.

Kuna wale waliokuwa wanaonana na wananchi, lakini hawakutumia nafasi zao kutatua changamoto zinazowakabili. Ieleweke, kutatua changamoto za wananchi, si kuwapa hela, bali ni kuwawakilisha kutafuta msaada wa kile wanachokitaka.

Pia, wapo ambao waliokuwa bize kuwazungumzia bungeni, lakini kurudi jimboni ilikuwa shida, hawakuwa na muda, kutwa wako katika vikao visivyo na mwisho, Nao wajue, wakati wa kurudi kwa wananchi nao umefika.

Uongozi unautaka, majukumu unayakwepa. Ni wakati wa kuvuna ulichopanda na ukumbuke kuwa 'ng'ombe hanenepeshwi siku ya mnada.'

Wananchi je? Ni wajibu wenu sasa kutambua nani anawafaa kuendelea kuwa kiongozi wa eneo lako, kulingana na hulka ya uwajibikaji wake, lakini si kwa sababu ya maarufu.

Wananchi wasikubali kupumbazwa na 'vizawadi' vya muda mfupi na vyenye lengo la kuombea kura.

Kama kiongozi anatoa msaada, ni vyema na ni wajibu wake kufanya hivyo. Lakini, isiwe kigezo cha ushawishi wa kuomba kura.

Kipindi cha uchaguzi hakijafika na kitakapofika, mnapaswa kuchagua wawakalishi ambao mnaamini watawawakilisha vyema, katika kuwaongoza, badala ya wale wanaotaka madaraka kwa ajili ya shughuli zao binafsi.

Msiwaonee haya viongozi wa namna hii. Wealezeni ukweli na kama kuwakataa muwakatae, kwa kuwa walishindwa kufanya kile mlichowaagiza au walichoahidi.

Msikubali kutumika kuwa madaraja ya kupandisha watu kufikia malengo yao, maisha yao yakiendelea kupaa na nyie mnabaki kuwa watu wale wale, msio na shule nzuri, majisafi na salama.

Hakikisheni kama kiongozi alitoa ahadi zake, alizitimiza na kama hakuzitimiza, basi muwe mliona juhudi zake za kuzitatua, lakini akakwama kwa sababu mnazozijua. Daima isiwe aliendа kula maisha mjini, akawaacha na shida zenu, leo anarudi akitaka kuchaguliwa tena.

Madhara ya kuchagua wasiyofaa na waroho wa madaraka, nadhani yanafahamika, hivyo ni wajibu wa kila mwananchi na jamii kupima.

## HABARI KITAIFA



Mafundi wa kampuni ya Estim, wakiendelea na kazi ya awamu ya kwanza ya upanuzi wa Barabara ya Morogoro, katika eneo la Kimara Stopover, jijini Dar es Salaam jana, itakayojengwa kwa njia sita kuanzia Kimara hadi Kibaha mkoani Pwani yenye urefu wa kilomita 19, ikiwamo ujenzi wa madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji. **PICHA: JOHN BADI**

# Mawaziri Afya EAC wataka utafiti milipuko ya magonjwa

**Na Zanura Mollel,** LONGIDO

MAWAZIRI wa Afya wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), wametaka wanachama wa jumuiya hiyo kufanya utafiti wa namna watakavyodhibiti magonjwa ya mlipuko maeneo ya mipakani.

Maazimio hayo yalikuja baada ya ugonjwa wa ebola kushambulia eneo la Liberia na jumuiya ilituma madaktari wa jumuiya kwenda kusaidia kutoa kinga.

Mwakilishi wa Katibu Mkuu wa EAC, Dk. David Malikowa, alisema magonjwa ya mlipiluko maeneo ya mpakani hayaepukiki lakini ni vyema kutafuata njia ya kukabiliana na hali hiyo.

Alisema magonjwa ya mlipuko ambayo ni hatarishi kwa maisha ya binadamu, wanyamapori na hata mifugo, lakini endapo watachukua tahadhari kwa haraka kuthibiti inawezekana.

Akizungumza na wanakamati wanaoshughulikia maandalizi ya zoezi hili linalotarajiwa kufanyika mwezi june 11-14 2019 katika eneo la Namanga Tanzania-Namanga Kenya katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Longido. Alisema kwa sasa wanaangalia mapokezi ya viongozi wa pande zote mbili juu ya zoezi hili linalotarajiwa, kufanyika kwa majaribio ya awali juu ya kuthibiti magonjwa ya mlipuko maeneo ya mipakani.

"Niwapongeze viongozi wote kutoka upande wa kenya (Kajado) na upande wa Tanzania (Namanga) Kwa kukubali na kupokea hili jambo kwa uzito wa juu," alisema.

Dk. Balikowa alieleza kuna magonjwa ya mlipuko yanayoambukizwa kutokana na mwingiliano wa watu na hii ni kutokana na matumizi ya teknolojia ikiwamo usafiri kwa watalii kuingia nchi kwa nchi.

Akitolea mfano ugonjwa wa ebola na kipindupindu na kusema wapo watu wanaosafiri kwenda maeneo hayo yenye mlipuko na tusipojipanga ni rahisi sana kuingia hata kwa wakazi wa EAC.

Lakini pia kuna magonjwa ambayo wanyama wakiwa nayo ni rahisi pia kumuathiri binadamu, mfano ugonjwa wa kimeta, homa ya ndege, homa ya Bonde la Ufa, brussela na hata homa ya nguruwe, hivyo jitihada za kuthibiti hili linahitajika tena kwa haraka.

"Kuna magonjwa ambayo binadamu au mnyama akiwa nayo yanaingiliana katika maambukizi na ili hili jambo lifanikiwe kuna umuhimu wa wizara husika zote, taasisi pamoja na wananchi kushirikishwa," alidai.

Aidha aliongezea magonjwa ya mlipuko hukwamisha shughuli za kitaifa kuendelea pamoja na uchumi kuporomoka, hivyo hali hii ina athari kubwa sana kwa jumuiya yetu niombe kile tunacho kidhamiria kifanyake ipasavyo.

"Boda hii ya Namanga pakitokea magonjwa ya mlipuko lazima shughuli za kitalii zitaathiriwa hapa nchini," alidai.

Alisema kwa sasa wameona waanze na Tanzania na Kenya katika majaribio haya ya awali dhidi ya mlipuko wa magonjwa mipakani, hivyo dunia na nchi za EAC inatazama hili, endapo litafanikiwa kama inavyotarajiwa basi zoezi hili litafanyika maeneo yote ya mipakani.

"Jumuiya ya Afrika Mashariki inayo mipaka mingi sana ila tumeanzia hapa kwanza mpaka wa Namanga na zoezi hili linaitwa, 'EAC cross border field simulation exercice," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Longido, Frank Mwaisumbe, aliitaka Halmashauri ya Wilaya hiyo kutenga bajeti ya maafa kwa kushirikiana na wataalam wa afya wilayani hapa.

"Mkurugenzi nakuagiza tengeni bajeti ya maafa, panapotokea matukio kama haya ya magonjwa ya mlipuko yaweze kutatuliwa kwa wakati muafaka," alisema.

Naye mwakilishi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Harrison Chinuka, alieleza zoezi hili la kupambana na kuthibiti magonjwa ya mlipuko katika maeneo ya mipakani linaratibiwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki

"Waratibu wa zoezi hili ni EAC, lakini wafadhili ni Shirika la Maendeleo ya Jamii nchini Ujerumani (GIZ) pamoja na Shirika la Afya Duniani (WHO)," alifafanua.

Alieleza hali halisi ya EAC kwa muda wa miaka mitano kumekuwa na ongezeko kubwa la magonjwa ya mlipuko, kutokana na maeneo yanayotunza vimelea mfano Bonde la Ufa.

# Watoto wazururaji kukamatwa

**Na Happy Severine,** BARIADI

MAOFISA elimu kata katika mkoa wa Simiyu, wametakiwa kushiriki kikamilifu katika kukamata na kuwahoji watoto wazururaji wasiokwenda shuleni.

Agizo hilo lilitolewa jana na Ofisa Elimu wa Mkoa wa Simiyu, Ernest Hinju, wakati wa kikao cha maofisa elimu wilaya, waratibu elimu kata na wadhibiti ubora kilichokuwa kikijadili mikakati ya elimu ya mkoa wa Simiyu.

Hinju alisema anasikitishwa kuona watoto wadogo wanazurura mitaani bila kwenda shuleni na wengi wanaangukia katika makundi mabaya, hivyo ni wakati wa waratibu elimu kata kuanza kulishughulikia suala hilo.

Alisema waratibu elimu kata wote kulingana na kata zao wanalo jukumu la kuwakamata na kuwahoji watoto hao ili kujua matatizo yanayosababisha wasiwe shuleni wakati serikali inatoa elimu bure.

Ofisa elimu huyo alisema kwa kufanya hivyo kutawasaidia watoto kupata haki zao na hata kuwatambua wale ambao wamevuka umri wa kujiunga na elimu ya msingi katika mfumo rasmi na kuwasaidia kuwaunganisha na elimu ya watu wazima (Memkwa).

Pia aliwataka waratibu elimu hao kuwachukulia hatua za kisheria wazazi ambao kwa makusudi wamekataa au wanakataa kuwapeleka watoto shuleni na matokeo yake wanawageuza kuwa ni kitegauchumi.

"ili kuwasaidia watoto wanaozurura mitaani bila kwenda shuleni, ni vyema tukawakamata na kuwahoji na kwa kufanya hivyo lazima tutawapata na kuwafungulia mashtaka wazazi wazembe wasiopenda na kutimiza mahitaji ya watoto wao.

Naye Julius Mbakiza, Mratibu Elimu Kata ya Mhango, alisema ni kweli kumekuwapo na wimbi kubwa la watoto wanaozurura mitaani bila kwenda shuleni na matokeo yake wanajiunga katika makundi mabaya.



# Mabilioni yaokolewa matibabu ya figo nje

INATOKA UK. 3

"Huduma zimesogezwa kwa watu wengi zaidi tofauti na hapo awali," Dk. Ndungulile alisema na kuongeza kuwa Watanzania wengi wamekuwa wakitumia dawa kiholela bila ya kupima na kufuata ushauri wa daktari hususani dawa aina ya Diclofenac na za asili ambazo hazijathibitishwa.

"Unakuta mtu anaumwa kichwa, amechoka ametembea siku nzima anaenda kununua dawa za kutuliza maumivu, anameza na maumivu yanatulia, wakati alitakiwa kupumzika na kunywa maji mengi," alisema.

Kiongozi huyo wa serikali alisema wagojwa wa figo wanazidi kuongezeka nchini, akiwataka wananchi kujiwekea utaratibu wa kupima afya zao mara kwa mara na kuepuka matumizi ya dawa za kutuliza maumivu kiholela.

Alitaja visababishi vingine vya magonjwa ya figo kuwa ni pamoja na kutofanya mazoezi, uzito wa kupindukia, matumizi makubwa ya sigara na unywaji wa pombe.

Alisema takwimu zinaonyesha duniani kote, inakadiriwa watu milioni 850 wanasumbuliwa na magonjwa ya figo na kila mwaka, watu milioni 2.4 hufariki dunia kutokana na magonjwa hayo.

"Magonjwa ya figo yanashika nafasi ya sita miongoni mwa magonjwa yanayochangia idadi kubwa ya vifo duniani, Bara la Afrika hasa kusini mwa Jangwa la Sahara ni sehemu yenye wagonjwa wengi wa matatizo ya figo," alisema.

Dk. Ndungulile alisema magonjwa ya figo yamekuwa yakiongezeka barani Afrika kufikia wastani wa saba hadi 25 na utafiti uliofanyika kaskazini mashariki mwa Tanzania katika ngazi ya kaya mwaka 2014, ulionyesha ugonjwa sugu wa figo unaathiri asilimia saba ya Watanzania.

"Katika utafiti huo, ilionekana kwamba uelewa mdogo kuhusu magonjwa ya figo unachangia kwa kiasi kikubwa kupata ugonjwa sugu wa figo na idadi ya wagonjwa hawa imekuwa ikiongezeka kwa kasi kubwa ikiashiria ukubwa wa tatizo hili nchini," alisema.

Alisema wizara imefanikiwa kuhakikisha kunakuwa na dawa na huduma bora za usafishaji damu kwa wagonjwa wa figo, akibainisha kuwa hadi kufikia Desemba mwaka jana, kulikuwa na wagonjwa 1,050.

Alisema magonjwa ya kisukari na shinikizo la damu ni magonjwa yanayoongoza kwa kusababisha matatizo ya figo.

Dk. Ndugulile alisema serikali imedhamiria kuweka mashine za kusafisha figo (Hemodialysis) katika hospitali za rufaa za mikoa yote 28 ya Tanzania Bara.

# Sinema ya Lipumba, Maalim Seif yaendelea

**Na Waandishi Wetu**

SIKU moja baada ya Prof. Ibrahim Lipumba kuchaguliwa tena kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi (CUF), upande unaomuunga mkono Katibu Mkuu wa chama hicho, Maalim Seif Shariff Hamad, umedai mkutano uliomchagua Prof. Lipumba ni feki.

Prof. Lipumba alitangazwa mshindi katika nafasi ya mwenyekiti katika uchaguzi uliofanyika juzi wakati wa mkutano mkuu wa chama hicho, akipata kura 516 na kuwashinda Zueit Mwinyi aliyepata kura 36 na Diana Daudi (16).

Katika uchaguzi huo, nafasi ya Makamu Mwenyekiti ilichukuliwa na Abbas Juma Mahunzi aliyepata kura 349.

Hata hivyo, taarifa iliyotolewa jana na Naibu Mkurugenzi wa Habari na Mawasiliano wa CUF, Mbarala Maharagande, ilieleza kuwa hawautambui mkutano huo na viongozi wote waliochaguliwa kupitia mkutano huo.

Maharagande alidai mkutano huo ni feki kwa kuwa haukuitishwa na viongozi sahihi na kwamba Prof. Lipumba hana sifa ya kuchaguliwa kuongoza chama hicho baada ya kujiuzulu uenyekiti mwaka 2015 na baadaye kufukuzwa uanachama na Baraza Kuu la Uongozi Taifa.

"Lipumba hana sifa ya kuchaguliwa kuongoza CUF. Baada ya kujiuzulu uenyekiti mwaka 2015, alifukuzwa uanachama na Baraza Kuu la Uongozi Taifa," Maharagande alidai katika taarifa yake hiyo na kuongeza:

"Baada ya kufukuzwa, alikata rufaa kwenye mkutano mkuu, rufaa yake haijasikilizwa na yeye mwenyewe hajawahi kuiondoa, kwa hiyo hawezi kuwa na sifa za kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa CUF."

Alidai Prof. Lipumba alirudishwa ndani ya CUF na Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, Jaji Francis Mutungi na chama kilipinga uamuzi huo mahakamani na hukumu yake itatolewa Jumatatu ya Machi 18 na Jaji Benhajj Masoud.

"Baraza Kuu la Uongozi la Taifa lililoitisha mkutano huo halina uhalali, halina akidi, halina wajumbe halali waliochaguliwa na Mkutano Mkuu au kuidhinishwa na Baraza Kuu halali. Kwa hiyo, hawawezi kuitisha Mkutano Mkuu. Mkutano Mkuu unabaki kuwa hewa, feki, haramu." Maharagande alidai.

Alidai Sura ya tano ya Katiba ya CUF imeweka utaratibu wa namna ya kufanya uchaguzi ndani ya chama, na sura ya tatu inaelezea muundo, ngazi za vikao na viongozi wa chama na kwamba hakuna uchaguzi uliofanyika katika ngazi za chini ili kupata wajumbe wa mkutano mkuu.

Alidai Mkutano Mkuu umehudhuriwa na watu wasio na sifa ya kuwa wajumbe halali, hivyo hawawezi kuchagua viongozi wa CUF.

Wakati upande wa Maalim Seif ukieleza hayo, Prof. Lipumba jana alidai jijini Dar es Salaam kuwa Katibu Mkuu wa chama hicho (Maalim Seif) ni mtu hatari asiyetaka suluhu katika mgogoro uliopo ndani ya chama.

Alidai msuguano unaoendelea ndani ya chama hicho kutokana na Maalim Self kukataa suluhu, akisisitiza kuwa yuko tayari kwa suluhu na alishafuatwa na viongozi wa dini akawasikiliza, lakini tatizo liko kwa Maalim Seif.

"Maalim Seif yeye ndiyo hataki suluhu, hata anapotafuatwa na masheikh, anawakubalia kukutana halafu ikifika muda, anaanza kutoa visingizio ambavyo havina maana, huyu Maalim Self ni mtu hatari, hataki suluhu," Prof. Lipumba alidai.

Alidai Maalim Self hakitakii mema chama hicho ndiyo maana kimekosa nafasi za uwakilishi katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Prof. Lipumba alidai tangu mwaka 2016, Maalim Seif amewafungulia kesi 39 wanazopambana nazo.

"Huyu amenishtaki mimi ambaye sihusiki, badala la kulishitaki Baraza Kuu kwa kuitisha mkutano, ndiyo maana kesi yake imeshindwa," Prof. Lipumba alidai.

Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, Sisty Nyahoza, alisema Ofisi ya Msajili ndiyo inayotunza katiba na kanuni za vyama vya siasa, hivyo ni jukumu lao kuhakikisha nyaraka zinatunzwa.

Alisema wanatakiwa kuhudhuria mikutano ya vyama vya siasa kwa kuwa sheria inawapa jukumu la kusimamia vinavyoendesha uchaguzi wake kwa mujibu wa katiba.

***Imeandaliwa na Beatrice Shayo na Gwamaka Alipipi**

# Mbowe, wenzake wasomewa upya mashtaka

INATOKA UK. 3

"Mnatakiwa mjipange kesi hii ina mawakili wengi usipokuwapo wewe wengine watakuwapo kuendelea na kesi, tunafanya kazi ya utoaji haki kwa mujibu wa sheria," alisema Hakimu Simba.

Alisema mahakama yake itasikiliza ushahidi wa Jamhuri Machi 28 na 29, mwaka huu dhamana ya washtakiwa inaendelea.

Mbali ya Mbowe washtakiwa wengine ni Mbunge wa Tarime Mjini, Esther Matiko; Katibu Mkuu wa Chadema, Dk. Vincent Mashinji; Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa; Naibu Katibu Mkuu Zanzibar, Salum Mwalimu; Mbunge wa Kibamba, John Mnyika; Mbunge wa Kawe, Halima Mdee; Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche na Mbunge wa Bunda, Ester Bulaya.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa hao wanadaiwa kuwa kati ya Februari Mosi na Februari 16, mwaka jana, wakiwa Kinondoni, Dar es Salaam kwa pamoja walikula njama na wengine ambao hawapo mahakamani ya kutenda kosa la jinai ikiwamo kuendelea na mkusanyiko isivyo halali na kusababisha chuki na uchochezi wa uasi.

Ilidaiwa kuwa Februari 16, mwaka jana, Bulaya alishawishi kutenda kosa la jinai katika viwanja vya Buibui vilivyopo Kinondoni,jijini Dar es Salaam alishawishi wakazi wa eneo hilo kutenda kosa la jinai kwa kufanya maandamano yenye vurugu.

Pia ilidaiwa kuwa Februari 16, mwaka jana katika barabara ya Kawawa eneo la Mkwajuni wilaya ya Kinondoni, washitakiwa kwa pamoja na wenzao zaidi ya 12, walifanya mkusanyiko na kukaidi amri halali ya ofisa wa jeshi la polisi Gerald Ngiichi na kusababisha kifo cha Akwilina Akwiline na askari polisi wawili Konstebo Fikiri na Koplo Rahim Msangi kujeruhiwa.

Siku ya tukio la kwanza na la pili, ilidaiwa kuwa katika viwanja vya Buibui vilivyoko Kinondoni jijini Dar es Salaam, kwenye mkutano wa hadhara, Heche alitoa lugha ya kuchochea chuki akitamka kwamba: "Kesho patachimbika, upumbavu ambao unafanywa kwenye nchi hii...wizi unaofanywa na serikali ya awamu ya tano...watu wanapotea...watu wanauawa wanaokotwa kwenye mitaro lazima ukome."

Maneno hayo yanadaiwa kuwa yalielekea kuleta chuki kati ya serikali na Watanzania. Washtakiwa wote waliposomewa mashtaka yao kwa nyakati tofauti walikana.

# Spika afunguka kufyekwa posho

INATOKA UK. 2

Joseph Musukuma, aliomba mwongozo wa kiti cha Spika akihoji lini Bunge litasitisha mshahara wa Lissu.

Musukuma alidai kuwa Lissu ameshapona na anazurura nje ya nchi na kutukana viongozi wa nchi, huku Bunge likiendelea kumlipa mshahara na posho.

Katika majibu yake, Spika Ndugai alisema: "Ni kweli, jambo hili la ndugu yetu, rafiki yetu, mbunge mwenzetu Tundu Antipas Lissu linahitaji kuangaliwa kipekee kwa maana ya kwamba mbunge hayupo jimboni kwake, hayupo hapa bungeni tunapofanyia kazi, hayupo hospitalini, hayupo Tanzania na taarifa zake Spika hana kabisa.

"Wala hajishughulishi hata kumwandikia Spika, kumwambia niko mahali fulani nafanya hivi na kama ni mgonjwa, hakuna taarifa yoyote ya daktari halafu unaendelea kumlipa malipo mbalimbali lakini sasa wanamwona yuko duniani."

"Kwa maneno ya Mheshimiwa Musukuma, (Lissu) anazurura, kwa hiyo nikuhakikishie Mheshimiwa Musukuma, yale yaliyo ndani ya uwezo wangu nitayafanya. Asante kwa ushauri," Aliongeza Ndugai.

Septemba 7 mwaka juzi, Lissu alishambuliwa kwa kupigwa risasi akiwa ndani ya gari nyumbani kwake Area D mjini Dodoma na watu wasiojulikana wakati akitoka bungeni.

Baada ya shambulizi hilo alipelekwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma kwa matibabu ya awali na siku hiyo hiyo usiku alihamishiwa Hospitali ya Nairobi, Kenya.

Alikaa Nairobi hadi Januari, mwaka jana, alipohamishiwa kwenda hospitali nyingine nchini Ubelgiji ambako Desemba 31, mwaka jana, alimaliza matibabu yake na kuanza ziara nchi mbalimbali.

Januari 19, Lissu akihojiwa na Idhaa ya Kiswahili ya BBC, katika kipindi cha Dira ya Dunia, alitangaza kugombea urais mwaka 2020 kama wanachama na viongozi wenzake wa Chadema watampa ridhaa hiyo.

Aidha, Januari 21, alihojiwa kwenye kipindi cha HardTalk kwenye Televisheni ya BBC na mtangazaji maarufu Stephen Sackur.

Kipindi ambacho kilizua mjadala mkubwa kutokana na namna alivyojibu maswali ndani ya HardTalk na Februari 9, aliendelea na ziara nchini Marekani na mataifa mengine.

# DPP awaumbua polisi

INATOKA UK. 2

Machi 8, 2019, niliwafutia washitakiwa wote wawili mashtaka hayo na mahakama ikawaachia huru," Mganga alisema.

Aliongeza kuwa, baada ya Rais Magufuli kupokea ukweli wa malalamiko hayo na hatua zilizochukuliwa, amempongeza Sadick kwa ujasiri aliouonyesha kwa kuweka wazi malalamiko yake.

Mganga aliwataka mawakili wote wa serikali wanaofanya kazi katika Ofisi ya Taifa ya Mashitaka, waendesha mashitaka wote nchini waliokasimiwa mamlaka ya kuendesha kesi za jinai na vyombo vya upelezi, kufanya kazi zao kwa mujibu wa sheria bila kumwonea mtu yeyote na wazingatie maslahi ya taifa.

"Hatua za kinidhamu na kisheria zitachukuliwa dhidi ya wote watakaokiuka maadili ya kazi zao," Mganga alisema.

# Maofisa elimu, wakuu shule wapewa kibano

**Na Happy Severine,** SIMIYU

MAOFISA elimu na wakuu wa shule za sekondari mkoani Simiyu, wamepewa kibano juu ya ujenzi wa vyumba vya madarasa huku wakitakiwa kukamilisha kazi hiyo kabla ya Aprili 20, mwaka huu.

Ofisa Elimu wa Mkoa wa Simiyu, Ernest Hinju, alitoa agizo hilo jana wakati wa kikao cha kuweka mikakati madhubuti ya elimu mkoani humo huku akisema kufikia wakati huo, kazi hiyo iwe imemalizika ili kuruhusu wanafunzi waliokosa nafasi kujiunga kidato cha kwanza waanze masomo.

Hinju alisema kuwa maafisa elimu wote pamoja na wakuu wa shule za sekondari wanatakiwa kusimamia vema ujenzi wa maboma hayo ili yaweze kukamilika kwa wakati na ubora unaotakiwa. Alisema kazi hiyo lazima ikamilike kwa muda uliokusudiwa kwa kuwa tayari kila shule imewezeshwa fedha kutoka Wizara ya elimu ili kusukuma ujenzi huo ukamilike kwa haraka.

Naye Edda Malick, kiongozi kutoka katika mpango wa kuinua ubora wa elimu Tanzania (Equip) alisema kwa upande wao wamekamilisha ujenzi wa maboma kwa asilimia 60.

Malick aliongeza kuwa wamefikia kiwango hicho kutokana na jitihada na usimamizi madhubuti wa maofisa elimu na wakuu wa shule.

Kwa upande wake, Ofisa Utamaduni kutoka Ofisi ya mkuu wa Mkoa, Charles Maganga, ambaye alikuwa mratibu wa kamati ya kuboresha mikakati ya elimu, alisema mkoa wa Simiyu ulipokea Sh. bilioni 1.3 kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) kwa ajili ya kukamilisha maboma ya vyumba vya madarasa 84.

Maganga alisema fedha hizo zimetolewa kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ili wanafunzi waliokosa nafasi ya kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu, wapate nafasi hiyo na kuendelea na masomo kama wenzao.




Balozi wa Ufaransa nchini, Frederic Clavier, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu sherehe ya Sanaa ya mapishi ya chakula kizuri cha Kifaransa itakayofanyika jijini Machi 21. Kulia ni Meneja Mkuu wa Hoteli ya Hyatt Regency, Garry Friend. **PICHA: HALIMA KAMBI**

# Ajali bodaboda zapungua Morogoro

**Na Christina Haule,** MOROGORO

VIFO vinavyosababishwa na ajali za pikipiki maarufu kama bodaboda, vimepungua mkoani hapa kutoka 21 kwa kipindi cha mwaka 2017/18 hadi kufikia kifo kimoja mwaka huu.

Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Morogoro, Michael Udeleli, alisema jana kuwa kupungua kwa vifo hivyo kumetokana na utayari wa madereva wa bodabora kukubali kwenda kusoma sheria za usalama barabarani na jinsi ya kutumia vyombo vya moto.

"Madereva wetu wamekubali kutii sheria bila shuruti kwa sasa na kufuata sheria za barabarani jambo ambalo limesaidia kupunguza ajali hizo kwa kiwango kikubwa," alisema.

Udeleli alisema madereva wa bodaboda na vyombo vingine vya moto, walikubali kwenda shule kwa hiari na wale watakaobainika kukaidi kwenda kusoma na kuvunja sheria za barabarani, watafikishwa mahakamani.

Aidha aliwataka watumiaji wa vyombo vya moto na wananchi kwa ujumla kutii sheria za barabarani ili kuepusha ajali zisizo za lazima na atakayebainika kuvunja sheria jeshi hilo halitosita kumchukulia hatua.

mmoja wa madereva wa bodaboda Manispaa ya Morogoro, Saidi Mkwinda, alisema zamani walikuwa hawana mwamko wa kuona umuhimu wa kujifunza sheria za barabarani, hivyo kuendesha bila kuzingatia sheria na kujikuta wakati mwingine wakipata ajali na pengine kupoteza maisha na hata kupata vilema vya kudumu.

Alisema kwa sasa wamepata mwamko wa kwenda kusoma na kuzijua sheria za usalama barabarani, hivyo kuepuka kukamatwa kila mara na polisi kwa makosa ambayo wanaweza kuyaepuka, ikiwamo uvaaji wa kofia ngumu.

Mkwinda alisema kwa sasa wamekuwa na mwamko mkubwa na wanalindana wenyewe kwa wenyewe ili kuhakikisha kila mmoja anazingatia sheria za usalama barabarani.

# Vijana watakiwa kukataa umaskini

**Na Sabato Kasika**

VIJANA wamekumbushwa kutokumbatia umaskini na badala yake wajitume kwa kuchangamkia fursa mbalimbali zilizopo kwa ajili ya kujiletea maendeleo.

Mtaalamu kutoka Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (Sido), Michael Malembeka, alisema hayo jana wakati akitoa mafunzo ya kutengeneza na kusindika bidhaa mbalimbali za biashara kwa vijana.

Vijana hao kutoka majukwaa ya vijana Manispaa ya Ubungo jijini Dar es Salaam, wanajifunza kutengeneza sabuni za maji na miche na pia kusindika vyakula mbalimbali, matunda na kuoka mikate.

"Katika maisha kuna vitu viwili, utajiri na umaskini. Kijana unaweza kuamua kuzingatia mafunzo haya au kuyaacha na usitegemee mtu katika maisha yako, lakini ukumbuke umaskini una sifa kuu mbili," alisema Malembeka.

Alisema umaskini unaishi mahali ambapo unavumiliwa na kama hauwezi kuvumiliwa, utaondoka, na pia mkufunzi huyo alitaja sifa ya pili kuwa mtu asipoushughulikia, utamshughulikia.

"Hivyo msiuvumilie...utasikia mtu anasema mimi ni maskini nitafanyaje, hapa ina maana unauvumilia umaskini, vijana jitumeni kwa kupambana kwa dhati na adui huyu ili kuhakikisha mnafanikiwa katika maisha yenu," alisema.

Alisema mafunzo hayo ni njia mojawapo ya kupambana na umaskini iwapo watayazingatia, lakini vinginevyo wanaweza kutoka wakiwa hawana kitu cha kwenda kufanya katika maeneo yao.

Kwa upande wake mmoja wa viongozi wa taasisi inayoratibu mafunzo hayo, Mpakani Tunaweza, Hussein Wamaywa aliwataka vijana kuhakikisha hawatoki watupu bali wawe na cha kujivunia.

"Mnafundishwa kutengeneza vitu vingi, na inawezekana kijana usipendelee kitu fulani, lakini ni muhimu upeleke ujuzi huo katika jukwaa lako, mwenzako anaweza kupenda ujuzi wa kile ambacho wewe hupendi," alisema Wamaywa.

Alisema vijana hao wakipeleka ujuzi huo katika majukwaa yao, inawezekana jukwaa likawa na wataalam wa kutengeneza bidhaa mbalimbali na hivyo mafunzo hayo kuleta tija.

"Hilo ndilo lengo la Mpakani la kuratibu mafunzo haya, cha msingi ni vijana kuwa makini kufuatilia kila hatua ambayo mkufunzi anaifanya ili wote mtakapotoka hapa muwe mmeiva kwa ujuzi za kutengeneza bidhaa kwa ajili ya maendeleo yenu," alisema.

Kiongozi huyo alisema muda wa siku tano kwa ajili ya mafunzo ya kutengeneza bidhaa, kusindika na kuoka unatosha kuwafanya vijana hao kupata kitu cha kujivunia kwa ajili ya maendeleo yao.

# Kahama kinara ukatili kijinsia

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

HALMASHAURI ya Mji wa Kahama, imeelezwa kuwa inaongoza kwa ukatili wa kijinsia hasa kwa watoto wadogo ukilinganisha na halmashauri zingine zilizoko mkoani Shinyanga.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya Mji wa Kahama, Abdulrahman Nuru, alibainisha hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake huku akisema ukatili uliopo ni ule wa wazazi wa kutelekeza watoto na wa kujifungua na kutupa watoto vichakani.

Alisema kila mwezi zaidi ya mashauri 300 ya ukatili wa kijinsia kwa watoto wadogo huripotiwa na kusababisha halmashauri kuongoza kuwa na ukatili mkubwa wa kijinsia kulinganisha na maeneo mengine.

Nuru alisema kwa mwaka jana mashauri ya ukatili wa kijinsia 1,300 yaliripotiwa tofauti na yale ambayo yanaripotiwa kituo cha polisi dawati la jinsia na kwamba kama wananchi hawataendelea kutoa taarifa takwimu zitaendelea kuongezeka.

Pia alisema Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 kifungu namba 21 kinaeleza wazi juu ya kila mwananchi au jamii kuwa na wajibu wa kutoa taarifa za ukatili wa kijinsia kwa watoto, mimba za ututoni ili kumchukulia hatua anayefanya ukatili huo na si kukaa kimya huku mtoto akiendelea kunyanyasika.

Hata hivyo, alisema atawachukulia hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kuwafikisha mahakamani wazazi wote watakaobainika kuwa na watoto wanaorandaranda mitaani huku wakiwa na umri wa kwenda shuleni.

Alisema tayari wameanza utaratibu wa kuwabaini watoto wote walioko mitaani na watakaobainika kuwa wanatoka nje ya wilaya ya Kahama watasafirishwa hadi kwao na wale wanatoka wilayani hapa wazazi wao watachukuliwa hatua za kisheria.

Nuru pia alisema asilimia kubwa ya watoto walioko mitaani wanatoka katika mikoa ya Geita, Kigoma, Kagera hasa wilaya za Ngara, Tabora, Bariadi na Singida. Alisema kila mwezi watoto huongezeka mitaani na hiyo inatokana na wilaya kuwa na mwingiliano wa watu wengi.




Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akichangia mada katika masuala ya kuboresha biashara huria barani Afrika wakati wa hitimisho la mkutano wa Africa Now Summit 2019 jijini Kampala, Uganda juzi. **PICHA: OMR**

# Vifo vya wajawazito, watoto vyashuka

**Na Magreth Magosso,** KIGOMA

MKOA wa Kigoma umepunguza vifo vya wajawazito kutoka 135 kati ya vizazi hai 100,000 kwa mwaka 2017 hadi 77 kwa mwaka 2018.

Hayo yalibainika jana wakati wa uzinduzi wa kampeni ya Jiongeze Tuwavushe Salama Mjamzito na Mtoto Mchanga, yenye lengo la kuhamasisha na kuwapa stadi viongozi wa serikali, asasi za kiraia na wadau wa maendeleo, jamii na watoa huduma katika kuokoa vifo vya wajawazito na watoto wachanga.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Dk. Paul Chaote, alisema wanaendelea na juhudi za kupunguza vifo hivyo ambavyo kitakwimu hali inaonyesha matumaini kwa wajawazito.

Pia alisema vifo kwa watoto wachanga vimepungua kwa wastani kutoka vifo 18 katika vizazi hai 1,000 kwa mwaka 2017 hadi vifo vinane kwa mwaka jana.

"Mpaka leo tuna asilimia 53 ya vituo vya afya kuwa na huduma ya dharura kwa mama mjamzito na ifikapo Juni, mwaka huu, tunatarajia kufikia asilimia 85 ya vituo vyote kutoa huduma ya upasuaji kwa mjamzito na wenye uzazi pingamizi.

"Lengo la kitaifa ni kufikia vifo 292 katika vizazi hai 100,000 kwa wajawazito ifikapo mwaka 2020, vifo vya watoto kutoka 25 hadi vifo 16 katika vizazi hai 1,000 kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2015. Kimsingi tunahitaji kusiwe na vifo vya uzazi," alisema Dk. Chaote.

Aidha aliipongeza jamii kwa kupokea elimu ya faida ya mjamzito kujifungua katika kituo cha afya na kwamba kwa mwaka 2017 waliojifungulia katika mikono ya watoa huduma ni asilimia 78 na mwaka jana ilifikia asilimia 98.5 wajawazito kujifungulia katika katika vituo vya afya na hospitali.

Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Brigedia Jenerali Emmanuel Maganga, ambaye alikuwa mgeni rasmi katika uzinduzi huo, alisema kampeni hiyo ni chachu ya mabadiliko kuondoa vifo vitokanavyo na uzazi na kuboresha uhai wa watoto wachanga.

Naye Mratibu wa Afya ya Uzazi kwa mama na Mtoto Kigoma, Bertha Ndalituki, alikiri kuwa ushirikiano wa viongozi, jamii na watoa huduma ni chachu ya kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kwa ustawi wa umma.

## Vijana 300,000 wanufaika ufadhili serikali ya Norway

**Na Boniface Gideon,** TANGA

ZAIDI ya Watanzania 300,000 kutoka mkoani Tanga wamenufaika na mafunzo mbalimbali yanayofadhiliwa na Norway ikiwa ni sehemu ya kuimarisha uhusiano baina ya nchi hizo mbili.

Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Thobias Mwilapwa, alisema juzi alipokuwa akimpokea Balozi wa Norway nchini, Elisabeth Jacobsen, aliyefanya ziara mkoani Tanga na kujionea mkoa unavyoendesha shughuli zake kuanzia kwa wananchi hadi viongozi.

Mwilapwa alisema kuwa balozi huyo alitembelea ofisi ya Mkuu wa MKoa wa Tanga, wilaya pamoja na ofisi ya Mkuu wa Polisi Wilaya ya Tanga (OCD) kwa lengo la kujionea changamoto wanazokutana nazo viongozi hao.

Alisema uhusiano kati ya Tanzania na Norway ni wa muda mrefu na Tanzania imenufaika katika nyanja mbalimbali ikiwamo kupeana taaluma kwenye mafunzo mbalimbali. Alisema zaidi ya Watanzania 300,000 hususan vijana, wamenufaika na mafunzo kutoka nchini Norway.

"Uhusiano huu ulianza tangu miaka ya 1960 na tunapendelea nao ili kuimarika na miradi mbalimbali ipate ufadhili ikiwamo dawati la unyanyasaji wa kijinsia," alisema.

Aliongeza kuwa taasisi binafsi ya TICC imekuwa kiunganishi cha mataifa hayo mawili kwa kuwa imekuwa ikifanya mambo makubwa ikiwamo kutoa mafunzo kwa watu mbalimbali pamoja na vijana wa Kitanzania na ubalozi huo kuendelea kuisaidia Tanzania katika nyanja mbalimbali kama vile elimu, afya na miundombinu.

Naye, Balozi Jacobsen alisema amefurahishwa na mkoa wa Tanga unavyoendesha shughuli zake na kuahidi kuendelea kushirikiana nao katika nyanja mbalimbali ikiwamo elimu, afya na uwekezaji.

"Sisi serikali ya Norway tumefurahishwa sana na utendaji kazi wa serikali ya Tanzania chini ya Rais John Magufuli na sisi tunaahidi kuendelea kutoa ushirikiano kadri tuwezavyo," alisema.

Pia aliipongeza serikali ya Tanzania kwa kufanya uwekezaji mkubwa wa bomba la mafuta kutoka Ohima nchini Uganda hadi Chongoleani, Tanga, utakaonufaisha maelfu ya watu.00000

HABARI ARUSHA



# Naibu Waziri aagiza matokeo ya utafiti yaandikwe Kiswahili

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

NAIBU Waziri wa Kilimo, Innocent Bashungwa, ameziagiza taasisi za utafiti wa kilimo nchini, kuandika matokeo yao ya utafiti kwa lugha ya kiswahili ili kuwezesha wakulima wengi wa vijijini, kuzielewa na kuzifanyia kazi.

Akitoa agizo hilo Jijini Arusha jana wakati akizindua Teknolojia ya Kilimo Hifadhi, (CASI), iliyofadhiliwa na serikali ya Australia kupitia kituo cha utafiti Selian kilichoibua teknolojia hiyo, Bashungwa, alisema kilimo hicho kina tija na kinatunza mazingira.

Alisema changamoto kubwa iliyopo nchini ni tabia ya watafiti wengi kupitia taasisi zao kuandika tafiti zao kwenye vitabu kwa lugha ya Kiingereza ambayo wakulima wengi hawaelewi lugha hiyo hasa wa vijijini.

"Sasa naagiza taasisi hizi za utafiti wa kilimo zibadilike anzeni kuweka mikakati ya kubadilisha vitabu vyenu vya tafiti na kuweka katika lugha ya kiswahili ili wakulima wengi wa vijijini waelewe na kuzifanyia kazi," alisema.

Alisema tafiti nyingi nzuri kama hiyo ya teknolojia mpya ya kilimo hifadhi (CASI), lakini imeandikwa kwa kiingereza hivyo ueneaji wake kwa wakulima ni wa polepole.

Aliagiza watafiti hao kuhakikisha wanaeneza teknolojia hiyo kwa njia ya midahalo ya kiswahili na vyombo vya habari kwa kuwapatia elimu waandishi ili nao watumie kalamu zao kueneza kwa wakulima wengi zaidi ya sasa.

Alisema serikali inapongeza kituo cha utafiti Selian na serikali ya Australia iliyofanikisha kupatikana CASI kwa sababu inamwezesha mkulima kutumia eneo dogo kuzalisha mahindi na mazao jamii ya kundekunde pamoja na kupata kipato kizuri chenye tija kwake na kuongeza pato la taifa ambalo kwa sasa kilimo huchangia asilimia 29.1.

Pia aliagiza Taasisi ya Kilimo nchini na Taasisi ya uzalishaji mbegu kukaa pamoja na wadau wa viwanda kama SIDO ili watoe dhana za kusaidia wakulima kupalilia na kuvuna, japo teknolojia hiyo inapunguza upaliliaji na uandaaji mashamba kwa muundo wake wa kuacha masalia shambani ambayo hutoa mbolea baada ya kuoza na kuzuia uotaji magugu.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mohmoud Mgimwa, alisema teknolojia hiyo nzuri licha ya kuongeza uzalishaji na kupambana na mabadiliko ya tabia ta nchi, pia inapunguza uharibifu wa mazingira.

"Tunachoomba itangazwe zaidi kwenye vyombo vya habari na serikali iongeze bajeti za watafiti ili wafanye kazi vizuri na kuharakisha kupeleka bungeni rasimu ya maadiliko ya sheria ili tutengeneze sheria yenye tija kwa kulinda wakulima," alisema.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Kituo cha Utafiti wa Kilimo Selian, Dk Joseph Ndunguru, endapo teknolojia hiyo itaenea kwa wakulima wengi zaidi itawezesha upatikanaji wa malighafi za viwandani na mazao mengi zaidi ya sasa.



Mchuuzi wa picha za kuchora akisaka wateja katika Barabara ya Sam Nujoma eneo la Mwenge jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# DC aonya watakaoharibu miundombinu mradi wa maji

**Na Zanura Mollel,** LONGIDO

SERIKALI wilayani Longido mkoani Arusha, imewaonya wananchi watakaojihusisha na uharibifu wa miundombinu ya mradi wa maji uliojengwa kuanzia wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro wenye thamani ya Sh. bilioni 15.

Akizungumza na Nipashe ofisini kwake jana, Mkuu wa Wilaya ya Longido, Frank Mwaisumbe, alisema mradi upo kwenye hatua nzuri na maji yameshaanza kuingia kwenye tanki lenye uwezo wa kuchukua maji zaidi ya lita 400,000.

Alisema serikali imetoa fedha nyingi kutekeleza mradi huo, na imewataka wananchi kuacha kuharibu miundombinu yake bali wawe mabalozi wazuri katika kuhakikisha wanautunza mradi huo.

"Niseme tu akibainika mtu yeyote anayeharibu au ana matarajio ya kuharibu mradi huu, atachukulia hatua kali za kisheria.

"Ni kweli wana Longido walikuwa na kiu, ndani ya siku 10 maji haya yataanza kusambazwa kwa wananchi, niseme nahitaji watunze huu mradi wa mabilioni ya fedha," alidai.

Aidha alisema utaratibu wa watu kuingizwa kwenye mfumo wa watumia maji na kulipia utawekwa wazi pindi mradi huu utakapo zinduliwa na mamlaka husika.

Alifafanua kuwa maji hayo yatagawanywa pia kwa wakazi ambao mradi huu umepita katika maneno yao wakiwemo wananchi wa Kijiji cha Elerai pamoja na kata jirani ya makao makuu ya wilaya ambayo ni Kata ya Namanga.

"Serikali iliahidi na imetekeleza na hata wao waliopitiwa na mradi huu wa maji watapata pia," alisema.

Mkazi wa Longido, Shinini Saibulu, alisema tangu wilaya hiyo ianzishwe kutoka Wilaya ya Monduli hawakuwahi kutegemea kuletewa maji, lakini sasa ameona kazi nzuri inayotekelezwa na viongozi.

Alidai kipindi cha ukame wanapata changamoto ya kuhamahama na mifugo kwenda kutafuta maji na malisho, lakini kwa sasa wana neema ya maji ndani ya wilaya.

Alisema wapo tayari kuungana na serikali kuhakikisha mradi huu unakuwa endelevu kwa kulinda na kuutunza kama tunavyotunza mifugo yetu pamoja na mali zingine.

"Tumependelewa wana Longido niseme tuu lazima tutunze huu mradi kwa faida ya vizazi vijavyo," alidai.

# Watano washikiliwa polisi tuhuma za mauaji

**Na Jaliwason Jasson,**
BABATI

POLISI mkoani Manyara wanawashikilia watu watano kwa tuhuma za kumuua fundi makanika, Emmanuel Kaaya (24) kwa kutumia kitu chenye ncha kali.

Taarifa za mauaji ya fundi huyo zilitolewa jana na Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Augustino Senga, wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake juu ya matukio mbalimbali yaliyotokea mkoani humo.

Kamanda Senga alimtaja mtuhumiwa anayeshikiliwa kuwa ni Anthony Kalinga, (29), mkulima wa madukani huko wilayani Simanjiro na wenzake wanne ambao hawajafahamika kwa majina kutokana na wao kuwa walevi na kushindwa kujieleza.

Alisema tukio hilo lilitokea Machi 11 saa 4:53 usiku ambapo alisema chanzo cha tukio hilo ni ugomvi uliotokana na ulevi kwani wote walikamatwa wakiwa wamelewa pombe za kienyeji kiasi kwamba walishindwa kujieleza.

Alifafanua kuwa uchunguzi zaidi unaendelea na mwili wa marehemu umehifadhiwa katika Hospitali ya Lutherani Orkesument, na kwamba uchunguzi ukikamilika watuhumiwa watafikishwa mahakamani.

Alitumia fursa hiyo kuwaonya watu ambao wanadhani mkoa huu ni kichochoro cha kufanya uhalifu waache mara moja vinginevyo hamna mhalifu atakayesalimika na kupita salama bila kutiwa mbaroni na polisi.

Aliwaambia waandishi wa habari kuwa wapo wahalifu wanaendelea kuuza madawa ya kulevya au wanaoyasafirisha madawa hayo kwa kupitia mkoani hapa na kusisitiza kwamba wasipoacha wataendelea kuwakamata bila huruma na sheria itachukua mkondo wake dhidi yao.

Aliwaomba wananchi wenye mapenzi mema na nchi hii kuendelea kutoa ushirikiano kwa askari polisi kwa kutoa taarifa sahihi ili polisi wazifanyie kazi taarifa hizo kwa ajili ya kudhibiti uhalifu unaohatarisha raia na mali zake.





# Nyuki wanaochavusha mimea hatarini kutoweka kwa kemikali

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

NYUKI wanaosaidia uchavushaji mimea inayozalisha chakula na mazao ya biashara hapa nchini, wako katika hatari ya kutoweka kutokana na matumizi makubwa ya madawa ya kemikali za viwandani wakati wa msimu wa kilimo.

Mtaalamu wa nyuki Tanzania, Dk. Hendry Njovu ameeleza kuwa matumizi ya dawa za kemikali katika mashamba hayo husababisha nyuki kufa na kuweka viumbe hivyo katika hatari ya kutoweka.

Dk. Njovu alikuwa akizungumza katika kongamano la watafiti na wataalam wa mazingira lililofanyika katika Chuo cha Kimataifa cha Usimamizi na Uhifadhi wa Wanyamapori Tanzania maarufu kama Mweka.

"Tatizo la uharibifu wa mazingira limetahiri kwa kiasi kikubwa nyuki hawa kwa asilimia 90 ambao kimsingi ndio wanaotegemewa kwa ajili ya uchavushaji wa mazao ya chakula na biashara.

"Hivi sasa wako katika hatari ya kutoweka kwa sababu ya kuwapo kwa athari za mabadiliko ya tabia nchi na wakulima kutumia kemikali za viwandani msimu wa kilimo."

Kutokana na hatari hiyo, Dk. Njovu ameeleza kuwa nyuki hao kwa sasa wameanza kupotea duniani na kwamba nchi ya China kwa sasa wanategemea binadamu kufanya shughuli za uchavushaji jambo ambalo kwa nchi zinazoendelea litakuwa gumu kutokana na kutumia gharama kubwa.

Kwa upande wake, Mkuu wa Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Mweka, Prof. Japhary Kidegesho alieleza kuwa kama hatua za haraka za kuhifadhi nyuki hazitachukuliwa kuna hatari ya nchi kukumbwa na baa la njaa kutokana na wadudu hao wanaotegemewa kwa ajili ya uchavushaji wa mimea na miti kutoweka.

Hata hivyo, Mkufunzi mmoja wa chuo hicho, Dk. Oliver Nyakuga amesisitiza kuwa kutokana na hali hiyo, bado elimu inahitaji kwa wananchi kuhusu umuhimu wa nyuki na kwamba mbali na upatikanaji wa chakula, wadudu hao ambao ni muhimu kwa maisha ya kibinadamu.

Andiko la Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa (FAO) kuhusu umuhimu wa nyuki pia linasema, 'uhai wa nyuki ni ustawi wa binadamu.'

FAO inaeleza wazi kuwa zaidi ya asilimia 75 ya chakula kinachozalishwa duniani kinategemea wadudu wachavushaji maua kama vile nyuki ambao hata hivyo uwepo wao duniani uko hatarini.



Waziri wa Madini, Doto Biteko, akiwa na viongozi wa kampuni ya Acacia wa mgodi wa North Mara ofisini kwake jijini Dodoma. Kulia ni Mbunge wa Viti Maalumu mkoa wa Mara, Agness Marwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ufugaji holela wakausha vyanzo vya maji

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

UFUGAJI holela na shughuli za kilimo zisizozingatia kanuni za utunzaji na uhifadhi wa mazingira unaofanywa na baadhi ya wafugaji katika Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro umesababisha kukauka kwa vyanzo vinane vya maji.

Vyanzo vya maji vilivyokauka mpaka sasa ni vile vilivyopo katika Kijiji cha Chemka ambavyo miti ya asili iliyokuwa kando kando ya maji hayo pia imetoweka.

Taarifa za kukauka kwa vyanzo hivyo ilithibitishwa na Mkuu wa Wilaya hiyo Lengai Ole Sabaya, baada ya kufika katika eneo hilo na kujionea uharibifu uliofanyika.

Kutokana na hali hiyo, Sabaya ametoa siku 18 kwa wataalam wa halmashauri hiyo kuweka mikakati ya haraka ya kupanda miti katika vyanzo hivyo pamoja na kuweka alama za mipaka mita 60.

"Nawapa siku 18 wataalam wa mazingira katika wilaya yetu, muwe mmetengeneza mpango mkakati wa kupanda tena miti mingine kuzunguka vyanzo hivyo mkishirikisha wananchi wa eneo husika, lakini pia zuieni wakulima na wafugaji kuingiza mifugo katika vyanzo vya maji,"alisema

Januari 31 mwaka huu, Bunge lilipitisha Muswada wa Sheria za Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira wa Mwaka 2018 ambao ndani yake kuna adhabu zilizowekwa ikiwemo mtu atakayepatikana kwa kosa la matumizi ya mabaya ya maji kutozwa faini ya kati ya Sh. milioni 5 hadi Sh. milioni 10.

Kwa kuwa sheria hiyo bado haijasainiwa na Rais Dk. John Magufuli na kuanza kutumika rasmi, Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004, Kifungu cha 57 (1), kinapiga marufuku shughuli za binadamu ndani ya mita 60 kutoka kwenye maeneo ya vyanzo vya maji.

Baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Chemka akiwamo Saleh Mshana na Tinini Lenjadai walizungumza muda mfupi baada ya serikali kufika katika eneo hilo, walidai kuwa kwa sasa wanakabiliwa na uhaba mkubwa wa maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani pamoja na umwagiliaji kutokana na vyanzo hivyo kukauka

"Hiki kijiji kilikuwa na vyanzo vya maji 16, lakini leo vilivyopo ni vichache na hata hivyo vilivyosalia havina maji ya kutosha kwa sababu watu wameharibu mazingira yake. Sasa endapo serikali haitaingilia kati kuzuia uharibifu wa mazingira unaofanywa na wakulima na wafugaji hali hii inaweza kuwa mbaya zaidi,"alieleza Mshana

## Ushirika kuuza kahawa kwa kampuni ya Japan

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

USHIRIKA wa vyama 32 vya ushirika wa kahawa mkoani Kilimanjaro (G32 KNCI-JVE Ltd), umetangaza kuuza kahawa yake tani 76.8 kwa kampuni ya Zensho ya Japan, kwa thamani ya Dola za Marekani 437,700.

Meneja wa ushirika huo, Gabriel Ulomi, amesema kwa sasa wako katika maandalizi ya kusafirisha kahawa hiyo kwenda nchini Japan.

Ulomi alikuwa akizungumza na Nipashe jana katika mahojiano maalum kuhusu mauzo ya kahawa na maendeleo ya mradi huo wa pamoja.

"Muda si mrefu, wakulima wataanza kunufaika na pesa za mauzo ya kahawa yao kutoka nchini Japan. Kampuni ya Zensho, licha ya kununua kahawa yetu, pia imekuwa ikitusaidia kuboresha afya za wakulima hususani afya ya mama na mtoto kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano,"alisema

Alisema Kampuni ya Zensho imekuwa na mahusiano mazuri ya muda mrefu na muungano wa vyama hivyo na kwamba mwaka huu pia wanakusudia kununua kahawa inayozalishwa bila ya kutumia dawa na mbolea za viwandani.

Zaidi ameeleza kuwa Zensho wanakusudia kununua kahawa inayozalishwa kwa njia ya kilimo hai kutoka kwa wakulima wa Mwika, Kinyamvuo na Mamba Kaskazini.

Kufuatia mafanikio hayo, Ulomi amewashauri wakulima wa kahawa mkoani Kilimanjaro kuanza kulima kilimo kisichotumia dawa wala mbolea za viwandani ili kupunguza gharama za uzalishaji la kulinda afya za wanywaji wa kahawa.

Amedai kuwa soko la kahawa linaelekea kwenye uzalishaji wa zao la kahawa isiyotumia dawa na mbolea za viwandani ili kuongeza pato la mkulima na kwamba mwaka huu kampuni ya Zensho linakuja hapa nchini kutoa elimu kwa wakulima kuhusu namna ya kuzalisha kahawa pasipo kutumia dawa na mbolea.

Alisema kampuni ya Zensho inataka kuhakikisha wakulima wanazalisha kahawa bora lakini mwaka huu, Kampuni ya Zensho tayari imetoa Dola za Marekani 33,000 kwa ajili ya kuboresha afya ya mama na mtoto.



Ukurasa 18

Matumaini mapya



Ukurasa 14

Mradi mpya wa benki kuwasogezea wafugaji Tanzania ya Viwanda



## AUAWA NA SIMBA ANAOWAFUGA

Ukurasa 15


# BUFE

Ijumaa Machi 15, 2019

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA




# Dakika 60 za Waziri Lukuvi jijini Mbeya zaendelea kutimua vumbi

**Na Nebart Msokwa,** Mbeya

MWISHONI mwa mwezi Januari mwaka huu, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, alifanya ziara ya kushtukiza katika Wilaya ya Mbeya.

Hapo akawa mgeni wa watendaji wa Idara za Ardhi na Mipango Miji wa halmashauri zote mbili za wilaya hiyo.

Waziri Lukuvi, alitumia saa moja katika ofisi za Jiji la Mbeya, alipogeuka shubiri kwa watumishi wa Idara ya Ardhi na Mipango Miji, jijini Mbeya kutokana na mazito aliyoibua katika ofisi hiyo.

Akizungumza na watendaji hao kwenye kikao kilichofanyika katika Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya na kuhudhuriwa na maofisa na wapima ardhi, kutoka katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, pamoja na wataalamu kutoka Ofisi ya ardhi ya Kanda, alisema ameabaini 'madudu' kadhaa katika eneo lao la kazi.

INAENDELEA UK.16

UCHUMI

## Habari katika picha



Ukurasa 17

KIUCHUMI ZAIDI Ukurasa 19

Takwimu za Biashara Ukurasa 20

Muhtasari wa Soko

## Biashara

Jumla ya Mauzo (bln) 22,136.24

Mauzo 109,584,255.00
Hisa 58,317

**Kielezo**

| | | |
|---|---|---|
| TSI | 4,207.58 | +0.00 |
| DSEI | 2,296.50 | -37.11 |

**ZILIZOPANDA**


| KAMPUNI | Bei | Badiliko% |
|---|---|---|
| KA | 180 | -2.70% |
| JHL | 9,500 | +1.06% |
| SWIS | 3,760 | +7.43% |
| EABL | 5,320 | -1.66% |

**ZILIZOSHUKA**

| KAMPUNI | Bei | Badiliko% |
|---|---|---|
| TCCL | 1,200 | -11.76% |
| ACA | 5,550 | -2.63% |
| NMB | 1400 | -1.41% |
| NMG | 2,510 | -1.57% |
| KCB | 840 | +2.44% |

UCHUMI

# Mradi mpya wa benki kuw wafugaji Tanzania ya Viw



Shughuli za ufugaji katika mandhari tofauti, ambazo zinatumia njia za asili. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**Na Renatha Msungu,** Dodoma

MOJA ya sheria, sera pia miongozo inayosimamia kampuni na mashirika ya ndani na nje ya nchi, ni kuwajibika kwa jamii, kuhudumia mambo mbalimbali ambayo jamii jirani inaweza kunufaika na shughuli za asasi husika.

Aidha, shughuli za kitaasisi ambazo zinafanyika na hasa za kibiashara, zinatakiwa kugusa malengo ya kitaifa kuichumi. Hapo ikajulikana mojawapo, ni mkongwe kilimo, ambayo ni 'uti wa mgongo' wa taifa.

Benki ya NMB katika kujipanga kwake kuwainua kiuchumi wakulima na wafugaji, imeendana mpango bajeti yake katika miaka mitano ijayo, kwa ajili ya kuwahakikisha wanainuka kiuchumi.

> **"Kwa kweli tumejipanga sana labda wafugaji na wakulima washindwe kuja kuzikopa fedha hizo ili kujiendeleza.**

Inaelezwa katika mpango huo, kuna sura inayohusu kuanzishwa viwanda vidogo vya uzalishaji maziwa pamoja na wakulima kujiinua katika soko la nje na ndani ya nchi.

Meneja Mwandamizi wa Idara ya Kilimo ya Benki ya NMB, Carol Nyangaro, anasema benki yake imetenga Sh. bilion 500 za kuwainua kiuchumi na tayari wakulima wameshaanza kukopa ili kujiendeleza na kilimo kwa ujumla.

Kwa mujibu wa Nyanagaro, ni mpango ulioanza kufanyiwa kazi mwaka 2015 na unakamilika mwakani, huku akijigamba kuona mabadiliko katika kilimo hicho kinachofadhiliwa na mpango wa benki kupitia mkopo tajwa.

Mtazamo huo unakamata sura mbili za kilimo na ufugaji, amba-



BIASHARA

Dakika 60 za Waziri Lukuvi jijini Mbeya zaendelea kutimua vumbi

Ukurasa 16

UCHUMI

Matumaini mapya wakulima Chai Kilolo

Ukurasa 18

BIASHARA

JICA ilivyovaa kiatu kuisindikiza nchi safari Tanzania ya Viwanda

Ukurasa 19


# wasogezea anda



zo ni sekta mbili zenye uhusiano wa karibu sana na zinaangukia katika kundi moja la tafsiri na hata uwajibikaji.

Kutokana na hilo, wakopeshaji hao wanawataka wakulima na wafugaji kujitokeza kuchangamkia fursa hiyo ya fedha zilizotolewa ili kuhakikisha wanafanikisha wanachokikusudia mbele ya jamii.

Mbali na ufugaji, pia benki hiyo inawajibika na ukopeshaji katika maeneo mengi ya umma.

Nyangaro anaiabia Nipashe kuwa, hivi sasa wafugaji na wakulima kupitia mikopo hiyo wameanza kuonesha mabadiliko makubwa katika biashara zao ikiwemo uzalishaji mzuri wa maziwa, mtazamo wa mbali akiamini yatafikia kusafirishwa nje ya nchi.

Mkoa wa Dodoma ni sehemu mojawaopo ya maeneo mengi nchini na hasa mkoa ya Kanda ya Kati, ambako ufugaji uko juu na kwa maana hiyo hata uzalishaji maziwa uko katika kiwango kikubwa kiasi cha kukosa soko.

Pia, katika rekodi, Tanzania pia ni miongoni mwa nchi zilizo na ufugaji wa wanyama kama ng'ombe na mbuzi, katika ngazi ya juu zaidi barani Afrika.

Nyangaro anasema, kuwa katika mpango wa muda mrefu wa aina hiyo ya mkopo, ni kwamba wanalenga kutoa msukuko wa kimtaji na kiuwekezaji, utakaofikisha nchi kuwa na mtaji wa kutosha, ili kuhakikisha wafugaji na wakulima wanaingia katika soko la kimataifa.

"Kwa kweli tumejipanga sana labda wafugaji na wakulima washindwe kuja kuzikopa fedha hizo ili kujiendeleza," anasema Nyangaro.

Anasema NMB itahakikisha wanasonga mbele katika kutekeleza mpango mkakati wao, wanaoamini utaisaidia sana jamii katika sekta hiyo.

### WAZIRI MPINA

Anasema, wameamua kuitisha mkutano wa wadau wa wafugaji na wakulima, kupitia wizara husika chini ya Waziri wa Mifugi na Uvuvi, Luhaga Mpina, ili kuhakikisha changamoto zote zinazowakabili, zinatatuliwa, bila ya kujali ukubwa wa tatizo.

Nyangario anafafanua kuwa, tayari wameshaweka mkakati wa kuwafikia wakulima na baadaye wafugaji, ili waweze kupata fedha hizo kwa ajili ya kujiendeleza katika kazi zao za kila siku.

Anasema, wameandaa mipango ya kipekee inayofuatilia kilimo na kuongeza idara hiyo inafanya vizuri na tayari asilimia 40 ya fedha zilizotengwa tayari zimepelekwa kwa wakulima kwa ajili ya kuendeleza kilimo.

Waziri Mpina mwenye dhamana ya Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina anakiri kuwa ni jambo zuri lililofanywa na benki ya NMB na mfano wa kuigwa, kwa sababu wameamua kuiendeleza sekta hiyo.

Waziri Mpina anaekeza imani yake, endapo itatekeklezwa ilivyolengwa pia na taasisi nyinginezo basi, sekta hiyo itakuwa juu na kusaidia uzalishai wa maziwa kufikia kiwango cha juu kama ilivyo kwa nchi jirani ya Kenya, ambayo iko juu katika uzalishaji wa bidhaa za mifugo.

"Tunaishukuru NMB tunaomba mpango mkakati wao uendelee hivi hivi," anasema Mpina na kufafanua kuwa, zaidi kwamba endapo uzalishaji wa maziwa utaongeza tofauti na ilivyo sasa, basi soko litakuwa kubwa na kuzifikia nchi za jirani katika uzalishaji wa maziwa ya ng,ombe.

Anasema, hivi sasa Watanzania wanazalisha lita billion 2.4 kwa mwaka, wakati Kenya wako katika kiwango cha lita bilion 5.7, jambo ambalo ni fedheha ukilingaisha na kiwango cha mifugo iliyopo nchini.

Waziri anasema, Tanzania ina malisho mazuri, lakini imeachwa nyuma na majirani kama Kenya, huku akirejea imani yake kwa mpango wa NMB, kwamba wafugaji watauchangamkia ili kuweza kuinua uzalishaji kiwango cha maziwa na kuingia katika soko la ushindani.

### MFUGAJI

Mfugaji Peter Mlewa, anasema wana kila sababu ya kushukuru mradi huo, kutokana na kuwakumbuka sekta hiyo ambayo imekuwa ikisahaulika kila wakati.

Mlewa anasema, kwa sasa wataitumia vema nafasi waliopata kutoka benki hiyo kuhakikisha wanafikia malengo yao ya uzalishaji maziwa mengi ambayo yatasambazwa hadi nchi za jirani.



# Simba aliyemuua mmiliki wake



Simba aliyemuua mmiliki wake. **PICHA: BBC**

MWANAMUME mmoja, ameshambuliwa na simba aliyemfuga nyumbani kwake mashariki mwa Jamhuri ya Czech.

Michal Prasek, alimiliki simba huyo mwenye miaka tisa na simba jike aliyemfuga kwa ajili ya kuzalisha, hatua inayoarifiwa kuzusha wasiwasi kutoka kwa wakazi jirani.

Baba wae Prasek, aliupata mwili wake ndani ya kizuizi cha simba huyo na kuambia vyombo vya habari, kwamba kilikuwa kimefungwa kwa ndani.

Wanyama hao waliokuwa wanaishi katika vizuizi tofuati, walipigwa risasi na kuuawa na polisi walioitwa katika eneo hilo kufuatilia mkasa huo.

Msemaji wa Polisi, aliwaambia waandishi habari kwamba, ilikuwa muhimu kwa simba hao kuuawa ili kumfikia marehemu.

Prasek, mwenye umri wa miaka 33, alimnunua simba huyo mwaka 2016 na simba jike huyo mwaka jana na aliwaweka wote katika vizuizi alivyoviteneza katika ua la nyumbani kwake, katika kijiji cha Zdechov.

Awali alikatazwa ruhusa ya kujenga vizuizi hivyo na alitozwa faini kwa kufuga wanyama hao kinyume na sheria.

Lakini, mvutano wake na maofisa wa serikali, ulikwama baada ya kukataa kuruhusu mtu yeyote kuingia kwake.

Ukosefu wa vituo mbadala katika Jamhuri hiyo ya Czech, imemaanisha kwamba haingewezekana wanyama hao kuondolewa kwa lazima.

Prasek aliteka vichwa vya habari vya vyombo mbalimbali mwaka jana, baada ya mwendesha baiskeli kupambana na simba hao wakati Prasek alipokuwa akiwatembeza, huku akiwa amewafunga kwa nyororo.

Baada ya polisi kuingilia kati, tukio hilo lilitazamwa kama ajali ya trafiki.

"Tukio la leo huenda likasaidia hatimaye kutatua tatizo hili la muda mrefu," anasema Meya wa Zdechov, Tomas Kocourek. **BBC**

**BEI YA MAZAO** >> MCHELE 186363.64/- | ULEZI 140947.37/- **FEDHA** >> RAND 165.91 | KSH 22.97 | USH 0.62

UCHUMI

# Dakika 60 za Waziri Lukuvi jijini Mbeya zaendelea kutimua vumbi

## • Ardhi yatekeleza maagizo kwa Mchakamchaka • RC Chalamila amfuata mtangulizi 'hapa kazi tu' • Meya: Kinachotuumiza siasa, tuzipishe kidogo

**INATOKA UK.13**


Mandhari ya katikati ya jiji la Mbeya, inayvoonekana kutoka angani. **PICHA: MILARDAYO**

Hilo lilianzia pale alipowahoji maswali mbalimbali kuhusu utendaji kazi wao, akasema amebaini kuwa watumishi hao hawana ratiba maalum inayowaongoza kutekeleza majukumu yao, hali iliyomkera na kutishia kuwachukulia hatua kali.

Vilevile anasema, alibaini kuwa watendaji hao wana kasi ndogo ya upimaji viwanja, urasimishaji wa makazi ya wananchi na ukusanyaji kodi ya ardhi, huku akirejea takwimu zilizoko wizarani zinaonyesha kuwapo madeni makubwa.

**'MADUDU' ARDHI**

Kaimu Mkuu wa Idara ya Ardhi na Mipango Miji wa jiji hilo, Emeliana Kihunrwa, alikiri kutokuwapo ratiba yoyote katika maandishi, isipokuwa wanatenda kwa kukubaliana kazi za kufanya kupitia vikao.

Ni majibu yaliyoonekana kumkera Waziri Lukuvi, ndipo alipoanza kuibua mapungufu mengine ya utendaji wa sekta ya ardhi, ndani ya jiji hilo.

Waziri Lukuvi, anasema Mbeya ni mji unaomkera kutokana na mpangilio duni wa makazi unaosababishwa na maofisa ardhi na mipango miji, kutowajibika ipasavyo kwenye majukumu yao.

Anasema, wananchi wanalazimika kujipanga kulingana na eneo mtu analolimiliki na kwamba maeneo mengi ya makazi hayajapimwa, pia wamiliki hawana hati miliki za maeneo hayo.

"Jiji hili halinifurahishi kwenye masuala ya ardhi. Hamna 'master plan' (mpango mkuu) ya mji na ndio maana, kila mtu anajenga anavyojua, wala hamuonyeshi kushtuka na mpangilio huo," anasema Lukuvi.

Anasema kasi ndogo ya upimaji viwanja na kuwamilikisha wananchi, inasababisha kuipotezea mapato serikali, kwani watu wanamiliki nyumba na viwanja, bila ya kulipia kodi kwa mujibu wa sheria.

Waziri anasema, taarifa za jiji hilo zilizopo wizarani kwake, zinaonyesha kuwa viwanja vilivyopimwa ni 26,500 lakini vilivyotolewa hatimiliki havizidi 23,000, hali inayofanya zaidi ya viwanja 3000 kuendelea kumilikiwa na watu, lakini hazilipi kodi.

Lukuvi huku akionyesha uerevu mkubwa katika utendaji unaohusu

> **"Jiji hili halinifurahishi kwenye masuala ya ardhi. Hamna 'master plan' (mpango mkuu) ya mji na ndio maana, kila mtu anajenga anavyojua, wala hamuonyeshi kushtuka na mpangilio huo.**

wizara yake, anasema ukusanyaji wa kodi za ardhi katika jiji hilo ni duni, kwani asilimia 70 ya wananchi wanamiliki nyumba na viwanja, lakini hawalipii kodi ya serikali.

Kutokana na hilo, Waziri Lukuvi anawafananisha maofisa hao na wahujumu uchumi na amewaagiza watendaji hao, kuanza kutekeleza majukumu yao ipasavyo, akiwapa muda hadi mwisho wa mwezi huu, viwanja vyote vya watu visiyolipiwa kodi, viwe vimeshaingia katika mfumo wa kodi.

**UCHELEWEHAJI HATI**

Baada kikao hicho kilichowaweka 'kitimoto' watendaji hao, Waziri Lukuvi alihamisha ziara yake katika Ofisi ya Kutunza Kumbukumbu za Idara ya Ardhi ya Jiji, alikodai kubaini udhaifu mkubwa zaidi.

Anasema, kulikuwapo ucheleweshaji wa makusudi katika utoaji hatimiliki za nyumba na viwanja zilizoombwa na wananchi, huku wengine wakiwa wamecheleweshewa kwa zaidi ya miaka 10, baada ya kukamilisha taratibu zao.

Wakati akiendelea na upekuzi, alieleza kubaini kuwapo mwananchi aliyepeleka maombi tangu mwaka 2011 na alilipia Sh. milioni 1.5, lakini mpaka sasa faili lake halijawahi kushughulikiwa na mtumishi yeyote wa idara hiyo.

Kutokana na hali hiyo, aliwaagiza Wakuu wa Idara za Ardhi katika Halmashauri zote nchini, kuwapatia hati wananchi wote waliocheleweshewa ili


Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, akifanya ukaguzi katika Masijala ya Ardhi, katika Halmashauri ya jiji la Mbeya, mwishoni mwa Januari mwaka huu, alipofanya ziara ya ghafla. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

waanze kulipa kodi.

Pia, akatumia fursa hiyo kuwaagiza wakuu hao wa idara kumpelekea orodha ya maofisa waliochelewesha hati hizo, ili wachukuliwe hatua za kisheria, kwa madai ni kitendo sawa na uhujumu uchumi unaoipotezea serikali mapato.

"Hawa sio wajinga kuacha mafaili yote haya bila kuyafanyia kazi. Watakuwa wanatengeneza mazingira ya 'kunywa' na inawezekana 'wamekunywa sana.' Sasa nataka wote walioomba wapatiwe haraka na muanze kukusanya kodi," aliagizwa Lukuvi.

**MKURUGENZI AKIRI.**

Mkurugenzi Mtendaji wa Jiji la Mbeya, James Kasusura, alikiri jiji lake kutokuwa na mpangilio mzuri na zaidi ya asilimia 90 ya makazi, yako kiholela.

Kasusura anasema, katika kukabiliana na hali hiyo, tayari wamepata ufadhili wa Benki ya Dunia, kwa ajili ya kuandaa ramani ya jiji hilo na wapo katika hatua za mwisho kuanza kazi hiyo.

"Kwa sasa tupo katika harakati za kupima zaidi ya viwanja 50,000 kwa ajili ya New Mbeya City katika eneo la Nsoho na nimemtuma Ofisa Ardhi jijini Dar es Salaam, kwa ajili ya kwenda kuonana na wafadhili wetu, kukamilisha taratibu," anaeleza Kasusura.

**MAKALA AKUMBUKWA**

Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Jeremia Minja, amemweleza Waziri Lukuvi, anamtaja aliyekuwa Mkuu wa Mkoa, Amos Makalla, aliyeko Katavi sasa, alifanya juhudi kubwa kuleta mabadiliko ya mpangilio wa mji.

Minja anasema, awali hali ilikuwa tete zaidi, kabla kazi hiyo ya msukumo wa Makalla kufanyika, huku akifafanua kuwapo changamoto nyingi ya migogoro ya ardhi ndani ya na mkoa kiujumla, ambayo Makalla alianzisha utaratibu wa aina yake wa kusikiliza kero na kisha kuzitatua.

Kwa mujibu wa ratiba hizo, ambazo Makalla alijiwekea, vivyo hivyo akawaagiza wakuu wa wilaya nao kuzifuata, ni kila Alhamisi, mwanzo na mwisho wa mwezi, alisikia kero za wananchi na kuzitolea maamuzi.

Vilevile, Minja anasema, lilianzishwa dawati maalumu katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, kwa ajili ya kupokea malalamiko ya wananchi na kuyaandalia utaratibu wa kuyashughulikia, hivyo migogoro mingi ikawa imepatiwa ufumbuzi.

"Hili Jiji lilikuwa na matatizo mengi. Hiki kitengo cha ardhi ndicho kilichokuwa kinalalamikiwa zaidi na wananchi, hivyo hawa wataalamu walifanya kazi ya kutatua migogoro badala ya majukumu yao na wakati huo 'it was real worse' (hali ilikuwa mbaya sana)," anasema Minja.

**MOTO WA RC**

Siku chache baada ya Waziri Lukuvi kuondoka, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila 'aliwawashia moto' watendaji wa Idara ya Ardhi na Mipango Miji, akiwanyooshea kidole cha uzembe na ndio mzizi wa mpangilio mbovu wa makazi.

Chalamila alitoa mtazamo huo wa ukali, katika kikao kilicholenga kuhamasisha usambazaji wa vitambulisho vya wajasiriamali, pamoja na wakuu wa wilaya, wakurugenzi wa halmashauri zote za mkoa huo na watumishi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA),

Alitoa mfano uliobeba haiba ya aibu, kwamba Maofisa Ardhi na Mipango Miji, wamefikia hatua ya kuuza maeneo ya wazi yayotengwa na serikali kwa ajili ya shughuli mbalimbali.

Aliwapa siku 14, maofisa hao kuainisha maeneo yote yaliyotengwa kuwa ya wazi na kumpelekea orodha na baada ya hapo, ataanzisha oparesheni maalumu ya kubomoa nyumba zilizojengwa kwenye maeneo hayo.

"Waziri Lukuvi alipokuja juzi hapa alisema jiji hili limepangwa ovyo. Sasa sijui kazi ya maofisa ardhi na mipango miji ni ipi? Maana Jiji letu halina sifa kabisa, sasa nataka mniletee orodha ya maeneo yote ya wazi na kama kuna eneo mtu amejenga nyumba nitabomoa," anatamka Chalamila.

Pia, akataja kashfa ya hatua ya maofisa hao kupima na kuuza eneo la Uwanja wa Ndege wa Zamani, huku akiapa kuwashughulikia wote waliohusika na upimaji huo.

Ardhi Mbeya yaamka

Mwishoni mwa Mwezi uliopita, ikiwa ni mwezi mmoja baada ya Waziri Lukuvi 'kutimua vumbi,' Halmashauri ya Jiji la Mbeya, lilitia saini makubaliano na kampuni binafsi, kwa ajili ya kuandaa mpango wa kuupanga mji huo (Master Plan).

Ofisa Mipango Miji wa Mbeya, Patrick Mwakilili, anasema ni mradi uliofadhiliwa na Benki ya Dunia, kupitia Mpango wa Uendelezaji Mji Kimkakati huku ukiwa ni mkataba wa miezi 18.

Anasema, mpango huo utahusisha upangaji wa matumizi ya jumla ya matumizi ya ardhi, huduma za kijamii na miundombinu, ili kuboresha hali ya mazingira, kiuchumi na kijamii kwa wananchi.

Mwakilili anasema matarajio ni kwamba, mpango utasaidia kuupangilia vizuri mji, huo ili kuwa na mwonekano mzuri na unaendana na hadhi ya jiji kwa muda wa miaka 20 ijayo, hadi mwaka 2039.

Meya wa Jiji la Mbeya, David Mwashilindi, anaahidi mkandarasi husika kupewa ushirikiano kwa kadri inavyostahili, katika hatua hiyo ya Jiji la Mbeya, kuondokana na makazi holela.

Anatumia nafasi yake, kuwataka watendaji wa jiji, kuweka kando siasa na kuchapa kazi kufikia malengo ya majukumu yao, akidai siasa ndio zimekuwa zinakwamisha shughuli za maendeleo.

# Biashara katika picha


Spika wa Bunge, Job Ndugai (kushoto), akimsikiliza Meneja wa TPB Benki Tawi la Dodoma, Edward Mlowo (katikati), walipotembelea ofisini kwake bungeni Jijini Dodoma jana. Kulia ni Ofisa Mikopo wa benki hiyo, Hamis Salehe. **PICHA: OFISI YA BUNGE**


Mkazi wa jiji la Dar es Salaam akijaribu bahati yake katika mchezo wa gurudumu la bahati uliowekwa nje ya banda maalum la Diamond Trust Bank Tanzania (DTB-Tanzania) kwenye viwanja vya Mlimani City jijini Dar es Salaam likitoa huduma kwa wateja ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani. **NA MPIGAPICHA WETU**



Meneja wa Huduma ya Airtel Money, Fidelis Kaijage, akizungumza jijini Dar es Salaam wakati akitangaza kugawa faida ya jumla ya Sh.bilioni 2.1 kwa wateja na mawakala wa Airtel Tanzania ambao wametumia huduma ya Airtel Money kwa miezi sita iliyopita kati ya Aprili na Septemba, 2018 . Kushoto ni Meneja wa Mawasiliano na Uhusiano Airtel Jackson Mmbando. **NA MPIGAPICHA WETU**

BEI YA MAZAO >> MAHINDI 50704.35/-| MAHARAGE 175000.00/-

UCHUMI

# Matumaini mapya wakulima Chai

• Ni matokeo ya mazungumzo kati ya uongozi wa wilaya na Benki ya Maendeleo ya Kilimo



Mashamba ya chai kama hili pamoja na kufufuliwa kwa kiwanda cha chai, kutaleta mapinduzi makubwa Kilolo. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Epson Luhwago**

ILIKUWA kiu ya siku nyingi lakini sasa si kiu tena. Maneno hayo yanasadifu na kutimia njozi za siku nyingi za wananchi wa Kilolo mkoani Iringa juu ya uwapo wa kiwanda cha kuchakata chai wilayani humo.

Kwa miaka mingi, wananchi wa wilaya hiyo hasa tarafa ya Kilolo ambako sehemu kubwa ya ardhi yake inafaa kwa kilimo cha zao hilo, walikuwa na matumaini makubwa ya kujikomboa kiuchumi kupitia chai.

Miaka ya 1980 kilimo hicho kilianzishwa rasmi na iliyokuwa Mamlaka ya Chai Tanzania na wakulima hasa katika kijiji cha Kidabaga na vya jirani, walijitokeza kwa wingi kuanza kuzalisha. Kasi hiyo na shauku ya wananchi ilitokana na kuwapo kwa kiwanda kidogo katika eneo hilo.

Lakini kama msemo wa "furaha ya nyani huishia jangwani" matumaini ya wananchi hao yaliyeyuka baada ya kufungwa kwa kiwanda mwishoni mwa miaka ya 1990. Hatua hiyo ilisababisha mashamba ya chai yaliyokuwa yamestawi kugeuka mapori.

Jitihada mbalimbali zilifanyika ili kufufua kiwanda hicho na kurejesha matumaini ya wakulima yaliyokuwa yamezimika kama mshumaa katika upepo mkali. Mazungumzo yalifanyika kati ya kampuni hiyo na serikali kuanzia mwaka 2006 wakati huo Profesa Peter Msolla akiwa Mbunge wa Kilolo na Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia na baadaye Kilimo na Chakula.

> **"Ujio wa mradi huo ni neema kubwa kwa wananchi wa Kilolo ambao walikuwa na kiu ya kuwapo kwa kiwanda ambacho kingewezesha kufufua kilimo cha chai na kuwakomboa kiuchumi.**

Hata hivyo, jitihada hizo ziligonga mwamba kutokana na mchakato huo kuingiliwa na masuala ya kisiasa, hivyo kubaki wimbo mzuri usioisha masikioni mwa watu na hatimaye matumaini yaliyokuwa yamefufuka yakafifia na hata kuona jambo hilo ni kama maji kupanda mlima.

Matumaini hayo yalifufuka baada ya uongozi wa serikali ya awamu ya tano kuingia madarakani. Mkuu wa Wilaya ya Kilolo, Asia Abdallah, baada ya kuteuliwa aliliweka suala hilo moja ya vipaumbele vya kuipaisha wilaya hiyo kiuchumi.

"Hakuna kinachoshindikana na hakuna kutaka tamaa, suala la kiwanda cha chai lazima tulivalie njuga kwani jambo hili ni mkombozi kwa wananchi wa Kilolo. Jambo la kwanza ni kuhamasisha wakulima kurejea tena mashambani na lingine ni kutafuta wawekezaji na wafadhili kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda," alisema mkuu huyo wa wilaya alipohojiwa miezi michache baada ya kuteuliwa kushika wadhifa huo.

**UTEKELEZAJI WAANZA**

Katika kuhakikisha ndoto hiyo inatimia, uongozi wa wilaya chini ya Abdallah ulianza mchakato wa kutafuta taasisi ambayo ingetoa mkopo wa kuendeleza kilimo cha chai na ujenzi wa kiwanda cha uchakataji wa zao hilo.

Hatimaye Septemba, mwaka jana, uongozi huo ulibisha hodi Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) na kufanya mazungumzo kuhusu utekelezaji wa azma hiyo.

Baada ya mazungumzo hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Japhet Justine, wakati huo akiwa anakaimu nafasi hiyo, alifunguka na kuthiibitisha kufanyika kwa mazungumzo kati ya benki hiyo na uongozi wa wilaya ya Kilolo.

Justine alisema katika mazungumzo na viongozi hao walijadili uwezekano wa kufufua kiwanda cha kuchakata chai ili kuongeza uzalishaji wa zao hilo lengo kubwa likiwa kuleta mapinduzi katika sekta ya kilimo ili kuwainua wakulima wadogo na wakubwa kutoka wilayani humo.

Pia alisisitiza kuwa katika mazungumzo yao, walijadiliana kuhusu uanzishwaji wa kiwanda ili kuhakikisha bidhaa ndogo kama majani ya chai yanatengenezwa nchini kwa ubora wa hali ya juu na kutumiwa ndani na nje ya nchi.

"Kuwapo kwa kiwanda hicho itakuwa moja ya njia za kuunga mkono azma ya serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Magufuli ya kujenga uchumi wa kati na wa viwanda ifikapo mwaka 2025 kwa vitendo," alisema.

Naye Abdalla aliushukuru uongozi wa TADB kwa kupokea wazo hilo litakalowezesha kutimia kwa ndoto hiyo lakini pia kwa jitihada zake za kuisogeza benki hiyo karibu na wakulima.

**YAMETIMIA**

Matokeo ya mazungumzo hayo yameanza kuzaa matunda baada ya TADB kutangaza zabuni ya ujenzi wa kiwanda cha chai wilayani Kilolo pamoja na maendeleo ya kilimo cha chai kwa ujumla.

Benki hiyo licha ya kutangaza zabuni hiyo, pia imeelezea kufadhili mradi wa uendelezaji wa kilimo cha chai unaofanywa kwa ushirikiano kati ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo, Chama cha Wakulima wa Chai wa Dabaga (Datega) na Kampuni ya Chai ya Kilolo (KTC).

Kupitia mradi huo, wanachama wa Datega wanamiliki hekta 3,600 ambazo zinafaa kwa kuanzisha mashamba madogo na makubwa ya chai, kiwanda cha kuchakata majani ya chai mashamba ya miti kwa ajili ya nishati ya mkaa.

Sambamba na eneo hilo, kuna ardhi yenye ukubwa wa hekta 10,000 zinazomilikiwa na wakulima wadogo katika vijiji 26. Ardhi hiyo inafaa kwa kuanzisha mashamba na uendelezaji wa kilimo cha chai.

**WAJIBU WA TADB**

Kupitia mradi huo, TADB inatarajia kutoa msaada wa kifedha kwa ajili ya uendelezaji wa mashamba ya chai katika hekta 3,600 zilizopo, ukarabati na uendelezaji wa hekta 184 zilizopo na uendelezaji wa wakulima wadogo wa chai katika kuibua fursa na kuongeza mashamba ya chai kutoka hekta 170 zilizopandwa chai hadi kufikisha hekta 13, 600.

Katika uendelezaji wa kilimo cha zao hilo, benki hiyo inakusudia uwezeshaji wa uanzishaji na uendelezaji wa kilimo cha mkataba cha chai na mashamba ya miti kwa ajili ya nishati iwapo kutakuwa na uhitaji huo.

Kwa upande wa kiwanda, benki hiyo inatarajia kuwezesha upatikanaji wa zana za kilimo kwa ajili ya kuongeza kasi ya uzalishaji wa majani ya chai katika mashamba yatakayoanzishwa, njia bora na za kisasa za uchumaji wa majani ya chai kwa kutumia teknolojia ya kisasa.

TADB kupitia mradi huo, inatarajiwa pia kutoa msaada wa kifedha kwa mwekezaji, kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa na benki hiyo ili kujenga kiwanda kitakachokuwa na uwezo wa kuchakata kilo 30,000 kwa siku, ujenzi wa vituo vya kukusanya majani ya chai na ununuzi wa magari ya kusafirishia majani kutoka mashambani mpaka kiwandani.

Ujio wa mradi huo ni neema kubwa kwa wananchi wa Kilolo ambao walikuwa na kiu ya kuwapo kwa kiwanda ambacho kingewezesha kufufua kilimo cha chai na kuwakomboa kiuchumi.

FEDHA >> USD 2300.38| Pauni 3065.26| Euro 2619.21

BIASHARA

# Namna biashara ya sanaa zinavyolindwa zisitetereke

Na Mwandishi Wetu

DUNIA ya sasa sanaa ni biashara na ubunifu ni mambo yanayowatajirisha mamilioni ya vijana iwe Marekani, China, India na hata Tanzania. Huu ni uwekezaji unaotumia talanta au vipaji vya aina mbalimbali ambao unahitaji kulindwa kisheria na kusimamiwa ili uwe na tija badala ya hasara na malalamiko.

Ubunifu huu unahusisha utunzi wa nyimbo, tungo za asili, mashairi , ngoma, mavazi, ugunduzi wa vitu mbalimbali kuanzia zana na uchongaji wa vinyago.

Moja kati ya masuala yanayowasumbua wasanii wengi na zaidi katika nchi zinazoendelea ni suala la hakimiliki na hakishiriki kwa wasanii na wabunifu wa sanaa. Ndiyo maana tunapenda kuwakumbusha wasanii wa Tanzania kusoma hii makala ili walinde kazi zao na kuwa wabunifu zaidi wasiibiwe.

Hapa nchini, mara baada ya sheria ya hakimiliki ya mwaka 1966 kuthibitika kwamba ina upungufu, mwaka 1999 Bunge lilitunga sheria mpya ya hakimiliki na hakishiriki namba 7 ya mwaka 1999, yenye sura ya 218 ya sheria za Tanzania kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2002.

Sheria hiyo imeletwa kulinda kazi za wasanii zinazolindwa na haki miliki na hakishiriki na nyingine zote zinazoendana na hizo. Kwa mujibu wa kifungu cha 2(c) madhumuni ya kutungwa kwa sheria hii ni kuhakikisha maendeleo ya wasanii, watunzi na wabunifu katika nyanja za nyimbo, maigizo na tasnia nyingine za kisanii.

Sheria hii ina madhumuni ya kuinua kazi za fasihi na za kisanii pamoja na nyingine zinazofanana na hizo.

Kwa mujibu wa sheria hii, kuna makundi makubwa mawili ya haki za wasanii zinazolindwa na sheria hii, ambazo ni haki ya kiuchumi na haki za kitamaduni ambazo mtunzi wa kazi zinazolindwa na sheria hii ana haki nazo.

Haki hizi, zinatokana na mkataba maarufu wa kimataifa wa Benne wa mwaka 1883 ambao Tanzania iliuridhia Julai , 1994 hivyo kuwa na wajibu wa kutimiza yaliyomo katika mkataba huo Hii ni kwa mujibu wa kanuni za sheria zilizomo katika mkataba huo wa kimataifa.

Kwa mujibu wa kifungu cha 3(i) inatoa angalizo kuwa, kazi zinazolindwa na sheria ni lazima ziwe zimetengenezwa na mtunzi Mtanzania au zile ambazo mtunzi wake si Mtanzania lakini ana makazi ya kudumu hapa nchini au kazi hizo zilizotengenezwa kwa mara ya kwanza hapa Tanzania, au ambazo ni za kusikika na kuona (audio-visual) ambazo mtayarishaji wake ni Mtanzania au makao makuu yake ya kutengeneza kazi hizo zipo hapa nchini.



Kazi za sanaa kama ngoma ya Muheme yenye asili ya Dodoma , bidhaa zinazotokana na kusuka ukiri kama kawa ambazo ni maarufu Visiwani Zanzibar, na kazi za sanaa za kuchora zikiwamo za Tinga Tinga, ni hazina ya utamaduni ambazo huzalishwa na vipaji ambavyo vinahitaji ulinzi kwa kutumia sheria vinginevyo huibiwa na kunufaisha wajanja wenye teknolojia na utaalamu wa kughushi. **PICHA: MTANDAO**

> **"Sharti la kazi za kisanii kulindwa na kigezo hiki ni iwe katika hali ya kushikika na kwamba mawazo hayatalindwa.**

Na kwa mujibu wa kifungu cha 3(3) wasanii wanaomiliki kazi za kisanii wana hakishiriki pia watapewa ulinzi na sheria hii. Katika kifungu cha 4, msanii ametafsiriwa kama mwigizaji, mwimbaji, mwanamuziki, mchezaji, au mtu anayeigiza, kuchonga au kufanya maonyesho jukwaani.

Sharti la kazi za kisanii kulindwa na kigezo hiki ni iwe katika hali ya kushikika na kwamba mawazo hayatalindwa.

Kwa mfano, kama A na B walio katika sehemu tofauti wana wazo linalofanana la kutengeneza wimbo unaohusu foleni za magari, na A akawa wa kwanza kuimba wimbo na kuurekodi B hawezi kumshitaki A kwa kumuiba wimbo, kwani alikuwa na wazo na wakati mwenzake ana video.

Kifungu hiki kinaendana na maamuzi ya Mahakama ya Uingereza katika shauri la University of London Press Ltd dhidi ya University Tutorial Press, (1916) 2 Ch.601 ambayo ilitafsiri maana ya kazi ya kisanii kumaanisha yaliyomo katika kifungu cha 5 cha sheria ya hakimiliki na hakishiriki ya Tanzania.



Kwa upande mwingine, imetaja baadhi ya kazi ambazo haziwezi kulindwa na sheria yenyewe ikiwa ni pamoja na habari zinazochapishwa au kutangazwa katika vyombo vya habari, sheria na maamuzi ya vyombo vya kutoa maamuzi kama mahakama na mabaraza, na pia wazo la aina yeyote ambalo halijawekwa katika hali ya kushikika na kudumu.

Haki ya kiuchumi katika sheria ya Tanzania, inapatikana chini ya kifungu cha 9, ambayo ni mtunzi wa kazi inayolindwa na sheria hii amepewa haki zote juu ya kazi yake, katika masuala yote yanayohusiana na kutafsiri kazi yake, kuikodisha, kuuonyesha umma, kupitia vyombo vya habari, kuisambaza au kuitumia hadharani.


# Takwimu za Biashara

Na Edward Ntwale & Elias Samweli

**Bei ya Mazao Ya Chakula kwa Sh/kilo 100 Machi 11, 2019**

| Mkoa | Arusha | DSM | Dodoma | Geita | Kagera | K'njaro | Kigoma | Manyara | Mbeya | Mwanza |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mahindi | 44,000 | 70,000 | 47,000 | 57,000 | 60,000 | 45,000 | 54,000 | 51,000 | 40,000 | 62,000 |
| Mchele | 200,000 | 230,000 | 180,000 | 130,000 | 185,000 | 180,000 | 180,000 | 200,000 | 150,000 | 180,000 |
| Mtama | 35,000 | 60,000 | 35,000 | 180,000 | 100,000 | 80,000 | 80,000 | 42,000 | 105,000 | NA |
| Uwele | 35,000 | 70,000 | 35,000 | 180,000 | 110,000 | NA | 60,000 | 100,000 | NA | 150,000 |
| Ulezi | 72,000 | 140,000 | 75,000 | NA | 150,000 | 180,000 | 150,000 | 120,000 | 120,000 | 160,000 |
| Ngano | 80,000 | 130,000 | 160,000 | 180,000 | NA | 100,000 | 150,000 | 120,000 | 130,000 | NA |
| Maharage | 155,000 | 210,000 | 175,000 | 170,000 | 150,000 | 180,000 | 130,000 | 150,000 | 210,000 | 160,000 |
| Viazi Mviringo | 70,000 | 90,000 | 65,000 | 70,000 | 75,000 | 65,000 | 90,000 | 50,000 | 50,000 | 80,000 |

## Mwenendo wa Shilingi




## Mafuta

**Bei : Kuanzia Machi 6, 2019**

| MKOA | DSM | Arusha | Pwani | Dodoma | Geita | Iringa | Kagera (Bukoba) | Katavi | Kigoma | Moshi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Petroli | 2,098 | 2,191 | 2,102 | 2,157 | 2,263 | 2,162 | 2,313 | 2,306 | 2,329 | 2,181 |
| Dizeli | 2,131 | 2,195 | 2,135 | 2,189 | 2,296 | 2,195 | 2,346 | 2,339 | 2,362 | 2,185 |
| M'Taa | 2,096 | 2,286 | 2,101 | 2,155 | 2,262 | 2,161 | 2,312 | 2,304 | 2,328 | 2,276 |

## Soko la Hisa la Dar es Salaam Kikao cha Machi 13, 2019

### Muhtasari

| | | |
|---|---|---|
| TSI | 3,481.50 | -9.94 |
| DSEI | 2,078.06 | -3.58 |
| Thamani za Hisa (bln) | 20,030.17 | |
| Mauzo | 112,850,875.00 | |
| Hisa | 884,582 | |

### Zilizopanda na Zilizoshuka

| Kampuni | Bei | Badiliko |
|---|---|---|
| CRDB | 125 | -7.41% |
| KA | 115 | -4.17% |
| USL | 15 | +50.00% |
| EABL | 4,700 | +0.43% |
| ACA | 6,300 | +0.80% |

### Viwango vya kubadilisha

| Fedha | Nunua | Uza |
|---|---|---|
| EUR | 2,591.28 | 2,617.65 |
| USD | 2,268.07 | 2,290.76 |
| KES | 22.38 | 22.56 |
| GBP | 2,947.82 | 2,977.52 |

## Bei za hisa hadi kikao cha Machi 6, 2019

| Kampuni | Bei ya mwisho | Bei Iliyopita | Ba'liko % |
|---|---|---|---|
| TICL | 385 | 385 | +0.00 |
| TCCL | 600 | 600 | +0.00 |
| TCC | 17,000 | 17,000 | +0.00 |
| TBL | 11,400 | 11,800 | -3.39 |
| SWIS | 2,000 | 2,340 | -14.53 |
| SWALA | 490 | 490 | +0.00 |
| PAL | 400 | 400 | +0.00 |

| Kampuni | Bei ya mwisho | Bei Iliyopita | Ba'liko % |
|---|---|---|---|
| NMB | 2,340 | 2,340 | +0.00 |
| NICO | 160 | 150 | +6.67 |
| MUCOB | 400 | 400 | +0.00 |
| MKCB | 800 | 800 | +0.00 |
| MCB | 500 | 500 | +0.00 |
| MBP | 490 | 490 | +0.00 |
| KCB | 990 | 970 | +2.06 |

| Kampuni | Bei ya mwisho | Bei Iliyopita | Ba'liko % |
|---|---|---|---|
| CRDB | 135 | 135 | +0.00 |
| ACA | 6,200 | 6,200 | +0.00 |
| TOL | 660 | 660 | +0.00 |
| TPCC | 2,020 | 2,020 | +0.00 |
| TTP | 120 | 120 | +0.00 |
| USL | 10 | 15 | -33.33 |
| VODA | 800 | 800 | +0.00 |

## VIWANGO VYA KUBADILISHA FEDHA

| FEDHA | KUNUNUA | KUUZA |
|---|---|---|
| KENYA SHS | 22.73 | 22.91 |
| UGANDA SHS | 0.58 | 0.62 |
| RWANDAN FRANC | 2.52 | 2.55 |
| BURUNDI FRANC | 2.18 | 2.20 |
| USD | 2277.37 | 2300.14 |
| POUND STG | 2996.33 | 3027.21 |
| EURO | 2573.20 | 2600.08 |
| CANADIAN $ | 1704.87 | 1721.40 |
| SWITZ. FRANC | 2263.56 | 2285.97 |
| JAPANESE YEN | 20.45 | 20.65 |
| SWEDISH KRONOR | 243.77 | 246.11 |
| NORWEG. KRONOR | 264.61 | 267.14 |
| DANISH KRONOR | 344.99 | 348.34 |
| AUSTRALIAN $ | 1608.05 | 1624.82 |
| INDIAN RPS | 32.74 | 33.05 |
| PAKISTAN RPS | 15.59 | 16.31 |
| ZAMBIAN KWACHA | 188.67 | 191.68 |
| MALAWIAN KWACHA | 2.91 | 3.12 |
| MOZAMBIQUE-MET | 36.21 | 36.51 |
| ZIMBABWE $ | 0.43 | 0.43 |
| SDR | 3161.55 | 3193.17 |
| GOLD (T/O) | 2975954.38 | 3006496.20 |
| S. AFRICAN RAND | 159.24 | 160.67 |
| UAE DIRHAM | 620.06 | 626.14 |
| SINGAPORE $ | 1679.85 | 1696.39 |
| HONK KONG $ | 290.11 | 293.01 |
| SAUD ARABIAN RIAL | 607.27 | 613.31 |
| KUWAIT DINAR | 7492.82 | 7562.02 |
| BOTSWANA PULA | 212.25 | 216.21 |
| CHINESE YUAN | 339.52 | 342.85 |
| MALAYSIA RINGGIT | 557.29 | 562.31 |
| SOUTH KOREA WON | 2.02 | 2.03 |
| NEWZEALAND | 1557.04 | 1573.53 |

## Interbank Foreign Exchange Market (IFEM)

| Tarehe | Idadi (Mn USD) | Juu | Chini | Wastani |
|---|---|---|---|---|
| **13/Mar/2019** | **4.60** | **2,312.65** | **2,298.94** | **2,300.14** |
| 12/Mar/2019 | 3.15 | 2,315.00 | 2,298.93 | 2,300.16 |
| 11/Mar/2019 | 3.95 | 2,313.00 | 2,298.95 | 2,300.20 |
| 8/Mar/2019 | 4.50 | 2,310.15 | 2,298.98 | 2,300.23 |

## Inter-bank Local Money Markets

| Tarehe | Kiasi (million-TZS) | Juu | Chini | Wastani (WAR) |
|---|---|---|---|---|
| **13/Mar/2019** | **40,100** | **6.50** | **4.50** | **5.58** |
| 12/Mar/2019 | 22,000 | 6.50 | 5.00 | 5.48 |
| 11/Mar/2019 | 36,000 | 6.50 | 5.00 | 5.49 |
| 8/Mar/2019 | 29,000 | 6.50 | 5.00 | 5.41 |
| 7/Mar/2019 | 8,000 | 6.50 | 4.90 | 5.46 |
| 6/Mar/2019 | 71,700 | 6.50 | 4.00 | 5.42 |

## Ziara ya kwanza Rais wa Ufaransa Kenya, ina nini?



Rais Uhuru Kenyatta, akimpokea mgeni wake, Rais Emmauel Macron wa Ufaransa, jijini Nairobi. **PICHA: MTANDAO**

RAIS Emmauel Macron wa Ufaransa, aliwasili jijini Nairobi, Kenya, yuko katika ziara ya siku nne ya nchi za Pembe na Mashariki ya Afrika Mashariki, kwa lengo la kuimrisha uhusiano wa kiuchumi na kijeshi.

Juzi alikutana na mwenyeji wake Rais Uhuru Kenyatta, walitarajiwa kuzungumzia jukumu la Kenya katika kuleta utulivu nchini Somalia, vita vyake dhidi ya ugaidi na kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi, kiutamaduni na kijeshi.

Rais Macron huyo, ni ziara ya kwanza kufanywa na kiongozi wa Ufaransa tangu Kenya kujinyakulia, uhuru wake 1963.

Akiwa huko Nairobi kiongozi huyo atahudhuria mkutano wa baraza la mazingira la Umoja wa Mataifa, linaloendelea kwa wakati uliopo na kukutana na viongozi wengine wa mataifa ya Afrika.

Ofisi ya Rais Macron, inaeleza kwamba Kenya ndio nchi pekee ya Afrika iliyofikia lengo la kufanya nishati mbadala kuwa asilimia 75 ya mahitaji yake ya nishati na hivyo watazungumzia ushirikiano katika nyanja za nishati.

Macron anafuatana na wakuu wa biashara kwa lengo la kuimarisha biashara kati ya nchi zao na kutia saini mikataba kadhaa ya biashara.

Mojawapo ya mikataba hiyo, ni mradi wa kiwanda cha kutengeneza magari 1,000 ya kampuni ya Peugeot mwisho wa mwaka 2019.

Wakati wa ziara hiyo kampuni za Kifaransa zitasaini mikataba na Kenya, yenye thamani ya Dola bilioni 2.26 (Sh. Trilioni 5.2).

Wachambuzi wanasema, ziara ya Macron inalenga kuongeza ushawishi wa Ufaransa katika kanda ya Afrika, ambako kuna Jumuiya ya Afrika Mashariki, pamoja na kushindana na ushawishi wa China ambao umepata nguvu katika nchi tatu anazotembelea, nazo ni Djibuti, Ethopia na Kenya.

Kabla ya kuwasili Nairobi, kiongozi huyo alikutana na mwenyekiti wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika (AU), Mossa Faki Mahamat, Mjini Addis Ababa, Ethiopia. .

Akiwa nchini Ethopia, alitia saini mkataba wa kwanza wa ushirikiano wa kijeshi na taifa hilo la Pembe ya Afrika, alitangaza msaada wa Dola milioni 96 (Sh. bilion 221) kwa ajili ya mradi huo, Rais Macron anasema: "Tumetia saini mkataba wa kijeshi mpya wa ulinzi ambao utaweka mpango wa kuimarisha ushirikiano na kufungua njia kwa msaada maalum kutoka ufaransa kusaidia Ethopia kuunda kikosi chake cha majini."

Macron anamsifu Waziri Mkuu wa Ethopia, Abiy Ahmed, kwa kuleta mageuzi ya haraka na muhimu katika nchi yake

"Muna Waziri Mkuu aliyewajibika miezi michache tu baada ya kuchukua madaraka. Yuko katika kuleta mageuzi makubwa ya kuimarisha uchumi na maendceleo ya nchi hii na kufanya kila kitu kuleta maridhiano kati ya wananchi wake na kudumisha amani katika kanda nzima," anaiongeza.

Kabla ya Ethiopia, Macron alifanya ziara nchini Djibouti ambayo ni moja ya washirika wa Ufaransa wakuu katika bara la Afrika, akilieleza koloni lake la zamani kuwa mshirika muhimu wa kihistoria na kijeshi na mlango muhimu kuingilia Pembe ya Afrika.

Ufaransa ina kambi yake kubwa kabisa ya kijeshi barani Afrika huko Djibouti sawa na Marekani na China. **VOA.**



# Ajali ya ndege ya Ethiopia yamuibua mkurugenzi ATCL

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

SIKU chache baada ya Ndege ya Shirika la Ethiopia kuanguka na kusababisha vifo vya watu 157 waliokuwa ndani yake, Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) limewatoa hofu wananchi kuhusiana na usalama wa ndege zake.

Mkurugenzi wa Uendeshaji wa ATCL, Capteni Said Hamad, alisema jana jijini Mbeya kuwa ndege za ATCL ni toleo tofauti na ndege ya Ethiopia iyoanguka hivi karibuni na wala hazina uhusiano.

Alisema toleo la ndege mpya za Tanzania ambazo ni aina ya Boeing 787-8, Airbus A220-300 na Dash 8- Q 400 ni zile zinazo aminika kiusalama na hazina rekodi mbaya kote dunani.

"Matoleo ya ndege zetu mpya ni tofauti na ndege ya Shirika la Ndege la Ethiopia iliyoanguka hivi karibuni, kwani ile ya Ethiopia ilikuwa ni Boeing 373 Max wakati sisi zetu ni toleo tofauti kabisa hivyo tutaendelea kuzitumia kwa sababu tunaamini ni salama" alisema Capt. Hamad.

Alisema kuwa matoleo ya ndege kama za Tanzania kwa sasa zinaaminika kuwa bora na salama na kwamba zimenunuliwa kwa wingi duniani kote kwa sababu zinaaminika.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila alisema kwa sasa idadi ya abiria kutoka Mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ambao wanatumia uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe uliopo mkoani Mbeya ni kubwa kiasi kwamba watu wananyang'anyana tiketi.

Aliliomba Shirika hilo kuongeza safari za ndege zake mkoani Mbeya ili kukabiliana na ongezeko hilo pamoja na kutoa huduma nzuri kwa wananchi.

Akijibu ombi hilo, Mkurugenzi Mtendaji wa ATCL, Mhandisi Ladislaus Matindi alisema shirika hilo litaongeza idadi ya ndege eneo hilo kutoka moja inayofanya kazi hivi sasa na kufikia tatu kuanzia Jumatatu ya wiki ijayo.

Alisema ndege zitakazoongezwa kwenye uwanja huo zitakuwa ni zile kubwa zenye uwezo wa kubeba abiria zaidi ya 200 na zitafanya safari zake mara nne kwa wiki kumaliza kabisa changamoto ya msongamano wa abiria.

Mhandisi Matindi aliwataka Watanzania kuliamini shirika hilo na kuelekeza wafanyakazi wa ATCL kufanya kazi kwa uadilifu ili kuongeza tija na kuvutia watu wengi zaidi kutumia usafiri wa ndege.



Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Emmanuel Maganga, akikata utepe wa kuzindua Sanamu ya Samaki aina ya Mgebuka katika barabara ya Lumumba eneo la Mwanga Sokoni jana katika Manispaa ya Kigoma/Ujiji. **PICHA: JOCTAN NGELLY**

# Serikali yashauriwa kuchukua hatua kunusuru zao la migomba

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

SERIKALI imeshauriwa kuchukua hatua za haraka kunusuru zao za migomba lililobainika kushambuliwa na kudhoofishwa na minyoo hatari iliyogunduliwa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Kituo cha Kibaha kilichopo mkoani Pwani.

Taasisi hiyo ilibaini kuwapo kwa minyoo hiyo ambayo hushambulia migomba na kusababisha athari nyingi ikiwamo mimea kubadilika rangi, kuzaa ndizi dhaifu na hatimaye mgomba kuanguka.

Akizungumza jana na Nipashe jijini Mbeya, Mtafiti kutoka Taasisi ya Kilimo, Kituo cha Kibaha, Ambilikile Mwanisongole, alisema wakati wanafanya utafiti walibaini kuwepo kwa aina tatu za minyoo ambayo ni michirizi, Fundo ambazo dalili zake ni kuota vinundu kwenye mzizi wa mgomba.

Mnyoo wa tatu ni Chimba ambao huchimba hadi chini ya mgomba na kusababisha kuoza na kueleza athari za minyoo hiyo kuwa ni mgomba kuanguka .

"Tulifanya utafiti katika mikoa inayolima kwa wingi zao la ndizi na tumebaini kuwapo kwa minyoo ambayo inatishia kudhoofisha zao hilo endapo hatua za haraka hazitachukuliwa kudhibiti kuenea zaidi kwa minyoo hiyo," alisema Mwanisongole.

Mtafiti kutoka Taasisi ya Kilimo Kituo cha Uyole jijini Mbeya, Daud Mbongo, alisema kutokana na kubainika kwa Minyoo hiyo ya mimea, watafiti na wataalam wa Kilimo kutoka Kituo cha Utafiti wa Kilimo cha Kibaha mkoani Pwani na Kituo cha Utafiti wa Kilimo cha Uyole mkoani Mbeya wameanza kutoa elimu kwa wakulima kuhusu namna ya kudhibiti na kukabiliana na athari za minyoo hiyo.

Alisema baada ya kubaini tatizo hilo wamekuja na suluhu ambapo wakulima walielekezwa namna ya kudhibiti hiyo minyoo ili isiendee kuwapo shambani.

Aliongeza kuwa wakulima ambao mashamba yao bado hayajavamiwa na minyoo hiyo walielekezwa namna ya kukabaliana nayo.

Baadhi ya wakulima wa ndizi kutoka katika Halmashauri za Rungwe, Kyela na Busokelo ambao walipatiwa elimu ya kudhibiti minyoo hiyo katika Kituo cha Ilenge wilayani Rungwe, wamekiri kuona dalili na athari za minyoo hiyo kwenye mashamba yao. Walisema licha ya kuona dalili na athari za minyoo hiyo kwenye migomba lakini hawakuelewa chanzo cha dalili hizo mpaka walipoanza kupewa elimu kuhusiana na minyoo hiyo.

# Ugonjwa wa kifafa cha mimba pasua kichwa

**Na Mwandishi Wetu,**
MBEYA

WANAWAKE watano wanapoteza maisha kila mwaka kutokana na ugonjwa wa kifafa cha mimba katika Hospitali ya Rufaa Kanda ya Mbeya katika kitengo cha wazazi kilichopo jijini Mbeya.

Kutokana na hali hiyo wanawake wameshauriwa kuhudhuria kliniki mara kwa mara kwa ajili ya kufuatilia maendeleo ya Mimba pamoja na kufuata masharti ya wataalamu ili kukabiliana na ugonjwa huo.


Akizungumza jana, daktari bingwa wa wanawake kutoka hospitali hiyo, Dk. John Francis, alisema ugonjwa wa kifafa cha mimba ni miongoni mwa magonjwa yanayosababisha vifo vya akina mama wajawazito.

Alisisitiza akina mama wajawazito kufuata masharti yanayotolewa na wataalam wa afya ili waweze kuepukana na magonjwa hayo ambayo yamechangia vifo.

Alitaja miongoni mwa dalili za kifafa cha mimba ni maumivu ya kichwa hasa kwenye kipandauso, uoni hafifu ,kuumwa tumbo la juu (Chembe ya Moyo), pamoja na kutapika mara kwa mara.

"Kabla kifafa cha mimba hakijampata mtu huanza kuumwa presha ya mimba ambayo inaweza kuathiri figo, ubongo na mishipa ya damu, pia hali hii inaweza ikasababisha mtu akavimba mwili mzima kwa hiyo asipotibiwa mapema anaweza kupata kifafa cha mimba,"alisema Dk. Francis.

Alisema ikiwa mama mjamzito ameona hali tofauti katika mwili wake ni vema akawahi mapema hospitalini ili aweze kufanyiwa uchunguzi na kupatiwa matibabu.





# Mkurugenzi Kunambi atangaza kutoa bure vyeti vya kuzaliwa

**Na Peter Mkwavila.**
DODOMA

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Godwin Kunambi, amesema watahakikisha watoto wote wenye umri chini ya miaka mitano, wanasajiliwa kwa ajili ya kupatiwa vyeti vya kuzaliwa bure.

Kunambi aliyasema hayo wakati akifungua mafunzo ya siku tatu kuhusu usajili na utoaji wa vyeti hivyo kwa maofisa watendaji wa kata, maofisa maendeleo ya jamii, maofisa afya watakaoshiriki kwenye utoaji wa nyaraka hiyo kwenye maeneo husika.

Akizungumza na wataalam hao Kunambi aliwataka wawajibike kikamilifu kwenye zoezi hilo na wafanikishe huduma hiyo kwa wananchi ili kila mtoto mwenye haki ya kupata cheti hicho apatiwe.

"Naishukuru sana Serikali Kuu na RITA (Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini) kwa kusogeza huduma hii huku chini kwa Wananchi, sisi kama Halmashauri tutaifanya kazi hii kwa ufanisi kwani jukumu letu kubwa ni kutoa huduma kwa wananchi" alisema Kunambi.

Kwa upande wake Mratibu wa zoezi hilo katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Aneth Mwambya, alisema mafunzo hayo ni ya siku tatu kuanzia Machi 11, hadi Machi 15, 2019 ambapo zoezi la usajili wa watoto na utoaji wa vyeti vya kuzaliwa litaanza katika ngazi ya kata.

"Tunatoa wito kwa kila mzazi mwenye mtoto mwenye umri wa chini ya miaka mitano wafike katika ofisi za kata na katika baadhi ya vituo vya kutolewa huduma za afya zinazotoa huduma ya mama na mtoto ili wasajiliwe kwa ajili ya kupatiwa vyeti hivi vya kuzaliwa" alisema mratibu huyo.

Alisema zoezi hilo litaanza kwa kampeni ya siku 12 kuanzia Machi 15, 2019, na baada ya muda huo huduma hiyo itaendelea kutolewa kama kawaida, na kwamba kila mzazi atatakiwa kuwasilisha nyaraka za awali zikiwemo Tangazo la kuzaliwa kwa mtoto au kadi ya kliniki kabla ya mtoto husika kusajiliwa na kupatiwa cheti.



Maofisa watendaji kutoka Idara ya Maendeleo, Jamii na Afya jiji la Dodoma, wakimsikiliza Mkurugenzi wa jiji wakati alipokuwa akitoa mafunzo kwa ajili ya utoaji wa vyeti vya watoto vitakavyotolewa na Wakala wa Usajiri, Ufirisi na Udhamini (RITA) jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wenye ulemavu wabuni mkakati kujikwamua

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

SHIRIKISHO la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu Nchini (Shivyawata) Mkoa wa Dodoma, limehimiza uundaji wa matawi ngazi ya vijiji na mitaa kwa ajili ya kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili.

Ushauri huo ulitolewa na Katibu wa Shivywawata mkoani hapa Jastane Ng'wamtalima alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema kuwa uanzishaji wa matawi hayo ni utekelezaji wa sheria namba 9 sura ya 3 ya mwaka 2010.

Katibu huyo alisema kuwa sheria hiyo inataka kila kijiji, mtaa, wilaya hadi mkoa kuunda kamati hizo za watu wenye ulemavu ili waweze kusaidiwa changamoto zinazowakabili.

Alisema kuwa kamati hizo za watu wenye ulemavu zitasaidia kutafuta ufumbuzi kuliko ilivyo sasa ambapo wanalazimika kutembea umbali mrefu kutafuta suluhisho la matatizo yao.

"Hata hivyo changamoto nyingi za watu wenye ulemavu ni kukosa uelewa wa elimu ya kutambua sehemu ya kupeleka kero zao, hii pia imechangia hata kukosa uelewa wa kuvitambua vyama vyao vya ulemavu kwenye maeneo wanayoishi kama ni msaada kwao endapo wakivianzisha vikundi hivyo" alisema.

Aidha alisema pia tatizo la kiuchumi limekuwa changamoto kubwa inayosababishwa na watu hao kushindwa kuchangamkia fursa zilizopo ikiwemo mkopo wa asilimia mbili unaotokana na mapato ya ndani katika halmashauri kwa ajili ya ukopeshaji wa vikundi vikiwamo vya watu wenye ulemavu.

Alisema kuwa kutokana na hali hiyo Shivywawata imehimiza uundaji wa vikundi vya ujarisimali na kuvisajili ngazi ya halmashauri, ili waweze kukopa mikopo na hatimaye kuondokana na utegemezi ambao ni changamoto kubwa kwa walio wengi.

Katibu huyo pia alisema kuwa kero nyingine ambayo imekuwa ikiwakabili watu wenye ulemavu katika ngazi za vijiji na mitaa ni baadhi ya viongozi waliopewa dhamana kushindwa kusimamia uundaji wa kamati ambazo zinaweza kuwatambua watu wenye ulemavu.

# Wananchi wamwagiwa sifa kwa kutoa ardhi bure

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA.

HALMASHAURI ya Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma, imewashukuru wananchi wa kijiji cha Mlowa Barabara, kwa kutoa ekari 164 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya Wilaya.

Hayo yalielezwa na Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo Athumani Masasi ,wakati alipokua akizungumza na Nipashe kuhusu ujenzi wa hospitali hizo.

Msasi aliwashukuru wananchi wa Kijiji hicho kwa kukubali kutoa eneo la ardhi yao ya ukubwa wa ekeari 164 ambalo litatumiwa na Serikali kwa ujenzi wa hospitali kubwa mbili kwa wilaya hiyo ambazo zitasaidia kuokoa afya za wananchi.

"Halmashauri yetu tunabahati kubwa, ilikuwa tuwe na hospitali moja ya Wilaya lakini baada ya Rais Dk.John Magufuli kuahirisha sherehe za maadhimsho ya sikukuu ya uhuru Disemba 9, 2018 alielekeza fedha hizo kujenga hospitali, tukapata bahati hiyo ya kupewa ijengwe kwetu"alisema .

Alisema awali Serikali ilitoa fedha za kujenga hospitali ya wilaya , halmashauri ikapendekeza ijengwe eneo la Chamwino Ikulu lakini baada ya kupewa fedha za uhuru wakapendekeza ijengwe Mlowa Barabarani .


Alisema ujenzi wa hospitali hizo mbili umeanza na halmashauri inategemea kujenga kwa kiwango kulingana na thamani ya fedha .

Mmoja wa wakazi wa kijiji hicho, Magreth Masimba, alisema akinamama wa vijiji jirani wanapata shida wakati wa kujifungu kutokana na kutokuwa na hospitali hivyo ujenzi wa huo utaokoa maisha yao.

"Tunayo zahanati ya kijijini hapa, lakini ikitokea mama anataka kujifungua na anahitaji upasuaji inabidi kupelekwa Mvumi au hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma, inahatarisha usalama wa maisha yetu na kuna wakati wengine wanapoteza maisha"alisema Masimba.

Kwa uapande wake, John Kisuka alisema kutokana na Kijiji kutoa eneo kubwa wanaiomba Serikali kuangalia uwezekano wa kujenga na chuo cha afya.

Kisuka alisema ujenzi wa hospitali hiyo utasaidia wananchi wanaoishi vijiji vya jirani na wanaotumia barabara kuu ya Dodoma Iringa.







Wavuvi wakirusha nanga baada ya kuwasili katika bahari ya Hindi eneo la Kivukoni Feri jijini Dar es Salaam juzi. Hivi karibuni kumekuwa na malalamiko kwa baadhi ya wavuvi kupigwa na kunyang'anywa nyavu zao na kusababisha kuwapo na uhaba wa samaki kwa baadhi ya maeneo nchini. **PICHA: HALIMA KAMBI**

# Watu watatu wadakwa kwa kughushi nyaraka za kusafiria

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

IDARA ya Uhamiaji Zanzibar inawashikilia Watanzania watatu kwa tuhuma za kutengeneza nyaraka mbalimbali za serikali na taasisi binafsi za ndani na nje ya nchi.

Watuhumiwa hao ni pamoja na Halima Mohmed Hassan mkazi wa Mfenesini, Miza Abdallah mkazi wa Kiembe Samaki na Eric Julius mkazi wa Fuoni.

Akizungumza na waandishi wa habari katika ofisi za idara hiyo Kilimani Mjini Zanzibar, Kamishna msaidizi wa idara hiyo, Kagimbo Hosea alisema watuhumiwa hao walikamatawa Machi 8, mwaka huu.

Alieleza kuwa watuhumiwa walikamatwa baada ya idara hiyo kushikilia hati ya kusafiria ya raia mmoja wa Comoro ambayo walitilia mashaka.

Alisema baada ya uchunguzi wa kina kufanyika ilibainika hati hiyo haikuwa halisi bali ni ya kughushi ambapo waliamua kuwasaka waliohusika na kuitengeneza.

Kamishna huyo alisema pamoja na hati hiyo bandia pia mtuhumiwa Eric alikutwa na hati mbalimbali ambazo anamiliki kinyume cha sheria.

Alizitaja baadhi ya nyaraka nyingine alizokutwa nazo mtuhumiwa huyo ni hati 11 za kusafiria za Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, fomu ya uhamiaji inayojazwa wakati wa kuondoka nchini, fomu za maombi ya viza, risiti za malipo ya serikali ambazo hazijajazwa, benki statement, fomu za maombi ya hati za masomo, vitambulisho vya Mzanzibar mkaazi, kadi za ATM na kadi za bima ya afya.

Aidha, Kamishna huyo alisema upelelezi bado unaendelea ili kubaini watuhumiwa wengine ambao wanahusika katika tukio hilo na ushahidi utakapokamilika watafikishwa mahakamani.

Aliwataka wananchi kushirikiana na idara hiyo kwa kutoa taarifa hususani za raia wa kigeni ambao wanaishi hapa nchini kinyume cha sheria .

# Wizara elimu bora kutimiza malengo yaliyowekwa

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, imesema itaendelea kuandaa na kutekeleza mpango wa elimu kwa ufanisi ili kutimiza malengo yaliyowekwa na Serikali chini ya uongozi wa Rais wa Zanzibar na Dk. Ali Mohammed Shein.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Simai Mohammed Said, aliyasema hayo wakati akizindua miradi mitatu ya elimu itakayoweza kuwasaidia wanafunzi kujua haki zao na kujitambua katika mustakabali wa maisha yao. Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha inatoa elimu bora kwa watoto na kuwa na taifa lililobobea katika elimu na kupata wataalamu bora zaidi.

Aliwataka wadau wote wa elimu wasichoke kuiunga mkono wizara hiyo katika kutekeleza miradi hiyo ili kuwasaidia watoto kujiepusha na vishawishi ambavyo havina umuhimu katika maisha yao.

Simai alitaja miradi hiyo alisema ni pamoja na mradi wa haki zetu, maisha yetu na kuwawezesha wanawake kujitambua ambayo itaweza kuwasaidia watoto wa Zanzibar.

Aidha, alisema miradi hiyo kwa kiasi kikubwa itaweza kuwasaidia watoto kuwajengea uwezo ili waweze kujielewa kujiamini na kufanya maamuzi sahihi na yenye muelekeo mzuri wa maisha yao.

Alieleza kuwa wizara itafarajika sana kuona kwamba watoto wanalelewa kwa kufuata misingi mizuri na imara kwa kujali na kuheshimu maadili, mila, silka na desturi ya kizanzibari.

Simai alisema watoto wanaishi katika dunia iliyojaa kila aina ya changamoto za maisha ikiwamo mmomong'onyoko wa maadili ambao umekuwa ukiharibu sana silka na tamaduni na kuharibu mfumo mzima wa maisha yao.

Alisema ni imani yake kwamba miradi hiyo itaendeshwa kwa ueledi mkubwa ili kuwasaidia wanafunzi kufanya maamuzi sahihi pale watakapoona kuna aina ya dalili ya kutaka kuwaharibia maisha yao.

Alipongeza Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Elimu, Sayansi na Utamaduni (Unesco), kwa maamuzi ya busara ya kuunga mkono utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kielimu Tanzania ikiwemo Zanzibar.

Kwa upande wake Naibu Katibu Mkuu Utawala wa Wizara hiyo, Abdalla Mzee Abdalla alisema, mmong'onyoko wa maadili ndiyo chanzo cha ongezeko la maambukizi ya Virus Vya Ukimwi (VVU), hivyo Unesco kuamua kuanzisha miradi hiyo itaweza kusaidia kurejesha maadili mema kwa watoto na kuweza kujitambua.

Naye mwakilishi wa Unesco, Mathias Herman, alisema shirika lao litaendelea kushirikiana na serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kusaidia sekta ya elimu na kuona watoto wanapata elimu bora.

## Kabaka amwaga sifa kwa Rais Shein

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT), Gaudensia Kabaka, amesema kuwa uongozi wa Rais wa Zanzibar, Dk Ali Muhamed Shein, umewajali wanawake kwa kuwapa nafasi mbalimbali za uongozi.

Akizungumza na wanawake wa Wilaya ya Kaskazini A, Unguja, alisema kuwa Dk Shein ni kiongozi bora na anawajali wanawake katika Serikali yake ambao wana uwezo mkubwa.

"Tumeshughudia hata nafasi za waziri wanawake nao hawajaachwa nyuma, wamepewa nafasi hiyo na wamekuwa wakifanya kazi vizuri,"alisema.

Aidha, Kabaka aliwataka wanachama, viongozi na watendaji wa CCM kudumisha umoja na mshikamano katika kusimamia maslahi ya chama hicho kwa kila ngazi ya kiutendaji na kiuongozi.

Alisema endapo wanachama hao watashirikiana kwa kila jambo na kufuata miongozo ya kikatiba na kikanuni iliyowekwa na CCM, hatua hiyo itasaidia kupunguza changamoto za kisiasa.

Alieleza kuwa ushirikiano ndio chimbuko la maendeleo ya taasisi yoyote hivyo wanachama wa mkoa huo wanatakiwa kudumisha tunu hiyo ili kuimarisha maendeleo ndani ya CCM.

Kabaka, alisema Serikali ya Zanzibar imetatua shida na kero za wananchi kwa kiwango kikubwa kupitia mambo mbali mbali yaliyotajwa katika muongozo wa ilani ya uchaguzi.

"Wana CCM tunatakiwa tutembee kifua mbele kwa kujivunia mambo mema yanayotekelezwa na Serikali yetu kwani Zanzibar inakuwa zaidi kimaendeleo,"alisema mwenyekiti huyo.

Naye Katibu Mkuu UWT Queen Mlozi, aliitaka jamii kulinda haki za msingi za watoto wa kike kwani wamekuwa wakikatishwa masomo yao bila sababu za msingi jambo ambalo ni hatari kwa maendeleo yao na jamii kwa ujumla.

Queen aliwataka wazazi na walezi kutofumbia macho ndoa za umri mdogo pamoja na mimba za utotoni kwani tabia hizo zisipothibitiwa zinakuwa vikwazo vya kuharibu maisha ya watoto wa kike.

# RATIBA

## CAPITAL TELEVISION

**Mon 11 March**
06:00 Al jazera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the spotlight rpt:
12:30 Drive it rpt
13:00 Series rpt : Grapes of justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:30 Usafiri wako rpt
15:00 Cookery rpt: Culinary Delight
15:30 Toyota world of wildlife rpt
16:00 CNN International
17:00 Eco@Africa rpt
17:30 Meza huru
19:00 The Décor rpt
19:30 Business edition
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 The Monday Agenda
21:30 Capital Prime News
22:00 Kipima Joto
00:00 Al Jazeera

**Tues 12 March**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 The Decor rpt
12:30 Mizengwe rpt
12:45 Aibu Yako
13:00 Series rpt: Grapes of justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:15 Local pgm rpt: Business Edition
15:00 Bundesliga kick off
15:30 Out and About rpt
16:00 Capchat rpt
17:00 Ripoti Maalum rpt
17:30 Meza huru
19:00 Innovation
19:30 Ripoti Maalum
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Ode To Joy
21:30 Capital Prime
22:00 Turning the Spotlight rpt
22:30 Iron Chef rpt
23:30 Al Jazeera

**Wed 13 March**
06:00 Al jazeera
08:00 CNN International News
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the Spotlight rpt
12:30 Culinary delight rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:30 Local Pgm: The Monday Agenda Rpt
15:15 Capchat rpt
16:15 CNN International
17:00 Innovation rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Sports Gazette
19:30 Business edition rpt
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Ode To Joy
21:30 Capital Prime News
22:00 Dakika 45:
22:45 The Décor
23:15 Al Jazeera

**Thurs 14 March**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Sports Gazette
12:30 Out n' about rpt:
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:30 Business Edition rpt
15:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
16:00 Dakika 45 rpt
17:00 In good shape
17:30 Meza Huru
19:00 Turning the spotlight
19;30 Usafiri wako
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Ode To Joy
21:30 Capital Prime News
22:00 Capchat rpt
23:00 Al Jazeera

**Frid 15 March**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Innovation rpt
12:30 The Decor rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:30 Ripoti Maalum rpt
15:00 Korean Dram rpt: Emperor of the sea
16:00 CNN International
16:30 The Monday Agenda rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Drive it
19:30 Eco@Africa
20:00 Aibu yako
20:15 Local Pgm: Business Edition
20:45 Series: Ode To Joy
21:30 Capital Prime News
22:00 Malumbano ya hoja rpt
00:00 Al Jazeera

**Sat 16 March**
08:00 CNN International
09:00 Drive It rpt
09:30 Turning the Spotlight rpt
10:00 Culinary delight rpt
10:30 Innovation rpt
11:00 Out n'about rpt
11:30 Sports Gazette rpt
12:00 Usafiri wako rpt
12:30 Eco@Africa rpt
13:00 Business edition rpt
13:30 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
14:30 Telenovela rpt: Ode To Joy
17:15 Ripoti Maaalum rpt
17:45 Bundesliga kick off
18:15 Capchat rpt
19:15 Mizengwe
19:30 The Decor
20:00 Iron Chef.
21:00 Out n' about
21:30 Movie: Grindstone road
23:00 Grapes of Justice rpt
01:00 Al Jazeera

**Sun 17 March**
08:00 CNN International
09:00 In good shape
10:00 Capchat rpt
11:00 Sports Gazette rpt
11:30 Iron chef rpt
12:00 Out n about rpt
12:30 Bundesligga Kick Off rpt
13:00 Ripoti Maalum
13:30 Series rpt: Grapes of Justice
15:15 Aibu yako
15:30 Drive it rpt
16:00 Dakika 45 rpt
16:45 Mizengwe rpt
17:00 The Decor rpt
17:30 Meza huru
19:00 Turning the Spotlight rpt
19:30 Cookery pgm:Culinary Delights
20:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
21:00 Shift
21:15 Capchat live
22:15 Telenovela: Ode To Joy
00:00 Al Jazeera

## ITV Daima WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY 11 March**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Hatua
10:55 Habari za saa
11:00 Kimya Milele
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jungu kuu rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Mjue Zaidi
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:10 Aibu yako rpt
18:15 Huduma ya kwanza
18:30 Kesho Leo
19:00 Afya ya Jamii
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Dakika 45
22:00 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**TUESDAY 12 March**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:15 Igizo: Mtego
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Afya ya jamii rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Uchumi na biashara
13:30 Kipindi Maalum rpt : TFDA
13:55 Habari za saa
14:00 Huduma ya kwanza
14:15 Telenovela: Destiny (Destino) rpt:
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Korean drama rpt: The Great Queen Seonduk
19:00 Jarida la wanawake
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Kipindi maalum: Ewura
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**WEDNESDAY 13 March**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Shamba shape up
10:55 Habari za saa
11:00 Korean: The Great Queen Seonduk
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jarida la wanawake rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Dakika 45
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino):
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi rpt
18:30 Ijue Sheria
19:00 Kipindi Maalum: TFDA
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Aibu Yako! Hata wewe?
21:10 Kipindi Maalum : Tanesco
21:40 Kesho Leo rpt
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**THURSDAY 14 March**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Elininyo
10:55 Habari za saa
11:00 Igizo: Elininyo
11:15 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al jazeera
12:30 Ijue Sheria
12:55 Habari za saa
13:00 Kipindi Maalum rpt: Ewura
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Igizo: Riziki
09:00 Usafiri wako
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Malumbano ya hoja
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**FRIDAY 15 March**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:20 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Kipindi Maalum rpt: Tanesco
12:55 Habari za saa
13:00 Mjue Zaidi rpt
13:45 Kesho leo rpt
13:55 Habari za saa
14:00 Kesho leo rpt
14:15 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
17:30 Ibada ya kiislamu
18:00 Jiji Letu
18:15 Igizo: Mizengwe
18:30 Shamba shape up
19:00 Uchumi na biashara
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Kipima joto
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**SATURDAY 16 March**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al Jazeera
09:00 Watoto wetu
10:00 Mjue Zaidi rpt
11:00 Jungu kuu rpt
11:30 Usafiri wako
12:00 Shamba Shape up
12:30 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:45 Igizo rpt: Riziki
15:15 Igizo rpt: Elininyo
15:45 Igizo rpt: Mizengwe
16:00 Igizo rpt: Kimya Milele
16:30 Igizo: Mtego rpt
17:00 Shamsham za Pwani
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Igizo: Riziki
19:00 Sanaa na wasanii
19:30 Jungu Kuu
20:00 Habari
21:00 Igizo: Kimya Milele
21:30 Hawavumi lakini wamo
22:30 Isidingo rpt
01:00 CNN International

**SUNDAY 17 March**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al jazeera
09:00 Watoto Wetu
10:00 Tafrija ya chakula cha mchana kwa watu wenye ulemavu
16:00 Korean drama: The great queen Seonduk
16:45 Mjue zaidi
17:30 Kipindi cha kikristo
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Mizengwe rpt
18:45 Matukio ya wiki
19:30 Igizo: Mtego
20:00 Habari
21:05 Mizengwe
21:00 Bongo Movie: Hard Price 2
22:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)


EATV




LEO USIKU SAA 3:00



IJUMAA
10:59 Jikoni Na Jane
11:00 DADAZ (live)
13:30 Kali Za Wana
14:00 Radio:PlanetBongo Live
15:00 FUNGUKA
16:30 #HASHTAG
17:00 5SELEKT
17:55 Kurasa
18:00 eNewz
18:30 Skonga
19:00 EATV SAA 1
19:30 MJADALA
21:00 Friday Night Live

FRIDAY NIGHT LIVE (FNL) ni mlipuko wa burudani unaounganisha EATV na East Africa Radio kukuletea Muziki mnene, burudani ya kupagawisha na mahojiano na wageni wanaoalikwa kutoka ndani na nje ya nchi.

eastafrica RADIO
05:00 EA Breakfast
09:00 Supamix
12:00 Kipenga Xtra
13:00 Planet Bongo
16:00 EA Drive
20:00 Kipenga
21:00 The Cruise

88.1FM DAR ES SALAAM


## RADIO One WEEKLY-SCHEDULE

| TIME | MONDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | RADIO ONE DOCTOR |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DAKIKA 45 |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 -03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | DK 45 ( MARUDIO ) |
| 23.00 HRS | |

| TIME | TUESDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA SHERIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 - 03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

| TIME | WEDNESDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA MICHEZO |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

| TIME | THURSDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA UKIMWI |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | MALUMBANO YA HOJA |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

| TIME | FRIDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | HIZI NAZO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18:30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.0O HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05HRS | KIPIMA JOTO |
| 23.00 HRS | WEEKEND SHOW |
| 01:00 - 03:00HRS | HIZI NAZO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

| TIME | SATURDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA KISWAHILI |
| 09.00 AM | WATOTO SHOW |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | MIWANI YA MAISHA |
| 11:00 AM | MTAA WA MAGOMA |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | CHAGUO LAKO |
| 15:00 HRS | MUZIKI NA MICHEZO |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.15 HRS | MIDUNDO MOTOMOTO |
| 18:00 HRS | BONGO TEN |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.15 HRS | CHEMSHA BONGO |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | WEEK END SHOW I |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | WEEK END SHOW II |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | WEEK END SHOW III |
| 01:00-03:00HRS | KISWAHILI ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | MUZIKI & MICHEZO ( MARUDIO ) |

| TIME | SUNDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA - FAMILIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | SUNDAY SPECIAL |
| 11: 00 HRS | TOP 20 |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13.30 HRS | NANI ZAIDI |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | MAMBO YA PWANI |
| 18:00 HRS | AFRICAN PANORAMA |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20:10 HRS | MBAVU ZANGU |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | MAMBO MSETO |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | RAFIKI I |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | RAFIKI II |
| 01:00 - 03:00 | FAMILIA ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00 HRS | RED CARPET ( MARUDIO ) |

## CAPITAL RADIO

### CAPITAL RADIO 2017 101.3 FM
### FAHARI YA MSIKILIZAJI/THE LISTENERS PRIDE

**MONDAY**
05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-20:00HRS BOZOUK TIME
20:00-21:00HRS HALI HALISI
21:00-22:00HRS SPORTS
22:00-01:00HRS LADHA LAINI

**TUESDAY - FRIDAY**
05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-21:00HRS BOZOUK TIME
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI
01:00-05:00HRS MUSIC & JINGLES

**SATURDAY**
05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS DK 90 DUNIANI
09:00-10:00HRS MUZIKI
10:00-12:00HRS KADOGOO
12:00-13:00HRS BONGO HITS 1
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS BONGO HITS 2
15:00-16:00HRS ZAIDI YA UMJUAVYO
16:00-18:00HRS THE SPLASH
18:00-21:00HRS LAID BACK
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS AK 47 LIVE
01:00-05:00HRS MUSIC

**SUNDAY**
05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS GOSPEL MUSIC
09:00-11:00HRS THE SUNDAY
11:00-13:00HRS TOP TWENTY
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS CAPITAL MICHEZONI
15:00-16:00HRS UKURASA WA MBELE
16:00-18:00HRS UNLIMITED REQUEST
18:00-21:00HRS JIACHIE
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI

# Trump asitisha safari za Boeing Marekani

**WASHINGTON,** Marekani

SIKU moja baada ya Mamlaka ya kuratibu safari za Ndege za Marekani (FAA) kusema haitasimamisha safari za ndege aina ya Boeing 723 Max, Rais Donald Trump ameibuka na kutangaza kusitisha usafiri wa ndege hizo.

Juzi, FAA ilisema haitasimamisha safari za ndege aina ya Boeing 737 Max, baada ya kutokea kwa ajali ya Ndege ya Ethiopian Airlines, ambayo iliua watu 157.

Kaimu ofisa mkuu wa mamlaka hiyo, Dan Elwell, alisema kwamba uchunguzi uliofanywa hadi kufikia juzi haujabaini hitilafu yoyote na mfumo wa ndege hizo, hivyo haoni haja ya kusitisha safari zake.

Jana, Rais Trump alitangaza amri ya dharura ya kusitisha usafiri wa ndege zote muundo wa Boeing 737 Max8 na Max 9 kwenye anga ya Marekani.

Rais Trump alisema ndege hizo hazitafanya safari zake nchini Marekani hadi pale uchunguzi utakapokamilika kubaini iwapo hitilafu ya kimitambo ilisababisha ajali mbili za Ndege aina ya Max 8, katika kipindi cha miezi mitano, na kusababisha vifo vya mamia ya watu.

**Rais Trump alizitaka ndege zote za muundo wa Max 8 na Max 9 ambazo zilikuwa angani wakati wa tangazo hilo, ziegeshwe punde tu zitakapotua.**

Muda mfupi baada ya Trump kutangaza hatua hiyo, maafisa wakuu wa kampuni ya Boeing inayotengeneza Ndege hizo, walitoa taarifa kupitia mtandao wa kijamii wa Twitter na kusema kuwa kampuni hiyo inaunga mkono kauli ya Rais huyo na kuongeza kwamba ni heri kuwa salama kuliko kujuta baadaye.

Marekani imejiunga na nchi 30 ambazo tayari zimetangaza kusitishwa kwa safari za ndege hizo huku uchunguzi wa mfumo wake wa kompyuta, ambao unashukiwa kusababisha ajali ya ndege hiyo Oktoba mwaka jana nchini Indonesia, na ile ya ndege ya shirika la Ethiopian Airlines, Jumapili iliyopita.

Rais Trump alizitaka ndege zote za muundo wa Max 8 na Max 9 ambazo zilikuwa angani wakati wa tangazo hilo, ziegeshwe punde tu zitakapotua.

Licha ya FAA na mashirika ya ndege ya Marekani kukaa kimya kufuatia shinikizo za kutaka ndege hizo zisitishe safari zake, wachambuzi wa masuala ya teknolojia ya ndege wanasema kuna uwezekano mkubwa wa hitilafu za kiuhandisi hasa kwenye mfumo wa kompyuta kwa ndege hizo za 737 Max.

Hadi kufika siku ya Jumapili ambapo ajali ya Ethiopian Airlines ilitokea, Shirika la Boeing lilikuwa limeuza ndege 400 ulimwenguni kote.

Wachambuzi wanasema kuwa hili ni pigo kubwa kibiashara kwa kampuni ya Boeing na mashirika mbalimbali ya ndege ulimwenguni kote. **VOA**



Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta, akiwa na Rais wa Ufaransa Emmanuel Macron pamoja na wajumbe wengine kwenye mkutano wa kimataifa kuhusu mazingira uliofanyika mjini Nairobi. **PICHA: DW**

# Jengo laporomoka Lagos, 11 wafariki

**LAGOS,** Nigeria

WATU 11 wamefariki na wengine 50 kujeruhiwa eneo la Ita-Faaji nchini Nigeria baada ya jengo kuanguka.

Tukio hilo limetokea juzi, ambapo wafanyakazi wa huduma za dharura mjini Lagos bado wanaendelea na kazi ya kuokoa maisha ya watu kutoka kwenye kifusi cha jengo hilo.

Jeshi la Polisi nchini humo lilieleza kuwa kikosi cha kuokoa bado kinaendelea na zoezi na kwamba chanzo cha kuanguka kwa jengo hilo bado hakijafahamika.

Serikali jijini Lagos ilieleza kuwa uchunguzi utafanyika baada ya operesheni ya ukoaji kukamilika na kuhitimisha kuwa wale wote waliohusika watashitakiwa.

"Ni vigumu kufahamu idadi kamili ya watu waliokuwa ndani ya jengo, kwa sababu jengo lililokuwa likitumika kwa matumizi mbalimbali ikiwamo shule iliyokuwa na wanafunzi 100, ghorofa ya katikati, kulikua na makazi ya watu wakiishi na familia zao na chini ya jengo kulikua na maduka ambayo wafanyabiashara walikua wakifanya biashara zao," ilieleza taarifa kutoka serikalini.

Taarifa zaidi zinaezeleza kuwa mbali na ghorofa lililoanguka, nyumba nyingine zilizokua na dosari kwenye eneo hilo, zilizowekwa alama kwa ajili ya kubomolewa zilipakwa rangi upya kufuta alama zilizowekwa na mamlaka.

Matumizi ya vifaa vya ujenzi visivyo na ubora ni kawaida nchini Nigeria na serikali haichukui hatua madhubuti kuhakikisha taratibu zinafuatwa.

Wakati huohuo, ndugu wa waliookolewa wamekua wakitembelea kwa wingi hospitali ambapo watu waliojeruhiwa wamefikishwa.

Baadhi ya majeruhi wamepata nafuu na kuruhusiwa kuonana na familia zao huku wengine wakilia kwa sababu hawafahamu walipo watoto wao wa shule. **BBC**

## Ethiopia yapeleka visanduku ndege kuchunguzwa

**ADDIS ABABA,** Ethiopia

SHIRIKA la ndege la Ethiopia, limesema kwamba limevisafirisha kwenda Ufaransa visanduku vya kurekodi kumbukumbu ya mawasiliano ya ndege au (black box) vya ndege ya Boeing 737 Max 8 iliyoanguka na kuwauwa watu 157, kwa ajili ya uchunguzi.

Taarifa iliyoandikwa katika mtandao wa kijamii wa Twitter, shirika hilo limesema ujumbe wa Ethiopia ukiongozwa na kitengo cha uchunguzi wa ajali AIB kimevipeleka visanduku hivyo huko Ufaransa.

Ethiopia imesema kuwa haina vifaa vya kusoma data zilizorekodiwa katika visanduku hivyo, na Ujerumani imesema haitavifanyia uchunguzi visanduku hivyo kwa kuwa haiwezi kusoma mfumo wa kompyuta uliotumiwa na shirika la Boeing.

Mkuu wa Shirika la Mamlaka ya Anga la Marekani, FAA, Daniel Elwell alisema kuwa visanduku hivyo vya kurekodia data viliharibiwa katika ajali hiyo.

Wakati huohuo, hali ya ukimya wa dakika moja ulifanyika nchini Kenya katika mkutano wa kilele wa Umoja wa Mataifa wa One Planet ambao Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron anahudhuria, kuwakumbuka waliofariki katika ajali hiyo. **DW**

## Bunge la EU lakataa Uturuki kujiunga na Umoja huo

**LONDON,** Uingereza

WABUNGE katika bunge la Ulaya, walipiga kura kwa wingi kulikataa ombi la taifa la Uturuki kutaka kujiunga na Umoja wa Ulaya (EU).

Wabunge hao wanadai kuwa Rais wa Uturuki, Tayyib Erdogan, amekuwa akijihusisha na vitendo vya ukiukaji wa haki za binadamu jambo ambalo ni kinyume cha maadili ya umoja huo.

Wabunge 370 walipiga kura kupinga ombi hilo la Uturuki dhidi ya wabunge 109 waliopiga kura kutaka Uturuki ikubaliwe kujiunga na EU, huku wabuge 143 wakikosa kupiga kura. EU umesema kwamba Uturuki haiwezi kujiunga na jumuiya hiyo kwa sababu ya kuhujumu uhuru wa watu kuzungumza, wapinzani kuwekwa viuzuizini na ukiukaji wa haki za kimsingi za raia.

Mbunge wa siasa za wastani za mrengo wa kulia kutoka Uholanzi, Kati Pir ambaye aliunga mkono kutoruhusiwa kwa uturuki kujiunga na EU alidai kuwa Rais Erdogan amekuwa akitumia mabavu katika uongozi wake kwa kuwakamata wapinzani, pamoja na kuporomoka kwa uhuru wa mahakama.

Msemaji wa chama kinachotawala nchini Uturuki AK, Omar Celik, amepuuza mbali matokeo ya kura hiyo kwa kusema hayana maana yoyote na ni batili. **DW**

# Waziri ang'aka kasi utendaji Bandari

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, ameelezea kutoridhishwa na kasi ya shughuli za bandari kutoka kwa taasisi tatu hali ambayo inachangia ucheleweshaji wa mizigo ya ndani na nje ya nchi.

Taasisi hizo ni Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TPA) na Shirika la Reli Tanzania (TRC).

Kamwele aliyasema hayo jijini Dar es Salaam jana wakati wa utiaji saini makubaliano ya ushirikiano kati ya TRC na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) kwa ajili ya ukarabati wa mabehewa 40 ambayo yatagharimu Dola za Marekani 600,000 (Sh. bilion 1.13)

"Tangu nimeingia sifurahishwi na kasi ya bandari kwa sababu ya hizo taasisi tatu TRA, TPA na TRC, hawa wawili TPA na TRC ni wa kwangu ndiyo maana juzi Rais John Magufuli aliniambia niliingilie kati. Nashukuru tulishirikiana tukaondoa hilo suala la kontena baada ya kufika bandarini lifunguliwe na mizigo kuondolewa ili kontena lirudi na meli badala ya mfanyabiashara kutakiwa kutoa Dola za Marekani 2,000 kama dhamani katika meli," alisema.

"Kazi ya paka ni kukamata panya sasa unapokuwa na paka halafu hakamati panya maana yake ni nini? Kwa bahati nzuri juzi nimemwandikia barua Waziri wa Fedha na Mipango tufanye kikao cha pamoja ili kutatua changamoto tulizo nazo," aliongeza.

Kamwelwe alisema ni kweli kuna sheria ambazo zinaonekana kama hazifanyi kazi, hivyo ni lazima waziangalie kama zinawasaidia na kama wanaona zinawakwamisha wawajulishe ili wazifanyie kazi.

Alisema amejaribu kuchunguza akagundua kwamba kuna mambo mengi ambayo yasipofanyiwa kazi yatasumbua likiwamo suala la kiutawala linalokwamisha mizigo bila sababu za msingi.

Waziri alisema tani zinazopokelewa bandarini kutokana na ukwamishaji wa taasisi hizo tatu ni chache, hivyo atakwenda kulishughulikia suala hilo na kwamba lengo la serikali ni kuona mapato yanaongezeka kupitia mizigo.

Aidha, alisema msaada walioupatiwa na WFP utaongeza uwezo wa shirika katika kuhudumia mzigo hususani unaopita bandari ya Dar es Salaam kwenda nchi jirani za Uganda, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), Zambia, Rwanda na Burundi.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa TRC, Masanja Kadogosa, alisema mabehewa ambayo yanahitajika kufanyiwa ukarabati mkubwa ni 500 na kati ya hayo, 200 yanagharamiwa na serikali.

Alisema mahitaji ya shirika ni zaidi ya mabehewa 800 na kwa sasa wana mabehewa 328, hivyo bado wana uhitaji wa behewa ili kuongeza kasi ya utendaji wao wa kazi.

Kadogosa alisema lengo la ukarabati wa mabehewa ni kuongeza ufanisi wenye tija katika usafirishaji wa mizigo kati ya Tanzania na nchi jirani kwa kutumia reli ya kati.

Mwakilishi Mkazi wa WFP, Michael Dunford, alisema msaada huo umelenga uboreshaji wa usafiri katika sekta hiyo na kwa mwaka huu watakuwa na mzigo wa chakula chenye tani 120,000 hadi 160,000 ambazo zitasafirishwa na TRC.




Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, akipiga makofi na baadhi ya wadau wa Afya mara baada ya kuzindua Jukwaa la "SITETELEKI" litakalozungumzia maswala ya Afya hususani vijana chini ya mika 25 ili waweze kujitambua na kuwa na tabia chanya.Uzinduzi huo ulifanyika jana Mkoani Tabora. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Mwandishi aachiwa kwa dhamana

INATOKA UK.4

cha polisi kwa kutoa taarifa za uchochezi.

"Nilipelekwa moja kwa moja polisi saa 11:00 jioni na nilipofika nikawekwa ndani na nikalala hadi leo (jana) hii ninavyoachiwa kwa dhamana na maelezo waliyochukua ya tukio la mimi kufuatilia taarifa ya maji machafu na sijahojiwa kitu kingine chochote na sijafanya kitu chochote," alisema.

Mapema jana asubuhi, waandishi wa habari walikusanyika ofisi za Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha kumsubiri ili kufahamu hatima ya mwenzao. Walipofika walipata taarifa Kamanda yuko kwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha ana kikao na ndipo walipoamua kumfuata huko.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusiana na sakata hilo katika kikao ofisini kwake, Mkuu wa Mkoa Arusha, Mrisho Gambo, alisema kushikiliwa kwa mwanahabari huyo kumetokana na makosa mengine na si suala la kufuatalia maji machafu yanayodaiwa na watu.

"Lakini msifikiri kuja kwenu kwa wingi hapa mnatutisha sisi serikali tusifanye kazi zetu hapa. Nilimwagiza RPC amwachie kwa dhamana jana (juzi), japo ana makosa mengine aliyofanya na si lazima tuwaeleze nyie mtaharibu upelelezi," alisema.

Mwenyekiti wa Chama cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Arusha, Claud Gwandu, alilaani kukamatwa kwa mwandishi huyo na kumwomba Mkuu wa Mkoa kama kuna tatizo washirikishane kabla ya kuchukua uamuzi wa kukamatana sehemu ya kazi.

"Tena kibaya mkuu tulipofuatilia jana kwa RPC alituambia amepokea maagizo toka juu yaani kwako wewe. Sasa hii inakuwaje?" alihoji.

Alisema chama hakitetei uovu lakini kukamata watu wakiwa kazini ni sawa na kutisha waandishi wasifanye kazi zao kwa misingi ya sheria na kuwataka waandishi kutoogopa bali waendelee kufanya kazi zao kwa kuzingatia sheria za kazi.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Arusha, Jonathan Shana, akizungumza katika kikao hicho, aliwaambia waandishi wa habari kuwa ameshatoa maelekezo ya kuachiwa kwa dhamana mwandishi huyo.

"Kweli Mkuu wa Mkoa jana uliniambia tumwachie kwa dhamana lakini tulikuwa bado hatujamalizana naye mahojiano na leo (jana) hii nimeshaagiza apewe dhamana," alisema.

Zaidi ya wiki moja sasa baadhi ya maeneo ya Arusha kumekuwa na malalamiko ya wananchi kuhara, kuugua matumbo na kutapika kwa madai ya kunywa maji ya Auwsa ambayo yameingiliana na maji taka, madai ambayo Auwsa wanayakanusha kuwa maji hayo ni safi na salama.

# Waziri wa Kilimo atishia kuifuta NFRA

INATOKA UK. 4

unaendana na mpango wa serikali wa kufikia maendeleo endelevu ya dunia.

"Serikali ya awamu ya tano inathamini na kupongeza WFP kwenye masuala ya chakula na lishe, lishe bado ipo chini, tuwahimize watu kula, cha kushangaza wanaoumwa ni wakulima wanaozalisha," alisema.

Alisema mamlaka husika zinapaswa kuwapa elimu wakulima kuhakikisha wanakula vizuri.

Hasunga alisema mashine hiyo ina thamani ya Sh. milioni 399.8 na itakuwa na uwezo wa kusafisha tani 100 za mahindi kwa siku.

"Nashukuru WFP kwa mashine hii, lakini naomba muangalie uwezekano wa kutusaidia pia kwenye kanda zetu zingine,"alisema.

Awali, Kaimu Mtendaji wa NFRA, Vumilia Zikankuba, alisema wamekuwa wakishirikiana kwa muda mrefu na WFP na mikakati wanayoifanya imesaidia serikali.

"Miongoni mwa mikakati ni kuboresha miundombinu ya kuhifadhi kwa kutumia teknolojia yenye uhifadhi kwa kuwa kila siku teknolojia inabadilika," alisema.

Alisema uuzaji wa tani 36,000 kwa WFP unaendelea na mpaka jana, walikuwa wamechukua tani 20,400.

"Tupo tayari kuwauzia kadri watakavyohitaji na yatakuwa na ubora unaotakiwa, tunakuhakikishia waziri, hatutakuangusha katika soko lolote la kimataifa, tutaendelea kuwauzia mazao yenye ubora," alisema.

Mwakilishi wa WFP Tanzania, Michael Dunford, alisema WFP inaangalia namna ya kumtoa mkulima katika kilimo kidogo na kuwa na kilimo kikubwa.

Alisema Dola za Marekani milioni 330 zimeingizwa nchini Tanzania na tangu mwaka 2010 kununua tani 500,000 za chakula, Kati yake, tani 200,000 zimetoka NFRA.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### NAFASI ZA KAZI


**WAFANYAKAZI WA HOTELINI**, Wanatakiwa wafanyakazi wa Usafi, Wahudumu, Wapishi na Meneja. Bagamoyo mjini, wawe na vyeti na uwezo wa kuongea Kingereza. Kwa Mawasiliano piga namba: 023-2440004/0657 233970/0768 296667

**MIRADI ITAKUPATIA PESA NA AJIRA:** Learn DESIGNING project proposals ,Find DONORS, Establish NGO .1784505108 / 0769505108 / 0716581562.


Uza,
Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza
Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0767 223 311

NIPASHE NI JIBU LAKO
NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA


### KUPOTEA KWA CHETI




**Claudian Tembe** anatangaza kupotea kwa chati cha kidato cha sita chenye index namba **S0153-0595** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la taifa mwaka 2015, Katika shule ya Sekondari Songea Boys.

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Polisi Taarifa: SO/RB/506/019**

215118002

### CHETI KIMEPOTEA




**MOHAMEDI MWAMSEMA KOMBO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.2745/0045 kilichotolewa na shule ya sekondari MTIMBWANI mwaka 2015.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOM/B.I/21/VOL.IX/616**

115117602

### CHETI KIMEPOTEA



**MARIETHA J. ROMWALD** anatangaza kupotelewa na cheti cha ACADEMIC CERTIFICATE chenye index no. **S0242-0033** kilichotolewa na shule ya **ST.MARGARET GIRLS SECONDARY SCHOOL** mwaka 2013.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **MOS/NB/10720/15.**

115117402

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 232233
Barua Pepe ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,
13/03/2019

### TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya JUMAMOSI tarehe 16/03/2019 kampuni ya **MEERO** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **MATEVES** kuelekea **MOROMBO** gari hilo lenye namba za usajili: **T747ASM/T/63DLR.**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita 4.8** |
| **Upana** | - | **mita 3.0** |
| **Kimo** | - | **mita 17** |

3. Njia itakayotumika **MATEVES** hadi **MOROMBO kupitia EAST AFRICA** gari litasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

115117802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO
Usimamizi wa mirathi **No;79/2019**

Ombi la **HILDA ENOCK/DANIEL ROBSON** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **BARAMU ROBSON BONA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe **25/03/2019** kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 14/03/2019.

115116702

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**GODLISTEN WILLIAM LYIMO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 132 ASM SUZUKI** ESCUDO. Chassis namba **TD01W136390.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KJN/RB/1520/2019.**

215116602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO
Usimamizi wa mirathi No;73/2019
Ombi la **PATRICK DANIEL WALUYE** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **KISA PETRO WALUYE**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 28/03/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa
Tarehe 13/03/2019.

115116802

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ALLY HUSSEIN NINGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 905 CBT** AINA YA SCANIA. Chassis namba **4466964**. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KJN/RB/1521/2019.**

115117202

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO
Usimamizi wa mirathi No;56/2019

Ombi la **AMINA IDD KITAMBI** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **IDD ABDALLAH KITAMBI**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 18/03/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

Tarehe 05/03/2019.

115116902

### KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**PHILIMINUS M. NJOJOLI** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **T 393 BCB** AINA YA T BETTER. Chassis namba **LZEPCKLB994801077.** Engine namba **ZJ16ZFMJA94510923.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **KW/RB/B/1/X193.**

115117102

### CHETI KIMEPOTEA



**GRACE L. RUTAHAKANA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.221/67** kilichotolewa na WERUWERU SEKONDARI mwaka 1980. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **OB/RB/2481/2019.**

115115702


JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?
Nipashe

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*
*Tupigie 0767 223 311*

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# NI VITA YA RONALDO NA LIONEL MESSI?



**TURIN,** Italia

BAADA ya Cristiano Ronaldo kufunga 'hat-trick' na kuchangia ushindi wa Juventus dhidi ya Atletico Madrid na kufuzu kwa robo fainali katika ligi kuu ya mbingwa, hasimu wake wa jadi Lionel Messi amefuata mkondo kwa mchango mkubwa ulioipa ushindi Barcelona dhidi ya Lyon kwa mabao 5-1.

Ukitathmini, Messi alifanikiwa pia kumpiku Ronaldo kwa kutoa mabao manne: mawili aliyoyafunga mwenyewe, na mengine mawili aliyotoa pasi safi kwa Gerard Pique na Ousmane Dembele.

Ushindi huo unairuhusu Barca kuendelea kuipeperusha bendera ya La Liga kama wawakilishi wa pekee wa Hispania katika timu nane za mwisho pamoja na kumpa fursa zaidi Messi kutimiza ahadi yake aliyotoa katika hotuba kwa mashabiki kabla ya msimu kuanza kulileta taji la Ulaya kwa mara ya kwanza tangu kushuhudiwa 2015.

Na kwa kweli, inaendeleza pia uhasimu mkubwa katika historia ya soka kuwahi kushuhudiwa.

Suala la kiasi gani wachezaji hawa wawili wanavyohamasishana ni la kuvutia sana, na ni rahisi mtu kumfikiria Messi akiwa amekaa nyumbani Jumanne usiku akimtazama Ronaldo akiiangamiza Atletico kwa mabao, akitazama televisheni kwa hasira na kukasirika huku pengine akisema: "Nitamuonyesha!"

Licha ya kwamba ni picha ya kuvutia kuifikiria, hata hivyo huenda sio ukweli angalau kwa mtazamo wa Messi.

Huenda atalionyesha katika namna tofauti, lakini Messi ana umahiri kama alivyo nao Ronaldo.

Kando na magoli na ushindi binafsi, lakini ukaribu wa mchezaji huyo wa Argentina ni mataji.

Ronaldo, tunaweza kusema, haonekani kuwa na furaha akiwa uwanjani, hadi iwapo amefunga goli na hata hapo furaha hiyo haidumu kwa muda mrefu, kwa sababu anataka kufunga bao lingine tena.

Na ukaribu huo wa kufunga mabao imekuwa na mchango mkubwa katika ufanisi wake kwenye kucheza soka ya kulipwa.

# *Messi amwagia sifa Ronaldo kuibeba Juventus*

**BARCELONA,** Hispania

NAHODHA wa klabu ya Barcelona, Lionel Messi amemwagia sifa hasimu wake, Cristiano Ronaldo kwa kutupia magoli matatu katika mchezo kati ya Juventus dhidi ya Atletico Madrid.

Messi amesema katika mchezo huo wa hatua ya 16 bora ambao Juventus ilishinda magoli 3-0, hakuamini kama Juventus wangefuzu na kudai kuwa ulikuwa usiku wa maajabu kwa Ronaldo, ambaye ndiye alifunga mabao yote.

"Cristiano na Juventus walikuwa vizuri sana (kwenye mchezo wa marudiano kati Juventus vs Atletico).

"Nilishangazwa na matokeo, kwani niliamini Atletico wangekuwa wagumu lakini Juventus walifanikiwa kuwazidi na Ronaldo akaonyesha maajabu yake kwa zile goli tatu," ameeleza Messi wakati akijibu maswali ya waandishi wa habari mara baada ya mchezo wa Barcelona dhidi ya Lyon.

Katika mchezo huo Messi alitupia magoli 2 kwenye ushindi wa mabao 5-1 walizowafungwa Lyon na kuifanya Barca kutinga hatua ya robo fainali ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.




# Silva asaini mkataba

**MANCHESTER,** England

MCHEZAJI Bernardo Silva, amesaini mkataba mpya wa miaka mitatu na klabu yake ya Manchester City ambao utamfanya adumu kwenye kikosi cha timu hiyo hadi mwaka 2025.

Nyota huyo anayecheza pia katika Timu ya Taifa ya Ureno amekuwa mchezaji wa 11 wa mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu England kusaini mkataba mpya tangu Januari mwaka jana walipoanza mchakato huo.

Inaaminika kuwa mkataba wake huo mpya utamfanya nyota huyo alipwe mshahara wa pauni 150,000 kwa wiki, akiwa katika msimu wake wa pili hapo Etihad Stadium, huku Real Madrid ikitajwa kuanza kumwinda mchezaji huyo.

Silva amekuwa katika kiwango bora na kumfanya awe mchezaji muhimu katika kikosi cha Pep Guardiola, akifuatiwa na Raheem Sterling, Aymeric Laporte na Ederson kusaini mkataba mrefu.

Mreno huyo mwenye umri wa miaka 24 amekuwa mchezaji maarufu katika klabu hiyo na jina la utani analoitwa ni Pablo Picasso ambalo amepewa na Benjamin Mendy.



HABARI MICHEZO

# Alderweireld akaribia kusajiliwa United

**LONDON,** England

KLABU ya Tottenham, imejiadaa kuanza maisha mapya bila ya beki wake nyota, Toby Alderweireld, katika kipindi cha majira ya joto.

Mkataba mpya aliosaini Desemba mwaka jana unaonyesha kuwa beki huyo wa kati, Alderweireld na Spurs atamaliza muda wa kuitumikia klabu hiyo mwishoni mwa msimu ujao.

Kutokana na mkataba huo kumbana nyota huyo, Spurs italazimika kukubali ofa ya pauni milioni 26 au zaidi kwa ajili ya kumuuza Alderweireld ndani ya wiki mbili za mwisho katika kipindi cha majira ya joto wakati dirisha dogo la usajili litakapofunguliwa.

Gazeti la The Mirror linaandika kuwa, Manchester United ndio inaongoza katika mbio za kuwania saini ya beki huyo mwenye umri wa miaka 30, ingawa pia Barcelona na Juventus nazo zinatajwa kumhitaji.

The Mirror limeendelea kuandika kuwa Spurs tayari imekubali kumpoteza Alderweireld kwa mahasimu wao wa mji mmoja.

Tangu alipojiunga na Spurs mwaka 2015, Alderweireld amecheza mechi za Ligi Kuu England zaidi ya 100 na amefunga mabao matano.

Alderweireld ambaye alihusishwa kuhama katika kipindi cha majira ya joto mwaka jana, lakini hakuondoka, amepangwa katika kikosi cha kwanza katika mechi nyingi za Ligi Kuu England kuliko katika misimu mingine iliyopita huko nyuma.

Kutua kwake Old Trafford, kutafungua milango ya kwaheri ya beki, Eric Bailly kuondoka klabuni hapo.






# KLOPP APAGAWA LIVERPOOL KUSONGA MBELE

**LIVERPOOL,** England

BAADA ya kupata ushindi wa mabao 3-1 mbele ya wenyeji Bayern Munich, Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp amekisifia kikosi chake kwa kazi kubwa waliyofanya hadi kutinga hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Klopp anaamini kuwa ulikuwa usiku bora kwa upande wake na wapo tayari kwa anayekuja mbele yao. Mabao mawili yaliyofungwa na Sadio Mane na moja likifungwa na Virgil van Dijk yalitosha kuihakikishia Liverpool nafasi ya kutinga hatua hiyo ya robo fainali na kujumuika na klabu nyingine za England ambazo ni Tottenham Hotspurs, Manchester United na Manchester City.

Hii ni mara ya kwanza kwa timu zote hizi nne za taifa hilo kutinga kwenye hatua hiyo tangu msimu wa mwaka 2008/9.

"'Kwenye mechi kama hii, huwezi kupumzika, hakika tulistahili ushindi. Ni vigumu kucheza ugenini dhidi ya Bayern Munich kwa kuwa ni timu kubwa lakini najivunia mno kwa kile kilichofanywa na vijana wangu," amesema Klopp akiwaambia waandishi wa habari.

"Jordan Henderson amejitonesha jeraha lake lakini natumaini hatokuwa sana, bao la kwanza nitatamani kuliangalia zaidi ya mara 1,000.

"Sehemu ya ulinzi ilikuwa iko vizuri na hatukujilinda kama vile tunavyofanya siku zote kwenye michezo yetu ya ugenini, Virgil van Dijk ametupatia muunganiko mzuri hasa kwenye mipira iliyokufa na ni hatari."

"Nilijua tungepata nafasi lakini sikuwa na uhakika kama ingetokea, lakini vijana wangu wameitengeneza na ilikuwa kitu kizuri kwetu."

"Sikutaka kuishushia kichapo Bayern, lakini nilihitaji ushindi kwa Liverpool. Ninahakika nitakuwa na mashabiki wengi wenye furaha kutoka Dortmund na kama nitaweza kuwasaidia basi itakuwa bora pia.

# *Sanchez akubali kuondoka United*

**MANCHESTER,** England

MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Alexis Sanchez, amekubali kuondoka ndani ya klabu yake hiyo kutokana na kukosa nafasi ndani ya kikosi cha kwanza.

Sanchez ameripotiwa akisema kuwa ataondoka kwenye timu hiyo baada ya kupona majeraha yake ya mguu anayosumbuliwa kwa sasa na anatambua hakuna ni timu chache ambazo zimekuwa zikimuhitaji kwa sasa.

Ole Gunnar Solskjaer, Kocha wa Manchester United yupo tayari kumruhusu Sanchez kuondoka baada ya kuona hawezi kuingia kwenye mpango wake moja kwa moja.

Tangu ajiunge na United msimu uliopita katika dirisha dogo akitokea Arsenal ametupia mabao matatu pekee na kucheza michezo 29 tu.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# KOCHA MOURINHO AMKUBALI ZIDANE

## Aeleza uamuzi wa kumrejesha ni sahihi kwa Madrid na Mfaransa huyo...

**LONDON,** England

KOCHA Jose Mourinho, amesema kuwa hajahuzunika baada ya mabosi wa Real Madrid kutangaza kumrejesha katika nafasi ya ukocha, Zinedine Zidane na kumwelezea Mfaransa huyo kuwa ndiye "chaguo sahihi" katika kuiongoza klabu hiyo.

**Zidane amereja katika klabu hiyo ikiwa ni miezi tisa baada ya kuamua kustaafu kuifundisha timu hiyo maarufu kwa jina la Los Blancos ili kurithi mikoba ya Santiago Solari, ambaye alitimuliwa wiki mbili baada ya kupoteza mchezo wa El Classico.**

Pia Madrid ikipokea kichapo kingine cha mabao 4-1 kutoka kwa Ajax ikiwa nyumbani.

Kichapo hicho kiliwaondoa vigogo hao katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na Kombe la Mfalme na kuwa nyuma kwa tofauti ya pointi 12 dhidi ya vinara wa La Liga, mahasimu wao Barcelona.

Mourinho ambaye tangu mapema Januari mwaka huu, alikuwa akihusishwa na mpango wa kurejea katika klabu yake hiyo ya zamani ya Real Madrid au Inter Milan itakuwa ni heshima kwake lakini akaongeza kwamba hana tatizo lolote baada ya Zidane kurejea katika nafasi hiyo.

"Hapana! Kwa nini nichukie?" alijibu kocha huyo, alipoulizwa na mwandishi wa habari wa kituo cha televisheni cha El Chiringuito.

"Sijawahi kusema kuwa au ninatarajia kurejea kuifundisha Madrid. Nafikiria ni sahihi, kwa upande wangu iko vizuri."

"Nafikiria uamuzi wako uko sawa kwa sababu ni kocha ambaye amepata mafanikio na amefanya vizuri kwa miaka mitano. Ni uamuzi sahihi kwa Madrid, ni uamuzi sahihi kwake pia.

"Ni nafasi nyingine muhimu na kubwa kwake kuthibitisha kuwa yeye ni mzuri kiasi gani, kwa sasa akiwa na mchakato mpya. Nafikiri ni jambo jema. Ninaitakia kila la kheri klabu hiyo."

Mourinho, ambaye ameshinda taji la La Liga na Kombe la Mfalme katika miaka yote mitatu aliyokaa Bernabeu, na amekuwa nje ya mpira tangu Desemba mwaka jana alipotimulia kuiongoza Manchester United.

Katika utawala wake wa kwanza, Zidane aliiongoza Madrid kushinda mara tatu mfululizo taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, na pia taji la La Liga mwaka 2017.

## ZISIKUPITE

### DORTMUND: SANCHO HAONDOKI

WINGA wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho, ambaye anatakiwa na Manchester United lakini Mkurugenzi wa Michezo wa klabu hiyo ya Ujerumani, Michael Zorc, amesema kuwa nyota hiyo raia wa England mwenye umri wa miaka 18 ataendelea kucheza katika Ligi ya Bundesliga msimu ujao. ***(Mirror)***

### POGBA KUBAKI UNITED

KIUNGO wa Manchester United, Paul Pogba (25), amebadilisha uamuzi wake wa kuondoka Old Trafford katika kipindi cha majira ya joto baada ya kufanya mazungumzo na kocha wa muda wa timu hiyo, Ole Gunnar Solskjaer. ***(Sun)***

### UNITED YAKUBALI KUSHINDWA

MABOSI wa United wamesema kuwa mbio za kumwania kiungo wa Barcelona, Ivan Rakitic ambaye ana umri wa miaka 31 zimekufa kutokana na uwezekano wa kumpata kuwa mdogo. ***(Evening Standard)***

### KLOPP ATAJWA BAYERN

RAIS wa zamani wa Bayern Munich, Franz Beckenbauer amemtaja Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp ndiye anafaa kupewa mikoba ya kuiongoza timu hiyo inayoshiriki Ligi ya Bundesliga. ***(Goal)***

### HAZARD AICHANGANYA CHELSEA

MSHAMBULIAJI wa Chelsea, Eden Hazard "hajasema chochote kuhusiana na Real Madrid", imeelezwa na mchezaji mwenzake, Willian. Mbelgiji huyo mwenye umri wa miaka 26 anahusishwa na mipango ya kuhamia katika klabu hiyo ya La Liga. ***(Mail)***

### NEYMAR KUFUNGIWA

MSHAMBULIAJI wa Paris St-Germain, Neymar (27), huenda akafungiwa kucheza mechi tatu za hatua ya makundi katika msimu ujao wa mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kufuatia maneno aliyoyasema baada ya timu yake kufungwa na Manchester United. ***(Times - subscription required)***

### RODGERS MAMBO SAFI

LEICESTER City imemlipa Kocha Brendan Rodger. na wasaidizi wake kama fidia baada ya kuamua kumfukuza kazi. ***(Telegraph)***

### ICARDI AJIPANGA KUONDOKA

JUVENTUS na Real Madrid zinatajwa kuwa mahali sahihi kwa straika wa Inter Milan, Mauro Icardi. Straika huyo mwenye umri wa miaka 26 hajacheza mechi yoyote ya ushindani tangu Februari ambapo alivuliwa kitambaa cha unahodha. ***(TyC Sports, via Calciomercato)***

### ALDERWEIRELD AKARIBIA UTD

MANCHESTER United imepewa nafasi kubwa ya kumsajili beki wa Tottenham, Toby Alderweireld ambaye ada yake ya usajili iliyotajwa katika mkataba wake ni pauni milioni 26. ***(Mirror)***

### BENITEZ AWEKWA MTEGONI

KOCHA Rafa Benitez ameelekezwa kusajili wachezaji chipukizi endapo atakubali kusaini mkataba mpya wa kuendelea kuifundisha Newcastle. Kocha huyo wa zamani wa Liverpool anaonekana atakumbana na ushindani wa kumnasa straika wa West Brom, Salomon Rondon (29) kumpa mkataba wa kudumu. ***(Mirror)***



Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS), Eng. Patrick Mfugale (wa kwanza kulia aliyevaa kofia), akiwaonyesha wajumbe kutoka Moroco na wageni wengine eneo la Nzuguni, Dodoma ambalo uwanja wa kisasa utajengwa hapo hivi karibuni. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# MKUDE AELEZA NAMNA SIMBA ITAKAVYOSHINDA

**Na Faustine Feliciane**

WAKATI ikiwa imebaki siku moja kabla ya mchezo wa mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kuchezwa, kiungo wa Simba, Jonas Mkude, amesema anaamini wachezaji wenzake watakaopangwa katika mechi hiyo watapambana na kuhakikisha "wanakisambaratisha" kikosi cha AS Vita.

**Simba inatarajia kuwakaribisha AS Vita katika mechi yake ya mwisho ya Kundi D itakayochezwa kesho kuanzia saa 1:00 usiku kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.**

Mkude, nahodha wa zamani wa Simba hatacheza mechi hiyo kutokana na kutumikia adhabu ya kadi mbili za njano.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkude alisema kuwa maandalizi ya mchezo huo yamekuwa bora zaidi kuliko walivyofanya katika mechi nyingine kwa sababu wanahitaji ushindi na si matokeo mengine.

"Nitaukosa mchezo wa Jumamosi, lakini Simba ina wachezaji wengi wenye uwezo mkubwa, nina imani wachezaji wenzangu watapambana kwa ajili ya timu ili ipate ushindi, kila mmoja anafahamu umuhimu wa mchezo huu ambao tunaucheza kwenye uwanja wa nyumbani," alisema Mkude.

Aliongeza kuwa ndoto ya wachezaji wote wa Simba ni kuona wanatinga hatua ya robo fainali ya michuano hiyo na wanafahamu wanachohitaji ni matokeo ya ushindi pekee.

"Kikubwa ninachoweza kusema ni mashabiki kujitokeza kwa wingi uwanjani, tupo nyumbani na wao wanajua umuhimu mkubwa sana kwetu kuweza kufanya vizuri," alisema kiungo huyo ambaye alipandishwa akitokea katika timu ya vijana ya umri chini ya miaka 20 (Simba B).

Tayari kikosi cha AS Vita kimeshawasili nchini kwa ajili ya mchezo huo ambao utatanguliwa na mechi nyingine ya kundi hilo kati ya Al Ahly dhidi ya JS Saoura itakayochezwa Misri.

Mara ya mwisho Simba kutinga hatua ya robo fainali ilikuwa ni mwaka 2003, wakati klabu hiyo ilikaa miaka 15 ili kucheza tena hatua ya makundi.

# Ngorongoro Marathon kumwaga medali

**Na Renatha Msungu**

WANARIADHA 1,000 wa kwanza watakaofanikiwa kumaliza mbio za Ngorongoro Marathon zitakazofanyika Aprili 20 mwaka huu, kila mmoja atapewa medali yake kwa kushiriki mbio hizo, imeelezwa.

Mratibu wa mbio hizo za kila mwaka, Meta Petro alisema jana kuwa medali hizo zinatarajia kutua nchini wakati wowote, kuanzia na lengo la kuwapa wanariadha hao ni kuongeza hamasa.

Petro alisema kuwa maandalizi ya mbio hizo yako katika hatua za mwisho na zimepangwa kuanzia katika lango Kuu ya kuingilia na kutokea kwenye Hifadhi ya Ngorongoro na kumalizikia kwenye viwanja vya Mazingira Bora mjini Karatu.

Alisema jana kuwa mbio za mwaka huu zitakuwa na msisimko wa aina yake na zawadi zitaongezwa tofauti na zile zilizotolewa mwaka uliopita.

"Mbio za mwaka huu zitashirikisha wanariadha wengi kutoka ndani na nje ya nchi kutokana na uhamasishaji uliofanywa na waandaaji, " alisema mratibu huyo.

Alitaja ada kwa wanariadha wanaotaka kushindana katika mbio za kilomita 21 ni Sh. 20,000 wakati zile za kujifurahisha za kilomita tano ni Sh. 10,000 wakati watoto watapewa namba za ushiriki kwa kutoa kiasi cha Sh 5,000.

"Tayari kuna shule zaidi ya tano za jijini Arusha zimethibitisha kuleta wanafunzi ambao idadi yao itakuwa ni zaidi ya 100 ili kushiriki mbio hizi lakini wao watachuana katika umbali wa kilomita mbili na nusu, " Petro alisema.

**MSIMAMO LIGI KUU BARA**

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Yanga | 27 | 21 | 4 | 2 | 45 | 18 | 67 |
| 2. Azam | 27 | 16 | 8 | 3 | 42 | 18 | 56 |
| 3. Simba | 20 | 16 | 3 | 1 | 43 | 7 | 51 |
| 4. Kinondoni MC | 29 | 9 | 14 | 6 | 32 | 20 | 41 |
| 5. Mtibwa Sugar | 28 | 12 | 5 | 11 | 29 | 21 | 41 |
| 6. Lipuli | 30 | 9 | 12 | 9 | 24 | 26 | 39 |
| 7. Coastal Union | 29 | 8 | 13 | 8 | 27 | 30 | 37 |
| 8. Mbao | 29 | 9 | 10 | 10 | 19 | 26 | 37 |
| 9. Mwadui | 30 | 10 | 6 | 14 | 34 | 37 | 36 |
| 10.JKT Tanzania | 30 | 8 | 12 | 10 | 18 | 24 | 36 |
| 11. Alliance | 29 | 9 | 9 | 11 | 23 | 30 | 36 |
| 12. Mbeya City | 28 | 9 | 7 | 12 | 28 | 32 | 34 |
| 13. Ruvu Shooting | 29 | 8 | 10 | 11 | 27 | 35 | 34 |
| 14. Kagera Sugar | 28 | 7 | 12 | 9 | 21 | 26 | 33 |
| 15. Stand Utd | 30 | 9 | 6 | 15 | 27 | 39 | 33 |
| 16. Ndanda | 28 | 8 | 9 | 11 | 17 | 29 | 33 |
| 17. TZ Prisons | 28 | 7 | 11 | 10 | 20 | 24 | 32 |
| 18. Singida Utd | 28 | 8 | 8 | 12 | 20 | 27 | 32 |
| 19. Biashara Utd | 28 | 6 | 9 | 13 | 20 | 29 | 27 |
| 20. African Lyon | 29 | 4 | 10 | 15 | 18 | 36 | 22 |

# *Mngazija, Is-haka wang'ara Zanzibar*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KAMATI ya mashindano ya Chama cha Soka Zanzibar (ZFA) imetangaza Kocha wa Selem View inayoshiriki Ligi Kuu Visiwani hapa, Ali bakari Mngazija kuwa Kocha Bora wa Februari.

Akizungumza na gazeti hili jana, Makamu mwenyekiti wa kamati hiyo, Hussein Ahmada alisema kuwa Mngazija alipata kura 40 huku mpinzani wake ambaye ni Kocha Mkuu wa KMKM, Ame Msimu, amepata kura 35

Ahmada alisema kuwa ili kumpata mshindi wa tuzo hiyo, kura zilipigwa kupitia mitandao ya kijamii inayoendeshwa na chama hicho ya akaunti za Twitter, Instagram pamoja na facebook kwa kuwapa wadau wake fursa ya kuteua mshindi.

Ahmada aliongeza kuwa katika kuchagua mshindi wa tuzo hiyo, makocha watashindanishwa kwa kuangalia vigezo mbalimbali ikiwamo kuangalia matokeo ya uwanjani katika mechi za mzunguko wa pili ambazo zimeanza hivi karibuni.

Mngazija amepewa zawadi ya cheti pamoja na Mchezaji Bora wa mwezi uliopita, Is-haka Omar ambaye pia anatokea Selem View baada ya kupata kura 30 dhidi ya Abdul Yusuph wa KVZ ambaye alipata kura 17.



Mourinho amkubali Zidane



Nahodha wa Barcelona, Lionel Messi (katikati), akiwa amekabwa na wachezaji wa Lyon, Fernando Marcal (kulia) na Marcelo katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyochezwa juzi usiku. Barca ilishinda 5-1.
**PICHA: MTANDAO**

# YANGA: LIPULI ITAKUFA HIVI

## Itashuka Samora bila ya Ajibu, Dante...

**Na Faustine Feliciane**

VINARA wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga, walitua salama mkoani Iringa jana jioni tayari kuwakabili wenyeji Lipuli Fc katika mchezo wa ligi hiyo utakaochezwa kesho lakini ikiwa bila ya nyota wake watatu wa kikosi cha kwanza.

**Nyota ambao itawakosa katika mchezo huo na wamebaki jijini Dar es Salaam ni pamoja na Ibrahim Ajibu, Andrew Vincent 'Dante' na Abdallah Shaibu 'Ninja' kutokana na sababu tofauti.**

Kukosekana kwa nyota hao hasa wachezaji wa safu ya ulinzi ya Yanga kupwaya kutawapa Lipuli FC nafasi ya kuondoka na pointi zote tatu kama washambuliaji wake watatumia vema nafasi watakazotengeneza.

Mratibu wa timu hiyo, Hafidh Saleh, aliiambia Nipashe kutoka Iringa kuwa nahodha wao, Ajibu, ameshindwa kusafiri na timu kutokana maumivu ya nyonga huku Ninja akiwa na adhabu ya kufungiwa kucheza mechi tatu.

"Dante ni majeruhi pia, hatukuweza kusafiri naye, Ajibu yeye alikuwa akilalamika maumivu ya nyonga hivyo hatoweza kucheza," alisema Saleh.

Naye Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Noel Mwandila, alisema licha ya kukosekana kwa wachezaji hao bado watapambana kuhakikisha wanapata matokeo mazuri kwa sababu wachezaji wengine waliobakia wana uwezo wa kutekeleza majukumu watakayopewa.

"Hatuwezi kusema hiyo itakuwa sababu ya sisi kutofanya vizuri, nawaamini wachezaji wote tuliokuja nao huku na kila mmoja atafanya kazi yake kuhakikisha tunatimiza tulichokikusudia, malengo yetu ni ushindi," alisema Mwandila.

Aliongeza kuwa wanawaheshimu Lipuli lakini wasitegemee wepesi kwa sababu ya kukosekana kwa nyota hao. Mwandila ataiongoza timu hiyo kutokana na Kocha Mkuu, Mwinyi Zahera kurejea kwao Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) ili kutekeleza majukumu yake ya Timu ya Taifa ya nchi ambayo yeye ni Kocha Msaidizi.

Yanga yenye pointi 64 inaongoza ligi hiyo yenye timu 20 wakati Lipuli wenyewe wako katika nafasi ya tano katika msimamo baada ya kujikusanyia pointi 41 baada ya kucheza mechi 30.

# Djuma awapeleka Simba robo fainali

**Na Somoe Ng'itu**

ALIYEKUWA Kocha Msaidizi wa Simba, Mrundi, Masoud Djuma, ameipa nafasi timu hiyo kusonga mbele katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa kuwafunga AS Vita kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), lakini amewataka wawe makini na watulivu zaidi.

Simba itakuwa mwenyeji wa AS Vita katika mechi ya mwisho ya Kundi D itakayochezwa kesho kuanzia saa 1:00 usiku kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Djuma alisema kuwa ili Simba wapate ushindi na watinge hatua ya robo fainali ya mashindano hayo yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF) wanatakiwa kuwadhibiti vema viungo na washambuliaji wa AS Vita.

Djuma alisema kuwa hakuna timu isiyofungika na Simba wanatakiwa kusahau matokeo waliyopata katika mchezo wa kwanza wakati walipokutana na Wakongomani hao.

Kocha huyo wa AS Kigali inayoshiriki Ligi Kuu Rwanda alisema kuwa faida ya kucheza nyumbani pia itawaongezea Simba nguvu ya kufanya vizuri katika mchezo huo utakaochezeshwa na waamuzi kutoka Morocco.

"Ni mechi ngumu lakini ninaipa Simba nafasi ya kushinda bao 1-0, kikubwa wawe makini kuwazuia AS Vita mbele na kati, hizo sehemu mbili wako vizuri," alisema mchezaji huyo wa zamani wa APR ya Rwanda.

**MAKAMBA KUONGOZA**

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara alisema kuwa wachezaji wao wanafahamu umuhimu wa mchezo huo ambao kauli mbiu yake ni "Do or Die" na kujipanga kuwapa furaha mashabiki wao.

Alimtaja Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), January Makamba ndiye atakuwa mgeni rasmi katika mchezo huo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >